**4 APRILI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Tatu – Tarehe 4 Aprili, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Tumaini Magessa.

Na. 28

### Jimbo la Busanda Kupata Halmashauri Yake

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza: -

Je, nini mkakati wa Serikali wa kulipatia Jimbo la Busanda Halmashauri, kwani michakato ya *DCC* na *RCC* iliwasilishwa TAMISEMI?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, mnaona eeh? Mheshimiwa Waziri sijamwita, amekuja. Hivi ndivyo ninavyotaka, namna hii. Usingoje kuitwa kwenye nchi kama hii ambayo inataka maendeleo ya haraka. Endelea. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Jimbo la Busanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita iliwasilisha maombi ya kupandishwa hadhi Jimbo la Busanda kuwa halmashauri kwenda Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa barua ya tarehe 24 Machi, 2020. Maombi hayo yalifanyiwa kazi kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadaye kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Je, ni lini zoezi la uboreshaji maeneo yaliyopo litakamilika, ukizingatia jibu kama hili lilitolewa mwaka wa fedha uliopita?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Katika Jimbo la Busanda tuna Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katoro ambapo wakati tunapewa

mamlaka mwaka 2014 kulikuwa na watu 86,231, lakini leo hii tunavyozungumza baada ya sensa, tuna watu 231,332 ikiwa ni ongezeko la watu 144,000. Tunakusanya mapato kama shilingi bilioni 1.3, tuna shule za msingi 24 na shule za sekondari 16. Je, nini mkakati wa Serikali kuipandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo ya Katoro kuwa Halmashauri ya Mji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa kuanzisha mamlaka mpya katika maeneo mbalimbali kote nchini ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. Kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele kuboresha kwanza miundombinu, majengo ya Utawala, ofisi na majengo mengine ya huduma za kijamii katika mamlaka ambazo zipo ili ziweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baada ya kukamilisha zoezi hilo la kuwezesha miundombinu, tutakwenda kuanzisha mamlaka nyingine. Kwa hiyo, tamko la Serikali litatolewa muda ukifika kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusiana na kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Katoro ambayo ni mamlaka ya mji, hili nalo linaenda sambamba na jibu langu la msingi kwamba baada ya kukamilisha taratibu hizo, basi tutaona namna ya kufanya kama itakidhi vigezo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Flatei.

Na. 29

**Posho za Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji, Mitaa na Madiwani**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawalipa posho Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji na kuongeza posho ya Madiwani ili kuwasaidia kutekeleza majukumu yao kikamilifu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. Serikali imeendelea kulipa posho za Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao ipasavyo. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga shilingi bilioni 1.7 ambapo kufikia Februari, 2024 shilingi bilioni 1.15 zimetolewa kwa ajili ya kulipa posho za Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga shilingi bilioni 20.8 kwa ajili ya kulipa posho za Waheshimiwa Madiwani katika halmashauri 168 ambapo kufikia Februari, 2024 kiasi cha shilingi bilioni 13.5 kimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuongeza na kuboresha vyanzo vyake vya mapato ili kuendelea kulipa posho za Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa kwa ufanisi zaidi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naleta swali hili kwa mara ya sita, lakini nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri ajue Mbulu Vijijini, Wenyeviti wa Vitongoji hawajawahi kupata hizi posho. Je, lini wanapata posho hizi ili kukidhi na kuweza kufanya shughuli zao kama swali langu linavyosema?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Niliwauliza, lini mnawaongezea posho Waheshimiwa Madiwani? Sikuuliza kama mnaendelea kuwalipa, nimeuliza, "lini"? Naomba jibu, lini mnawaongezea posho Waheshimiwa Madiwani ili waweze kufanya kazi kama inavyostahili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Flatei Massay, ni kweli ameuliza swali hili mara kadhaa kwa nia njema ya kutaka kuona Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa wanapata posho zao za kila mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inathamini sana kazi za viongozi hao. Ndiyo maana imeendelea kutenga fedha kupitia Serikali Kuu na mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vitongoji vya halmashauri hiyo ambavyo havijalipwa, nimwelekeze Mkurugenzi wa Mbulu Vijijini kuanza kutenga fedha kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza kulipa posho kwa kadri ya maelekezo ya Sheria na Miongozo iliyopo ili viongozi hao wapate posho zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu hoja ya lini tunapandisha posho za Waheshimiwa Madiwani, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya kuona uwezo wake wa kifedha na baadaye itatoa

tamko kuhusu namna gani tunakwenda kulifanyia kazi suala hilo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa Serikali inatenga fedha nyingi kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kwa sababu tunajua umuhimu wa wenyeviti hawa, ni lini tutaona umuhimu wao kwa kuwalipa posho isiwe fedha kama sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba posho za viongozi hao ambao ni Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa siyo fedha. Zipo kwa mujibu wa Mwongozo na Serikali inahakikisha inalipa wenyeviti hao kwa kadri fedha zinavyopatikana. Changamoto iliyopo ni uwezo wa halmashauri zetu kulipa wenyeviti wote kwa wakati, ndiyo maana Serikali inaendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuwezesha halmashauri kukusanya zaidi ili ziweze kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwasisitiza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kuongeza uwezo wa halmashauri na kuweka kipaumbele katika kuwalipa viongozi hao. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Nusrat.

Na. 30

**Upungufu wa Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari Ikungi**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kumaliza tatizo la uhaba wa Walimu Shule za Sekondari na za Msingi katika Wilaya ya Ikungi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Hanje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitatu 2021 hadi 2023, Serikali iliajiri jumla ya walimu wa shule za sekondari 13,128 na walimu 16,751 wa shule za msingi na kuwapangia vituo kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho cha miaka mitatu, 2021 hadi 2023 Serikali imeajiri na kuwapanga jumla ya walimu 314 katika Halmashauri ya Ikungi. Kati yao, walimu 240 ni wa shule za msingi na walimu 74 ni wa shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuajiri walimu na kuwapangia vituo mara baada taratibu za kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kukamilika kwa ajili ya kuongeza walimu katika maeneo yenye uhitaji mkubwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali, Jimbo la Singida Mashariki lina uhaba mkubwa wa walimu hususan walimu wa masomo ya sayansi ambapo mpaka sasa tunapungukiwa walimu 449. Hapo tunajumlisha shule za Munkinya, Choda, Mkiwa, Ikungi, Mungaa, Dung'unyi, zote. Sasa ni kwa nini Serikali isiweke mkakati madhubuti kwa ajili ya kuhakikisha Jimbo la Singida Mashariki linapata walimu wa kutosha kwa sababu ni wilaya ambayo inabeba majimbo mawili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Wilaya ya Ikungi ambayo ina majimbo mawili, imekuwa inatengewa fedha pungufu, sawa na wilaya nyingine ambazo zina jimbo moja, hususan kwenye miradi ya elimu. Ni kwa nini sasa Serikali isione umuhimu wa kuongeza fedha za miradi ya maendeleo katika Wilaya ya Ikungi kwa kuzingatia kwamba ina majimbo mawili na siyo jimbo moja (Singida Mashariki na Singida Magharibi)? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeendelea kufanya jitihada za kupeleka walimu wa masomo ya sayansi, hisabati na masomo mengine katika halmashauri zote ikiwemo Jimbo la Singida Mashariki. Katika ajira zilizopita, kipaumbele kilikuwa walimu wa sayansi na ajira zote ambazo zinafuata, walimu wanaopewa kipaumbele ni wa sayansi kwa sababu tuna upungufu mkubwa katika maeneo mbalimbali kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kupeleka walimu wa sayansi wa kutosha kwa awamu ili kupunguza pengo la walimu katika hamashauri hiyo na Jimbo la Singida Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na Halmashauri ya Ikungi kuwa na majimbo mawili na kwamba inapewa fedha sawa na halmashauri zenye jimbo moja, fedha za Serikali zinapelekwa kwa halmashauri. Kigezo ni halmashauri, kwa kuzingatia idadi ya watu, ukubwa kijiografia na mambo mengine. Kwa hiyo, pamoja na kwamba ina majimbo mawili, lakini vigezo vingine vyote vinakwenda *in favor* kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma wanazostahili. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Gwajima atauliza kwa niaba ya Mheshimiwa Kisangi.

Na. 31

**Kupeleka *Pipes* za Gesi Majumbani – Dar es Salaam**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaweka *pipes* za gesi Jijini Dar es Salaam kila nyumba ili wananchi wapikie nishati nafuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Jimbo la Kawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* imeshasambaza miundombinu ya gesi asilia katika nyumba 880 katika Jiji la Dar es Salaam. Pia imejenga bomba la gesi *(pipe)* lenye urefu wa kilomita 12.4 kutoka Mwenge hadi *Mbezi Beach* kupitia barabara ya Bagamoyo na tayari viwanda viwili na hoteli sita zimeshaunganishwa na bomba hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha wananchi wengi Jijini Dar es Salaam wanatumia gesi asilia, *TPDC* kwa kushirikiana na Kampuni ya *TAQA Dalbit* inafanya utafiti za mahitaji ya gesi asilia kwa njia za kusambazia utakaokamilika Julai, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti huu utaonesha namna bora ya kufikisha mabomba kwenye maeneo yenye changamoto na utabainisha maeneo gani yanayoweza kupelekewa mabomba na maeneo gani hayawezi kupelekewa mabomba ambapo njia nyingine zitatumika kuhakikisha gesi inawafikia wananchi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa mkakati wake wa kuhakikisha kwamba sasa tunakwenda kupata nishati safi na salama ya kupikia. Ni jambo kubwa, tunampongeza sana na wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wamelipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba, kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wamehamasika na wako tayari katika matumizi ya nishati safi ya gesi ya kupikia, lakini kwa kuwa changamoto kubwa ni gharama ya hiyo gesi na Serikali imeonesha mipango ya kusambaza gesi hiyo ambayo ina gharama nafuu kwa wananchi, je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuelekeza nishati hiyo au mabomba hayo kwenye maeneo yenye wananchi wengi kama Kawe, Mwenge, Mbagala, Manzese na maeneo mengine, badala ya ku-*base* kwenye eneo hilo hilo la *Mbezi Beach* na Mikocheni peke yake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tunao mpango wa kuhamasisha matumizi ya gesi asilia nchini, na kwa sasa hivi tunao mkakati wa kupeleka gesi kwenye nyumba takribani 10,000. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba

maeneo hayo ambayo ameyataja yenye watu wengi yatafikiwa na huduma hii ili waweze kutumia gesi kwa gharama nafuu zaidi kwa sababu gesi hii inayounganishwa majumbani ina unafuu zaidi kuliko gesi ile ya *LPG* ya mitungi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Serikali imehamasisha matumizi ya nishati safi na Watanzania wengi hasa wa vijijini wamehamasika, lakini bei, kwa maana ya gharama ya ujazaji wa gesi ni kubwa sana. Nataka kujua, nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha inatoa ruzuku ili kupunguza gharama za gesi kusudi wale wananchi maskini wa kijijini waache kutumia kuni na mkaa, watumie gesi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ambao tunaenda kuukamilisha hivi karibuni ili kuweka mkakati wa kukabiliana na changamoto zote ambazo zinawazuia wananchi wasiweze kutumia gesi katika kupikia. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, baada ya mkakati huu kukamilika, tutakuwa na mikakati madhubuti wa kuwawezesha wananchi wote kutumia gesi safi ya kupikia ili kupunguza matumizi ya mkaa na kuni.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda.

Na. 32

### Uhitaji wa Walimu Chuo cha *VETA* Kitangari – Newala Vijijini

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka walimu katika Chuo cha *VETA* Kitangari ili kuleta ufanisi wa elimu inayotolewa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Mtanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kupeleka Walimu katika Chuo cha *VETA* cha Kitangari kwa ajili ya kuleta ufanisi na tija katika elimu na mafunzo ya ufundi stadi yanayotolewa kwa wananchi wa Newala ili waweze kushiriki vema katika kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* imeshapeleka jumla ya walimu sita katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Newala kilichopo Kitangari ili kuwezesha utoaji wa mafunzo katika fani tatu zilizopo pamoja na masomo mtambuka. Aidha, katika ikama na bajeti ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imekasimia walimu watatu wa masomo mtambuka ambayo utekelezaji wake utafanyika baada ya kuidhinishwa utekelezaji wa ikama hiyo. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, napenda kufahamu mkakati ambao Serikali inao katika kuajiri watumishi ambao sio walimu. Kwa mfano, pale chuoni hakuna *matron,* hakuna *patron*, hakuna dereva wala wapishi, mkakati ukoje ili huduma ziweze kutolewa kwa ukamilifu katika chuo kile?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kupitia majibu ambayo Serikali imeyatoa, imeonesha kwamba fani ziko tatu, na ni kweli fani tatu tu ambazo zinatolewa kati ya fani nyingi ambazo tunatarajia zitolewe ili wanafunzi wengi au wananchi wengi wapate nafasi ya kupata ujuzi. Mfano, hakuna fani ya mafundi magari, hatuna fani ya ujenzi, hatuna fani ya uunganishaji wa vyuma pamoja na mabomba. Mpango wa Serikali wa kuongeza fani nyingine ukoje ili kuwakwamua wananchi wa Newala ambao wanahitaji fani hizi ili waweze kujiendeleza kimaisha? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna kuhusiana na suala la watumishi wasiokuwa walimu, naomba nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Maimuna kwamba kunapo mwezi wa Tatu mwaka huu, 2024 tayari tulishatangaza nafasi za watumishi wasiokuwa walimu kwa vyuo vyetu vyote vya *VETA*. Kwa hiyo, mara tu baada ya mchakato huu kukamilika, baadhi ya watumishi watakaopatikana tutawapeleka katika chuo hiki cha Kitangari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili kuhusiana na suala la kuongeza fani, Mheshimiwa Maimuna nadhani anafahamu kuna maboresho ambayo tunaendelea pale kwa maana ya ujenzi wa mabweni na ukarabati wa karakana pamoja na madarasa. Kwa hiyo, tutaendelea kuboresha kwanza miundombinu na baada ya uboreshaji huo wa miundombinu, utaratibu wa kuongeza fani sasa tutaweza kuufanya ili uweze kuendana na miundombinu iliyopo katika eneo hilo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Kilave.

Na. 33

**Ununuzi wa Magari ya Zimamoto Temeke**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua Magari ya Zimamoto kwa ajili ya Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Mchicha – Temeke?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, masuala ya "kwa niaba, na jina la Mbunge" yameshatolewa. Kwa hiyo, nenda moja kwa moja kwenye jibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunikumbusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na jitihada za kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepata jumla ya magari 12 ya Zimamoto na Uokoaji yaliyopatikana kutoka katika mkopo wa *Euro* milioni 4.9 kutoka katika Serikali ya Austria ambapo yatasambazwa katika vituo vilivyoainishwa, kikiwemo Kituo cha Temeke. Vituo vingine vitakavyonufaika ni pamoja na Ilala, Kinondoni, Dodoma, Mwanza, Morogoro, Mbeya, Arusha na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha taratibu zote za mkopo wenye masharti nafuu wa thamani ya Dola za Marekani milioni 100 kutoka Taasisi ya *ADEX* iliyopo Umoja wa Falme za Kiarabu *(UAE)* kwa ajili ya kupata vitendea kazi mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa magari 150 ya zimamoto na uokoaji kwa matumizi ya nchi nzima. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo, mara nyingi magari haya yanapokwenda kuzima moto, maji yanaisha katikati. Je, Serikali ina mkakati gani wa kununua maboza ya maji ambayo yataweza yakavutwa pale maji yanapokwisha kwenye magari ya kuzimia moto ili kutumika kuzima moto? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali itagawa lini magari haya ambayo ameyasema katika vituo mbalimbali ambavyo amevitaja vikiwemo Temeke, Ilala na Mikoa mingine? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilave, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika magari yaliyowasili pale Dar es Salaam tunayo magari maalum ya maboza ambayo kazi yake kubwa ni kubeba maji ya msaada pale ambapo yale magari ya oparesheni yanapoishiwa. Magari yale yana uwezo wa kubeba maji kuanzia lita 5,000 mpaka 10,000. Katika mazingira ya kawaida, mazingira yale yatasaidia sana katika kuboresha huduma za kuzima moto kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya swali lake la pili ambalo…

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Naam!

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mtayagawa lini hayo magari ambayo tayari yapo? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, yale magari yanasubiri tu utaratibu wa kuzinduliwa na baada ya uzinduzi wake, magari yale yataenda kwenye operesheni mara moja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, kutokana na ongezeko kubwa la watu katika Jimbo la Mbagala, Serikali haioni ipo haja ya kuanzisha Kituo cha Uokoaji na Zimamoto katika Jimbo hilo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chaurembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezingatia hilo na ndiyo maana unaona katika mpango unaokuja, tunaleta magari karibu 100 yatakayogawiwa nchi nzima na Mbagala tutaiangalia kwa upekee wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Miji wa Liwale ni Mji unaokua kwa haraka sana. Sasa tunahitaji kuwa na Kituo cha Zimamoto pamoja na vifaa. Ni lini Serikali itatuletea vifaa vya zimamoto kwenye Wilaya ya Liwale?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia swali dogo la Mheshimiwa Kuchauka, katika mpango unaokuja wa Wizara ya Mambo ya Ndani, ni kuhakikisha huduma hizi za zimamoto zinaimarishwa nchi nzima. Hivyo, tumechukua ombi lake na tutapita huko na kuangalia vile vigezo vinavyostahili kuanzisha Kituo cha Zimamoto katika Wilaya yake. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Waziri amesema kwamba kuna magari ambayo yatanunuliwa, katika Manispaa ya Shinyanga hatuna gari la zimamoto, tunatumia magari ya wadau. Je, Shinyanga itakuwa katika mgao huo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kwamba katika yale magari yatakayokuja awamu ya pili ambayo ni magari zaidi ya 100, yanalenga kuhudumia mikoa yote ya Tanzania na katika mazingira ya kawaida, Shinyanga itakuwemo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wetu wa Iringa, tunayo misitu katika Wilaya ya Mufindi na Kilolo na kumekuwa kuna na mioto inayojitokeza kila wakati. Tunaiomba Serikali iangalie katika huo mgao, basi isikose katika Mkoa wetu wa Iringa kutupatia gari la zimamoto. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la Mheshimiwa Mbunge limepokelewa na litafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hii siyo Wizara ya Mheshimiwa Waziri Pinda, lakini amejibu kama mwendokasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Antipas Mgungusi.

Na. 34

**Kuanza Kazi kwa Mkandarasi wa Barabara ya Malinyi kwa Mtindo wa *EPC+F***

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza:-

Je, lini Mkandarasi wa Barabara ya Lupilo, Malinyi, Kilosa kwa Mpepo hadi Londo ataanza kazi kwa mtindo wa *EPC + F*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara kwa utaratibu wa *EPC+F* unahusisha kufanya usanifu wa barabara kabla ya kuanza ujenzi. Kwa sasa Mkandarasi ameanza na anaendelea na usanifu wa kina. Aidha, Serikali na wakandarasi wanaendelea na taratibu za kupata fedha kwa ajili ya malipo ya awali kwa miradi yote ya *EPC+F* ukiwemo huu wa barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo hadi Lumecha Mkoani Ruvuma. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antipas.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini kwa sasa wakati tunasubiri mchakato huo, barabara ya Malinyi imefungwa, haipitiki kwa maana ya barabara ya *TANROADS.* Je, Serikali ipo tayari kupeleka fedha za dharura kwa Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa kwa ajili ya kutatua dharura hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *TANROADS* tayari wanaendelea na shughuli za kuifungua barabara. Tulituma fedha za awali, na tayari Meneja wa Mkoa wa Morogoro, mkoa ambao umeathirika sana, ameishaingiziwa fedha tangu jana kwa ajili ya kuendelea kufungua barabara ambazo zimejifunga. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mlowo – Chitete – Kamsamba ilitengewa bajeti mwaka huu wa fedha 2023/2024 na sasa hivi tumebakiwa na miezi miwili tu. Swali langu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba, tutarajie kuna

pesa yoyote atatupelekea kuanza kujenga kilomita zozote au ndiyo tunyamaze hivyo hivyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya Mlowo – Kamsamba tayari imeshapata kibali, itatangazwa muda siyo mrefu ili tuanze kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa taratibu zote zimeshakamilika kwa hiyo barabara ya Mlowo – Kamsamba, nilitaka kujua sasa, lini itatangazwa rasmi ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyomjibu Mheshimiwa Condester Sichalwe, ndiyo barabara hiyo hiyo kwamba tutaitangaza muda wowote ili ianze kujengwa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Masasi – Nachingwea ilisainiwa mkataba kwa utaratibu wa *EPC+F,* ni lini itaanza kujengwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi la swali hili, barabara zote za *EPC+F* tunategemea zilishasainiwa na tumesema kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha itakuwa tayari wakandarasi

wameshaanza kwenda *site* kwa ajili ya kuanza kuzijenga. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 20 Machi, Makamu wa Rais alifanya ziara Jimbo la Hai na aliagiza kutekelezwa kwa ahadi za Mheshimiwa Rais za Ujenzi wa barabara ya Kwasadala – Kware – Remira, Kwasadala - Bwani na Bomang'ombe - *TPC*. Je, ni lini sasa ujenzi wa barabara hizi utaanza? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, barabara hii tutaiingiza kwenye bajeti kwa sababu zilikuwa zinafanyiwa usanifu, zianze kufanyiwa usanifu ikiwa ni maandalizi ya kuzijenga hizo barabara kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya *Usa River* kwenda mpaka Oldonyosambu ujenzi wake ulisimama kwa muda mrefu baada ya kufika lango la *ANAPA*. Je, ni lini Serikali itaendelea na ujenzi huo kutoka Ngarenanyuki hadi Oldonyosambu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusaidiana na wenzetu wa TAMISEMI, barabara hii ni kweli ilisimama, lakini tunaendelea kutafuta fedha ili mvua itakapokatika, basi tuendeleze kuijenga hiyo barabara. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Kilolo kupitia Kidabaga kwenda Idete hadi sasa haipitiki kutokana na maporomoko. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za dharura kwa ajili ya kuifanya ile barabara iweze kupitika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, halafu Mheshimiwa Kawawa jiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge alifika ofisini na tayari Mheshimiwa Rais ameshatoa fedha za dharura. Kwa hiyo, Meneja wa Mkoa wa Iringa ameshapewa maelekezo aende akafungue hiyo barabara ambayo imejifunga. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara ile ya Mtwara – Pachani ambayo inakwenda mpaka Nalasi upande wa Tunduru, ni barabara ya kiulinzi pia. Je, ni lini hasa Serikali itaanza kuijenga barabara ile kwa lami kama ilivyoahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi 2025? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja yenye urefu wa kilomita 300, Serikali inachofanya sasa hivi ni kuhakikisha kwamba inapeleka fedha kwa ajili ya kuijenga kwa lami ama kwa zege na kutengeneza madaraja ili iweze kupitika kwa mwaka wote wakati Serikali inafuta fedha ya kujenga barabara yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 51(4), maswali ya nyongeza hayatazidi matatu. Nimeruhusu maswali manane kwa sababu najua huko Majimboni kumewaka moto. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Utalii. Mheshimiwa Gulamali, kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Almasi.

Na. 35

**Adhabu kwa Watumishi wa *TFS* Wanaodhuru Raia na Mali Zao**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE K.n.y. MHE. SEIF K. GULAMALI** aliuliza:-

Je, ni adhabu gani inatolewa kwa Watumishi wa Wakala wa Huduma za Misitu *(TFS)* wanaobainika kudhuru raia na mali zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Misitu Sura 323 imeweka makatazo ambayo mtu yeyote anayekiuka makatazo hayo anakuwa ametenda makosa ya jinai na hivyo kulazimika kuchukuliwa hatua za kisheria. Aidha, katika utekelezaji wa majukumu hayo, watumishi wanatakiwa kuzingatia sheria, kanuni na misingi ya haki za binadamu. Hivyo, endapo mtumishi atabainika kudhuru raia au mali zake, atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 na kanuni zake pamoja na Amri za Kudumu za Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu za Mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo mtumishi wa *TFS* atabainika kukiuka masharti ya kazi na kama atakuwa ametenda kosa la kijinai na kinidhamu, mwajiri atamfungulia mashtaka kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma zikisomwa pamoja na kifungu cha 9(3) cha Amri za Jeshi la Uhifadhi za Mwaka 2022. Pindi mtumishi huyo akikutwa na hatia, anaweza kufukuzwa kazi, kupunguziwa mshahara au kushushwa cheo na mshahara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almasi.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kulipa fidia kutokana na madhara wanayopata raia kwa vitendo vya baadhi ya watumishi wabaya wa *TFS*? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas vipi? Saumu imekushika asubuhi? Mheshimiwa Waziri, umemsikia? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yote ya haki za binadamu yanatekelezwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo. Nimhakikishie Mheshimiwa Almasi, pale watumishi wetu watakapokuwa wamefanya makosa chini ya sheria hizo, fidia stahiki zitatolewa kwa mujibu wa sheria iliyopo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itawalipa fidia kwa kifuta machozi kwenye Vijiji vya Hunyari, Kihumbu, Mariwanda, Sarakwa, Mugeta Kyandege na Tingirima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, jibu swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo kwenye hatua za mwisho za kufanya uhakiki na uthamini wa madai ambayo tumeyapokea na pindi uthamini huo utakapokamilika, tutawalipa wahusika haraka iwezekanavyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa *Eng.* Mwanaisha Ulenge.

Na. 36

**Kufufua Viwanda Vilivyokufa – Tanga**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kufufua viwanda vilivyokufa katika Mkoa wa Tanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya kufufua viwanda vilivyokufa ukiwemo Mkoa wa Tanga, kwa kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wamiliki wa viwanda vilivyobinafsishwa, wenye nia ya kuviendeleza, kuvirejesha Serikalini na kuvitangaza upya kwa njia ya zabuni ya wazi; viwanda vilivyobinafsishwa kwa wamiliki walioshindwa kuviendeleza kabisa; na pia kuendelea kuvutia wawekezaji wapya wa kujenga viwanda vipya kwa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ulenge.

**MHE. *ENG.* MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza ni kwamba Sheria ya Kodi na Sheria za Uwekezaji hazisomani, kwa maana miradi mingi inafunguliwa lakini wawekezaji hawafanyi hivyo kwa sababu hakuna vivutio. Je, ni lini Serikali italeta hapa sheria hizo ili ziweze kupitiwa upya na ziweze kusomana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Shirika la *UNDP* limewezesha mikoa mbalimbali kuanzisha miongozo ya uwekezaji, na kule Tanga tumeanzisha na tumeanza kuzindua miongozo ile ya uwekezaji. Ni nini sasa Serikali inafanya baada ya miongozo ile kuenea Tanzania nzima ili dhamira ile ya kuanzisha viwanda iweze kutimia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli bado kuna changamoto kwenye baadhi ya sheria na pia kwenye sera za uwekezaji. Serikali imeishaanza kupitia sheria mbalimbali za taasisi zetu, sheria za kodi, na vile vile tumeanza kuboresha au kuhuisha sera zetu mbalimbali ikiwemo Sera ya Uwekezaji, Sera ya Viwanda na Sera ya Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, haya niliyosema ndiyo ambayo Serikali tunafanya sasa ili kuhakikisha sera zetu na sheria zetu zinaendana na mahitaji sahihi kulingana na uhalisia wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kama nilivyosema, tumeshaanza kutengeneza miongozo mbalimbali ya uwekezaji na miongozo hii au makongamano haya yamekuwa yakifanyika katika mikoa mbalimbali ikiwemo Mkoa wa Tanga. Matokeo haya katika Mkoa wa Tanga mahususi ni kutengwa kwa maeneo. Kwa mfano, maeneo yale kongwe ya maeneo ya uwekezaji 68, haya yamewekwa kwa ajili ya kujenga viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, miongozo hii sasa imeshaanza kuzaa matunda, na wawekezaji wengi wameshaanza kuonesha nia ya kuwekeza katika nchi yetu, na pia katika Mkoa wa Tanga ambako Mheshimiwa Mbunge ameuliza.  Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:**  Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, sana. Jibu la Serikali linatia matumaini. Naomba kufahamu katika mwendelezo huo wa kufufua viwanda, je, Viwanda vya Losaa Kilimanjaro, Kilimanjaro *Machine Tools, Moshi Leather* na Kilimanjaro *Utilization* viko katika mpango huo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika mikakati ambayo tumeiweka ni pamoja na kufufua viwanda. Kiwanda hiki cha Losaa ambacho tayari tumeshapeleka Shirika letu la Maendeleo ya Viwanda Vidogo Tanzania *(SIDO),* wameshaenda kufanya tathmini ya namna ya kufufua kiwanda kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kilimanjaro *Machine Tools* tayari tumeshaweka mitambo mipya mbalimmbali ambayo inafanya kazi, na tunaendelea kuongeza kwa kuweka bajeti katika mwaka huu ili kununua mitambo mingine ya kuyeyusha chuma katika kuhakikisha vipuri mbalimbali vinatengenezwa katika viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaenda hatua kwa hatua kuhakikisha kuwa viwanda vyote ambavyo vilikuwa vimekufa vinafufuliwa na hasa katika Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Mipango, Ofisi ya Rais.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu niongezee kwenye majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri pale kwa Mheshimiwa Eng. Ulenge kwamba, sasa hivi katika *reform* za Mashirika ya Umma, tunaunganisha taasisi ambazo zinahusika na uwekezaji kwa maana ya *TIC* na *EPZA*. Kwa kufanya hivyo, tutazipitia upya sheria zote husika na yale Mheshimiwa Mbunge aliyoyasema tutayaangalia. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Nollo.

Na. 37

**Kituo cha Madume Bora ya Ng'ombe – Bahi**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha Kituo cha Madume Bora ya Ng'ombe Wilayani Bahi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Mabadiliko ya Sekta ya Mifugo wa Miaka Mitano Kuanzia Mwaka 2022/2023 hadi Mwaka 2026/2027. Aidha, kupitia mpango huo, uboreshaji wa mbari za ng'ombe unafanyika kupitia matumizi ya madume bora na uhimilishaji ambapo kwa upande wa madume, Wizara imesambaza bure madume bora ya ng'ombe wa nyama 366 kwenye vikundi vya wafugaji katika halmashauri nane ili kuzalisha mifugo yenye tija zaidi ile ya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Wizara kwa sasa ni kusambaza madume bora ya ng'ombe kwa vikundi vya wafugaji ili kuboresha mifugo yao badala ya kuanzisha vituo vya madume. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imepanga kununua madume bora 200 yatakayosambazwa kwa vikundi vya wafugaji, wakiwemo wafugaji wa Halmashauri ya Bahi ambao watapewa madume 20. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naishukuru sana Serikali kwa ahadi ya kunipatia madume 20 ya ng'ombe katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza. Kiasi hiki cha madume 200 ambayo Serikali inanunua ukilinganisha na idadi ya ng'ombe tuliyonayo ni hatua kidogo sana. Kwanza, hata hayo madume yenyewe tunayachosha kwa maana ya wingi wa majike yaliyopo. Je, Serikali haioni kwamba badala ya kununua madume 200 tuongeze tufike angalau hata 1,000 ili nchi nzima katika maeneo ya wafugaji tuweze kupata madume mengi na kwa uhakika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Dodoma tuna Kituo cha Utafiti wa Malisho pale Mpwapwa na hapa Kongwa, lakini ukija katika Wilaya yangu ya Bahi kwenye kata za wafugaji ukianzia pale Chifutuka, Chipanga na Chikora, hakuna hata nyasi moja ya utafiti ambayo imeletwa katika wilaya yetu. Je, Serikali ina mpango gani wa vituo hivi ambavyo vina miaka mingi, lakini taarifa zake na matunda yake hayafiki katika wilaya zinazovizunguka? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hili la madume 200. Ni kweli madume 200 ni wachache na mpango wa Serikali ni kuongeza kadri ya upatikanaji wa bajeti. Tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko tayari kuongeza madume hao kadri ambavyo bajeti inapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili la nyasi, tayari wataalam wetu wanaendelea na utafiti katika maeneo mbalimbali ya nchi, ukiwemo Mkoa wa Dodoma. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mara tu utafiti utakapokamilika, basi mbegu za nyasi bora zitakwenda katika Jimbo lake la Bahi. Kwa sasa watafiti wetu wanafanya utafiti katika maeneo mbalimbali ikiwa ni Mkoa wa

Morogoro, Mkoa wa Dodoma na maeneo mengine, na Bahi pia watafika kwa ajili ya kukamilisha utafiti huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutakuja Bahi kwa ajili ya kukamilisha utafiti huo na majibu yatakapopatikana, wataalam wetu wako tayari kutoa elimu kwa wafugaji wetu ili waweze kutumia nyasi hizo zinazotakiwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magige, halafu Mheshimiwa Asia jiandae.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itajenga Kiwanda cha Nyama na Malighafi za Mifugo Wilayani Ngorongoro kwa kuwa 80% ya wananchi katika wilaya hii ni wafugaji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa Kiwanda cha Nyama, Serikali inaendelea kuhamasisha wawekezaji mbalimbali katika maeneo mbalimbali ili kuwekeza katika sekta hii kwa sababu imeonekana viwanda hivi vina tija katika mazingira hayo. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge pia kama ana mawasiliano na wadau mbalimbali katika maeneo mbalimbali wanaoweza kuwekeza katika sekta hii, pia tuko tayari kushirikiana nao katika kuhakikisha kwamba viwanda hivi vinapatikana katika Taifa letu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, nini mpango wa Serikali kwa vikundi vya wafugaji wa Simanjiro, Kiteto na Hanang kuleta mbegu ya madume bora?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, ni kwamba madume bora yapo na katika bajeti ya mwaka huu pia tutaongeza idadi ya madume bora, na Wilaya ya Hanang, Kiteto, Simanjiro na maeneo mengine kote ambako wanahitaji madume bora, tuko tayari kuwapelekea. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa bei ya madume bora wamekuwa ni ghali sana hasa kwa hawa wa Serikali, kwa nini Serikali isipunguze bei sana ili wafugaji waweze kununua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli madume hawa bei yake ilikuwa iko juu. Ilikuwa ni shilingi 4,000,000/= mpaka shilingi 6,000,000/=, lakini kwa *concern* hiyo ya Mheshimiwa Mbunge, pia madume hao wameshashuka bei. Sasa madume hao wanapatikana kwa shilingi 1,000,000/= mpaka shilingi 1,500,000/=. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kupokea ushauri kama bei hiyo pia itakuwa bado inawatatiza wafugaji wetu, tuko tayari kuishusha na kuona namna ambavyo tutawasaidia wafugaji wetu katika maeneo mbalimbali. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mpango mzuri wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, madume bora wanapatikana, lakini ni ukweli usiopingika kwamba wapo ng’ombe wa asili, kwa mfano wenye asili ya Wafipa ambao wanapatikana ndani ya Mkoa wa Rukwa ambao *size* yake ni kubwa

na wanafanya vizuri kama wanyamakazi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba hatupotezi *specie* hii ambayo ni nzuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kuhamasisha ufugaji wa kisasa, na hawa ng'ombe wa asili anaowasema Mheshimiwa Mbunge kama wataonesha kuwa na tija, tuko tayari kuwalinda, lakini kusema kweli kwa sasa Wizara inajikita zaidi kwenye kuhamasisha ufugaji wa kisasa, wenye tija, wenye kutumia eneo dogo na kwa faida kwa ajili ya wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wataalam wanaendelea kufanya uchunguzi wa jambo hili na ikionekana mbegu hizi za Wafipa zina faida kwa wafugaji wetu, tuko tayari kuzilinda na kama zinaonekana hazina faida, ni vizuri wafugaji wetu wakajifunza kufuga kisasa kwa ajili ya faida yao ya baadaye. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali yamekwisha na kila Mbunge aliyesimama kapewa nafasi.

Sasa kuna matangazo ya wageni wetu. Kwanza niwape taarifa kwamba tunaye Kaimu Waziri Mkuu kwenye Bunge letu hili ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Ummy Mwalimu. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, nikianza na wageni waliokaa katika Jukwaa la Spika, ni wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge, ambao ni viongozi kutoka Benki ya *NMB* wakiongozwa na Ndugu Aziz Dachi, Mjumbe wa Bodi ya *NMB;* Ndugu George Mandepo, Mjumbe wa Bodi ya *NMB;* Ndugu Juma Kimori, Afisa Mkuu wa Fedha; Ndugu Alfred Shao, Afisa Mkuu, Wateja Wakubwa na Serikali; Bi. Vicky Bishubo, Mkuu wa Idara ya Biashara ya Serikali; Bi. Rahma Mwapachu, Mkuu wa Idara ya Masoko, Mawasiliano na Mahusiano; Bi. Lilian Kisamba, Meneja

Mwandamizi wa Mahusiano na Uwajibikaji kwa Jamii; Bi. Janeth Shango, Meneja Kanda ya Kati; na Bi. Grace Matemu, Meneja wa Tawi la Bunge. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, ambao ni wanafunzi wa Theolojia ya Upadri kutoka Chuo cha Upadri Kipalapala, Mkoa wa Tabora na Mtawa wa Shirika la Mt. Benedicto kutoka Jimbo Kuu la Mwanza. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga, ambao ni wapiga kura wake kutoka Kalenga Mkoa wa Iringa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 18 wa Mheshimiwa George Mwenisongole, ambao ni Madaktari na Wauguzi kutoka Hospitali ya Benjamini Mkapa ya Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 40 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka kutoka Taasisi ya *Tanzania One,* Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ambao ni marafiki zake aliosoma nao Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne katika Shule ya Sekondari Jitegemee ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 100 na walimu wanane kutoka *St. Florence Academy* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 65 na walimu 10 wa Shule ya Msingi Mt. Gemma Galgan ya Jijini Arusha. Karibuni. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni mmoja, Ndugu Ester Elisha Kweyamba, ni mjasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunaye mgeni mmoja wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Ma-*broker* wa Madini Tanzania (CHAMMATA) kutoka Jijini Arusha. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anawatangazia Wabunge wote kuwa utaratibu wa kuomba nafasi ya kuchangia hoja za Wizara mbalimbali ni kupitia Mfumo wa Bunge Mtandao. Mpaka sasa Wabunge ambao wameomba nafasi ya kuchangia hususan Bajeti hii ya Waziri Mkuu ambayo ilianza jana tarehe 03 Aprili, 2024 ni wachache sana.

Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote wenye nia ya kuchangia Bajeti hii ya Waziri Mkuu na bajeti nyingine, wanakumbushwa kufanya hivyo sasa kwa kutuma maombi yao kupitia Mfumo wa Bunge Mtandao. Maombi nje ya mfumo hayatashughulikiwa. Ukikwama kwenye mfumo, wapo wataalam wa TEHAMA kwenye Bunge watawasaidia kuweka majina humo.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea.

Tunaanza na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Makoa na Mheshimiwa Dkt. Pauline Nahato.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii uliyonipa ya kuchangia Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kuipongeza Serikali chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na viongozi wote akiwemo Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu na Viongozi wote wa Serikali kwa jinsi wanavyofanya kazi nzuri sana ya maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Sensa ya Watu. Sensa iliyopita inaonesha kwamba nchi yetu idadi yetu imeongezeka sana. Ni zaidi ya miaka 10 tulikuwa hatujafanya sensa, lakini nilikuwa na hoja katika eneo hilo kwamba baada ya sensa tumekuwa tuna maswali mengi humu hasa ya kuongeza maeneo ya utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mahali popote kama kuna watu wameongezeka hata kwenye familia zetu lazima kuna vitu vitabadilika tu, lakini baada ya sensa hii ukiangalia maeneo ya utawala, kwa mfano, kata zetu ni zile zile hata baada ya sensa hii, mitaa ni ile ile na vitongoji ni vile vile. Suala la utoaji huduma baada ya watu kuwa wameongezeka kwa kweli inakuwa ni shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iangalie upya suala la namna ya kugawa maeneo na kutenga bajeti ambapo itasaidia wananchi kupata huduma kwa urahisi baada ya sensa hii ya kuongezeka kwa watu, kwa sababu bado sehemu za utawala ni zile zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali hasa kwenye suala la umeme. Upatikanaji wa umeme ulikuwa ni mgumu sana katika kipindi kilichopita, lakini kwa sasa kuna unafuu mkubwa. Naipongeza sana Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameweza kushughulikia kwa kiwango kikubwa hili tatizo la umeme. Umeme ni uchumi na bila umeme shughuli nyingi zinasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, bado kuna tatizo. Hata juzi hapa tumeona tatizo la kukatika kwa umeme karibu nchi nzima, na moja ya sababu ambayo imetolewa ni kwamba maji sasa yamezidi, sijui mvua zimezidi, sasa maji yanakwenda kwenye mitambo, yanaharibu mitambo. Naishauri Serikali, wakati inanunua vitu hivi, nilitegemea kwamba suala hilo wangekuwa wameliona.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapotegemea kwamba mvua zitakuja katika kiwango kidogo, au unasikia kuna mafuriko na vitu kama hivyo, nilitegemea Serikali ingekuwa imechukua tahadhari kwamba maji hata yakizidi, basi mitambo isizimwe kwa sababu maji yamezidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona kwenye taarifa moja kwamba, hata mitambo ya Bwawa la Mwalimu Nyerere ilizimwa kwa sababu hiyo ya kwamba maji yalizidi yakawa yanaingia kwenye mitambo. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kuliangalia hilo kwa sababu kwa kweli halijakaa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa namna walivyoshughulikia suala la utwaaji wa maeneo, na hasa maeno yanayolizunguka Bunge. Niliangalia ile Taarifa ya Kamati ya Bajeti ukurasa wa 4 – 5, Serikali ilikuwa imetoa fidia ya shilingi bilioni 12.2 kwa ajili ya wale wakazi ambao wanazunguka maeneo ya Bunge, kwa maana ya taasisi mbalimbali. Wengine wameshaanza kuhama na wameshaondoka, lakini kuna baadhi bado wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taasisi kama *GPSA* bado wapo, pia *NFRA* bado wapo na Bodi ya Nafaka, pengine na taasisi chache. Naomba Serikali kwa sababu tayari imeshatoa fidia na hawa waliobaki waweze kuondoka ili sasa maeneo yaweze kufanyiwa shughuli ambazo Bunge imepanga kuzifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukue mfano wa wenzetu wa Kenya au Zambia, sisi hata wakija wageni wetu humu tunakutana

nao *canteen;* wakija wananchi wetu, tunakutana nao *canteen* au nje ya Bunge, lakini pia hata magari ya Waheshimiwa Wabunge mengi yanakaa nje na mengine mbali kabisa, kitu ambacho pia ni hatari, hakiko salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa hizi nchi nilizozitaja na nyingine, nadhani ni pamoja na Rwanda, maeneo ya Bunge ndiyo kuna Ofisi za Wabunge humo humo ambazo wanaweza kukutana na wapigakura wao maeneo ya Bunge. Hata vifaa vyao vya usafiri vinakuwa ndani ya maeneo ya Bunge. Kwa usalama, pia ni muhimu kwa maeneo hayo kuchukuliwa haraka ili yaweze kufanyiwa kazi ambayo ilikuwa imepangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la mbolea ya ruzuku na hasa mwaka jana, 2023. Mwaka jana Serikali kweli ilifanya kitu kizuri kutoa mbolea kwa wananchi katika sehemu nyingi. Hata hivyo, nikichukulia kilichotokea Tabora, maeneo mengi hasa kwenye jimbo langu la Tabora Mjini, mbolea ya ruzuku ilikuja lakini utaratibu wake wa kugawa ulikuwa hauko sawasawa kabisa. Wananchi wengi walipanga foleni hata siku mbili bila kupata mbolea, lakini na wengine waliishia kutokupata kabisa na usumbufu ulikuwa ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mliona mpaka kwenye vyombo vya habari wengine mpaka walikuwa wanalalamika kwamba walipata majeraha mbalimbali kwa ajili ya kugombania mbolea. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba, inapotoa tena mbolea ya ruzuku kama ilivyotokea mwaka jana, 2023 na siku nyingine basi utaratibu upangwe, uwe mzuri, ambao hautakuwa usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona nichangie hayo maeneo machache. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango wako. Niwakumbushe tena Waheshimiwa Wabunge, jioni kuna shughuli ya *NMB* ya futari. Kwa hiyo, msije mkasahau mkaondoka.

Namwita Mheshimiwa Makoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Nahato na Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami nichangie katika hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu. Pia naipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napitia hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nimeona namna Serikali ilivyopeleka fedha mfano kwenye hili Fungu 65, walipangiwa kwenye miradi ya maendeleo shilingi bilioni 14.7 na zimeenda shilingi bilioni 10 mpaka Februari, 2024. Ni jambo la kuipongeza Serikali, lakini ni vema pia Serikali ikaangalia sana hapa katika hili Fungu 65 kwamba, fedha hizi ziende kwenye programu za kusaidia vijana katika kuwapatia ujuzi na programu za kukuza kazi za staha kwa vijana kwa malengo yale yale ya kuwasaidia kuweza kujiajiri na kupata maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo basi, nilikuwa napitia hotuba hii nikaona kuna hii programu ambayo ilianzishwa ya kazi za staha ambayo asilimia 100 inategemea fedha kutoka kwa wafadhili. Kwa maana hiyo, walihitajika wapate shilingi bilioni 1.3 mpaka Februari, 2024, walipata shilingi milioni 310 peke yake. Jambo hili limesababisha programu yenyewe kutokuwa na tija na mwaka wenyewe wa fedha ndiyo huu unaisha, na ukiangalia hata hiyo shilingi milioni 300 imetumika kwenye kuboresha Sera ya Taifa ya Vijana, Hifadhi ya Jamii ikiwemo na fedha ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia programu hii, iko katika hatua za chini sana, lakini uhitaji kwa vijana katika mitaji na vitu kama hivyo ni mkubwa kwa ajili ya kutengeneza ajira. Kwa hiyo, ninaunga mkono ushauri wa Kamati ya kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ijikite zaidi kwenye kuwajengea uwezo na kuwapa ujuzi vijana pamoja na kujikita kwenye hiyo programu hasa ya kuwagusa wale vijana wenyewe kwenye hiyo *project*.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nilizoziona kwenye bajeti hii ya Wizara na nilivyopitia hotuba ya Kamati, inaonekana kwamba, bado tija haijaonekana juu ya hizi programu mbili ambazo ziliwalenga vijana. Kwa maana hiyo, sasa Serikali ijikite moja kwa moja kuhakikisha hizi *project* zinaleta tija kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengi na changamoto nyingi ambazo zinawa-*face* vijana na watu wenye ulemavu. Kwa maana hiyo, Serikali inatakiwa sasa iongezwe nguvu na juhudi kubwa katika kuhakikisha miundombinu inajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja, mimi niko Jimbo la Mjini Kondoa lenye Kata nane na mitaa 36. Vijana wa mjini wanatarajia wawekewe miundombinu mizuri kwa ajili ya kuendesha maisha yao. Mfano, miundombinu ya umeme bado utekelezaji wake upo chini sana. Kwa sisi ambao tupo kwenye Majimbo ya Mijini, umeme ni ajira kwa vijana, na umeme unawasaidia vijana kuweza kujitegemea katika shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukikuta mitaa ya mjini haina umeme halafu tunataka vijana waweze kujiajiri, haitawezekana. Maana yake mjini hatuna mashamba, tunatarajia tupate umeme na miundimbinu iliyoboreshwa ndiyo vijana waweze kujiajiri. Hata huo ufundi ambapo tunakwenda kuwapa hizi *project* za kuwaongezea ujuzi vijana, kama miundombinu haijakaa vizuri kwenye majimbo yetu, basi moja kwa moja hatutafikia malengo. Tunawapeleka watoto kwenye vyuo vya ufundi, wakija mitaani wanakutana na miundombinu hafifu ambapo wanashindwa kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiongelea vijana wa Jimbo la Kondoa Mjini mathalani, kuna mitaa zaidi ya 10 hata nguzo ya umeme hakuna. Sasa utawapelekaje vijana hawa kwenda kujifunza kuchomelea au kujifunza saluni na vitu vingine kama hivyo? Watawezaje kutumia ujuzi wao hali ya kuwa miundombinu hiyo haitoshelezi? Kwa maana hiyo, naomba, kwa kuwa hii ni Ofisi ya Waziri Mkuu, ndiyo ina Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu na Naibu Waziri

Mkuu yupo dada yetu Mheshimiwa Judith Kapinga ambaye nilimweleza masuala haya ya umeme, naye ameyachukulia *serious,* na ninadhani kupitia Bunge lako, Mheshimiwa Kapinga aliniahidi kwamba *weekend* hii atakwenda kutembelea jimboni kuona hali halisi ya miundombinu ya umeme ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaa haina nguzo ya umeme na haina umeme. Kwa maana hiyo, hata ukipeleka ujuzi kwa vijana kule, hawawezi kutekeleza majukumu yao kwa sababu hawana miundombinu ya kusaidia kuwafikisha pale wanapotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kupitia Bunge lako, nakuomba mambo mawili. Kwanza, naomba Naibu Waziri atekeleze ahadi yake ile ya *weekend* kwenda kutembelea Jimbo la Kondoa Mjini tukaone hali ya mitaa ambayo haina umeme, lakini cha ajabu unakuta kuna Jimbo lina vijiji 84 na vijiji vyote vina umeme, ila mitaa 36 haina umeme.

Mheshimwa Naibu Spika, vijana wa mjini hawana mashamba, wanatarajia wachomelee, wafungue saluni, wauze maduka ya vinywaji, lakini hakuna umeme, watafanyaje? Kwa maana hiyo, hilo nilikuwa naomba lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili katika kuwajengea uwezo vijana ili kuwasaidia kupata miundombinu, tujikita hapo hapo kwenye umeme, iko mitaa yangu ambayo ilipata bahati ya *project* za umeme wa *REA,* ni muda umeenda sana, karibu mwaka wa pili huu, ila kwenye hiyo Kata ya Suruke miundombinu imekamilika, lakini mkandarasi hajawasha umeme. Kwa maana hiyo, ujio wa Naibu Waziri unaweza ukamsukuma mkandarasi kwenda kuwasha umeme ili wale vijana waweze kupata miundombinu ya kujipatia kipato kwa kufungua biashara ambazo zinaendana na masuala ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili kuna mtaa ambao umerukwa na nguzo za umeme zipo, zimekaa pale, hazina kazi.

Nimeulizia, nikaambiwa kwamba zitaondolewa pale na kupelekwa jimbo lingine la vijijini. Sasa kama mji unakosa umeme halafu nguzo zimepelekwa mtaani, kesho zinanyanyuliwa zinahamishwa kupelekwa sehemu nyingine za vijiji, tunaona hapa kuna haja ya kuliangalia hili vizuri. Ukienda kukuza vijiji ukaacha miji ikabaki haina umeme, bado itakuwa hatujaitendea haki hii miji, na tutakuwa hatujafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako pia liweke msisitizo juu ya jambo hili kwamba nguzo zile zilizopo pale zibaki zihudumie mitaa. Hata kama ni za mkandarasi, lakini kwa sababu najua Naibu Waziri Mkuu yuko hapa, anaweza akaelekeza nguzo zile zikabaki zifanye kazi kwenye Mitaa ya Guruma na Chemchem. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka tu nikutajie. Mpaka leo kwenye mitaa 36 hakuna hata nguzo na ni Halmashauri ya Mji. Kuna Mtaa wa Chemchem, Mtaa wa Kwa Mtwara, Tampori, Hachwi, Kutumo, Chora, Mongoroma, Chandimo, Guruma, Chavai, Choi, Gongo na Kereri. Maeneo haya yana wakazi wengi na makazi mengi lakini hakuna umeme. Kwa hiyo, ili kuwasaidia watu wale na jamii zile za mjini, na kwa sababu hatuna mashamba mijini, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu iweze kusaidia mitaa hii kupata umeme ili ile sera na *project* ya Serikali ya kuweza kuwasaidia vijana kujiajiri iweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Paulina, atafuatiwa na Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami pia nichangie siku ya leo. Awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kunipatia nafasi nami kuweza kuchangia. Namshukuru sana Waziri Mkuu kwa hotuba

yake ya jana ambayo ni nzuri sana na iliyosheheni mambo mengi sana ambayo kwa kweli yanaonesha kwamba nchi yetu tunakwenda mbele sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika suala la sekta ya afya. Nitajikita katika sekta ya afya kwa sababu taarifa nyingi sana za masuala ya afya haziwafikii wananchi, na zinapowafikia pia, zinafika kwa malalamiko. Nakupongeza sana dada yangu na Naibu Waziri, mnafanya kazi kubwa sana katika masuala ya afya, na kwa kweli tumesogea mbele sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nijikite leo kuelezea mambo ambayo Serikali inayafanya ambayo wananchi wengi hawayajui au wanapata taarifa ambazo siyo sahihi. Nianze kwa kusema tu kwamba, Tanzania katika miaka hii mitatu ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya kazi kubwa sana katika kuongeza wigo wa masuala ya afya. Watu wengi walikuwa wanakwenda nje kwa ajili ya afya, lakini sasa hivi tumepunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze tu kwa haraka haraka kusema kwamba, huduma za ubobezi zimeongezeka sana katika nchi ya Tanzania. Kwa mfano, suala la ugonjwa wa figo lilikuwa ni gonjwa ambalo likipatikana, watu walikuwa wanaona labda ni suala gumu, lakini sasa hivi katika nchi yetu katika mwaka 2020 mpaka 2023, teknolojia imeongezeka sana kiasi cha kuweza kutengeneza figo kwa kutumia matundu madogo na kuweza kuweka figo kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, hayo ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jambo la pili ni katika upandikizaji wa uroto. Uroto ilikuwa ni changamoto kubwa sana na ndiyo unaotengeneza *white blood cells* katika mwili. Uroto ukikosekana, basi mtu hawezi kuishi, lakini Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu amefanya kila njia, na kuanzia mwaka 2021 tumekuwa na

wagonjwa 11 wameanza kupandikizwa uroto na wanaishi kwa matumaini. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana pamoja na Naibu Mawaziri, tunawapongeza sana kwa kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe katika sehemu hii ya afya kulikuwa na tatizo kubwa la kuondoa uvimbe kwenye ubongo. Ilikuwa mtu akipata *trauma* au tatizo la ubongo, ilikuwa ni shida. Ilikuwa mara nyingi huyu mtu kuishi siyo rahisi, lakini kwa muda mfupi sana Rais ameweza kufanya hili jambo na tunaweza sasa kupitia matundu ya kwenye pua, wagonjwa sita wamefanyiwa *operation* ya ubongo. Kwa kweli ni mafanikio makubwa kwa muda wa miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Rais pamoja na Mawaziri na wafanyakazi wote wa Wizara wameweza kuvunja mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa kutumia mionzi bila upasuaji. Hili jambo lilikuwa siyo la kawaida. Tuna wagonjwa 510 ambao ni wengi, lakini kwa muda wa miaka mitatu wameweza kupatiwa matibabu hayo. Sasa hivi hata likitokea tatizo lolote la mawe katika mfumo wa mkojo mtu anaweza akaenda kupata matibabu katika hospitali zetu. Kwa hiyo, ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni upasuaji wa saratani ya utumbo mpana kwa njia ya haja kubwa. Kwa kweli pia lilikuwa ni changamoto. Ilikuwa mtu akipata saratani, inaonekana ni ugonjwa mkubwa sana na wengi walikuwa wanakufa. Miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu, na miaka mitatu ya Waziri Ummy Mwalimu pamoja na Naibu wake na Mawaziri wengine, wagonjwa 410 wameweza kufanyiwa hii huduma na kwa kweli ni mafanikio makubwa sana. Sasa hivi hata mtu akiwa na tatizo hilo la saratani ya utumbo siyo *issue* tena ya kufikiria kufa. Kwa hiyo, ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niendelee kusema tu kwamba, kumekuwa na ubobezi katika masuala ya uzazi. Saratani ya uzazi

ilikuwa ni changamoto sana. Mwanamke alikuwa akipata matatizo ya saratani alikuwa anajiona labda huenda ni mtu wa kufa, lakini kuanzia Julai, 2020 muda mfupi sana watu 92 wamepata hii huduma. Hivi tusema nini? Kwa kweli afya imeboreshwa sana katika hii miaka mitatu. Tunampongeza sana Rais wetu, tunaipongeza sana Serikali pamoja na Mawaziri wote ambao mmefanya hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna upasuaji wa ubobezi wa kupandikiza nyonga na magoti kuanzia mwaka 2022. Februari tu mpaka leo watu 135 tumeokoa shilingi ngapi za Watanzania? Kwa kweli, tuwe wakweli, tuseme Rais amefanya kazi kubwa sana. Nimeenda leo kwa *data* ili kuonesha kwamba sekta ya afya imefanikiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna upasuaji wa matundu madogo ambayo yanaitwa *endoscopy procedures,* watu 24 wamefanyiwa upasuaji na umefanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hivi, afya ndiyo kila kitu. Mtaji wa binadamu ni afya. Tunakwenda sasa kuboresha bima kwa wote, tutafanikiwa. Kwa namna tulivyokwenda, hakuna jinsi, tutafanikiwa. Hakuna mahali ambapo, hata mkuyu ulianza tu kama mchicha, tutafanikiwa. Kwa hali ilivyo sasa hivi, wagonjwa wana matumaini. Tumetoka huko kwenye ma-*paracetamol* tumekwenda huku kwenye upasuaji mkubwa, wala watu hawafikirii kwenda nje. Nampongeza sana Rais kwa kazi anayofanya na vilevile nawapongeza sana madaktari ambao wamejitolea. Hii sasa inawajengea vijana wetu ari ya kuona kwamba, kumbe haya yanawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi sana waliokuwa wanafikiria wakimaliza tu mtihani, japo walikuwa wanapenda sana kupata *Division One,* walijua hawawezi kuajirika Tanzania, lakini hawa wanaofanya hizi kazi ni Watanzania na ukienda hata Mloganzila ni Watanzania. Mheshimiwa Dkt. Ummy Mwalimu, Waziri

wa Afya, mimi nakuita *Doctor*, hongera sana pamoja na Naibu wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile salamu nyingi ziende kwa Rais wetu, amefanya kazi kubwa. Afya ya wananchi inapoimarika, basi kazi zitafanyika. Najua mengi ni muhimu, barabara ni muhimu, na kila kitu ni muhimu, lakini ndugu zangu mtu kama huna afya, utatumia hivyo vitu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa haya matibabu sasa hivi yanapatikana nchini, naomba nitumie fursa hii kuwaambia, tusinung'unike, jambo likitokea kama uvimbe na kadhalika, tujitokeze, huduma zipo, na zinapatikana. Kwa kweli Rais anafanya kazi kubwa, naomba salamu hizi zimfikie na kwa kweli, Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye Wizara hii muhimu na Kaimu Waziri Mkuu anisikilize vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua adha ambayo wanapata wastaafu wetu, sote tunajua kikokotoo bado ni janga na hii haijaisha, mpaka iishe. Ilianza kulalamikiwa tangu sheria inatungwa. Hitaji lao ilikuwa wachukue mafao kwa mkupuo asilimia 50, mkaleta asilimia 33. Bado kuna manung'uniko kwa watumishi. Nikiwaonesha meseji zangu za askari, walimu, manesi na madaktari, ni shida. Mtu anastaafu anapewa shilingi milioni 17, na hajajenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua mtumishi wa umma anafanya kazi kwenye mazingira gani? Kuteleza si kuanguka, turudi tukae tuwasikilize. Hizi ni fedha zao Serikali inaweka, wapeni mafao kwa mkupuo kwa 50% na hiyo nyingine mwape kidogo kidogo. Yale mafao ya mkupuo ndiyo yanayowasaidia, siyo hiki ambacho mnawapa kila mwezi. Wakiweka misingi, hayo maisha mengine yatakuwa ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisema hapa tangu mnabadilisha sheria, mnasema mnabadilisha sheria ili kuwe na manufaa, lakini tulikuwa tunajua mlikuwa mnajua mifuko inakufa na hamkufanya tathmini, mkaenda mkaunga tu huko huko. Madhara yake ndiyo haya. Sasa leo mifuko yetu ina shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia mfuko mmoja tu hapa unaohusu watumishi wa Serikali wa *PSSSF*. Kwa mujibu wa Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ukwasi unatakiwa uwe 40%, lakini ripoti ya *CAG* ya kila mwaka inaonesha ukwasi ni 20%. Kwa sababu gani? Serikali mnachukua fedha kwenye mifuko, mnaenda kuwekeza lakini hamlipi. Wakati tunapitisha bajeti hapa mwaka 2020/2021mlilipa kwa *non cash bond* shilingi trilioni 2.1, mkasema mwaka ujao wa fedha mnalipa shilingi trilioni 2.4, mpaka leo hamjalipa. Sasa hii mifuko itawezaje kuwa *stable*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupa tu mfano, nianze na takwimu za mwezi Juni, 2020 ambapo michango ya wanachama kwenye mfuko ilikuwa shilingi 1,364,000,000/= huku mahitaji ya mafao ilikuwa shilingi 1,554,000,000/=. Nyongeza waliyokwenda kuchukua kwenye vyanzo vingine ni shilingi 190,000,000/=. Sasa kwenye hiyo nyongeza umeenda kuchukua kwenye *investment income* yao ambayo kwa mwaka huo ilikuwa shilingi 400,000,000/=, *can you imagine!* Wakipunguza hapo wanabaki na nini? Yaani hapo wamejikusanya kwenye *investment* zao kwa mwaka, *PSSSF* shilingi milioni 400. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya, nakuja mwaka ulioishia Juni, 2022 ambapo michango ya wanachama ni shilingi bilioni 1,526 huku mahitaji ya mafao ni shilingi bilioni 1,697. Pungufu waliyokwenda kuongeza ni shilingi milioni 171. Ukiangalia *investment return* yao kwa mwaka huo ni shilingi milioni 587. Sasa wakitoa hapo, wanabaki na nini? Yaani kwa mwaka wameangalia waliko-*invest* kule ni shilingi milioni 500, halafu sasa wapunguze shilingi milioni 177, mfuko ambao Serikali inaenda kukopa haiwalipi, inaenda ku-*invest* maeneo mbalimbali hairudishi fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia ukurasa wa 28 wa Hotuba ya Waziri Mkuu, ameongelea vizuri tu, ndiyo hatukatai ku-*invest PSSSF* huko Mkulazi ambako anasema mmezalisha sijui tani 50 za sukari, wamewekeza asilimia 96, lakini kwa miaka minne wamepata hasara ya shilingi bilioni 11. Hawa watu ambao *investment income* yao kwa mwaka ni shilingi milioni 500, ukienda Kiwanda cha Mbozi wame-*invest* mtaji wa 86%, wamepata hasara kwa miaka minne mfululizo shilingi bilioni 4.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wanachukuaje fedha za wanachama waende kupeleka sehemu ambayo inapata hasara? Inaonekana walikuwa hawajafanya tathmini ya kina kuhusiana na *investment* kwenye eneo hilo. Hizi fedha ni za wastaafu. Hatukatai kuchukua fedha hizi ili kuwekeza, lipeni madeni basi, tuone hata huko kwenye mshiko wao kwa mwaka unaeleweka. Sasa mnakomba mabilioni halafu wenyewe wanabaki na shilingi milioni 500! Jamani, kweli! Hata wakitaka kulipa wastaafu ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la dawa za kulevya. Nasema kila siku, nina mdogo wangu ameathirika na yuko *sober house* ya Bagamoyo. Lazima Serikali mwekeze kwenye kutibu. Lengo la kuanzisha Tume lilikuwa ni kuzuia, kukamata na kutibu waraibu wa dawa za kulevya. Mmejikita kwenye kukamata, na sasa hivi mnakamata sana. Mnajua ni kwa sababu gani? Kwa taarifa ya Umoja wa Mataifa huko duniani, wazalishaji wa dawa za kulevya wameongezeka kwa 25%. Hizo mnazozikamata ni ndogo, bado

watu wanaingiza kimya kimya huku vijana wetu wanaathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati mnaendelea kupambana, hakikisheni wale walioathirika mnawatibu, na mkishawatibu mtapunguza magonjwa ambayo yanatokana na kutumia dawa za kulevya. Watu wanaharibika ini, figo, mwisho wa siku mnakuwa na mzigo mzito wa kuhudumia magonjwa ambayo yanatokana na dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwa sasa hivi *multiclinics* ziko 11 tu. Tathmini ambayo mnaitumia sasa hivi ya wagonjwa mlionao 530,000 ni ya tangu mwaka 2014. Kweli! Hamjafanya tathmini, mnawezaje kuhakikisha mnapambana na hili janga? *Multiclinics* 11! Haya, ukienda tu pale kwa mfano *multiclinic* ya Mwananyamala, watu wanaokunywa dawa pale ni msongamano, watu 1,500; nenda Muhimbili, watu 1,200; nenda *multiclinic* ya Tanga, ni zaidi ya watu 1,000, lakini walioathirika kwa takwimu zilizopitwa na wakati ni 530,000. Idadi ya watu 30,000 ni ambao wanajidunga, 500,000 ni wale ambao wanavuta na/au wanalamba. Sasa, mnawezaje kupambana bila takwimu ambazo ni *latest*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yenyewe mna *rehab* moja na haijaisha. *Seriously,* kwa tatizo kubwa namna hii, kweli! Halafu huku mnatupatia taarifa sijui mmekamata bangi mmechoma, sijui nini. Bado kuna tatizo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa na mtu ambaye unamhudumia, mosi, *future* yake imeharibika; lingine amekuwa ni mzigo wako wa milele. Leo kuna *Sober Houses* 40, lakini mnazisaidiaje? Hizo ni za watu binafsi, ninyi Serikali hamna, ilhali tatizo ni kubwa sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa mujibu wa mikataba ambayo nchi yetu imeridhia na kukubaliana Kimataifa katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya, ni pamoja na kushirikisha wadau mbalimbali na siyo kazi inayoweza kufanywa na Serikali tu. Kwa hiyo, tunachokifanya, *Sober Houses* zinazoanzishwa na wadau, kila mwaka Serikali ndani ya Bunge lako Tukufu imekuwa ikitenga bajeti ya kuzisaidia hizo *Sober Houses* ili ziweze kufanya kazi nzuri ya kuendelea kuwahudumia warahibu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima Waheshimiwa Wabunge tujue kwamba kazi inayofanywa na Serikali ni nzuri sana kwa kushirikiana na wadau hao ambao wamekuwa wakianzisha hizo *Sober Houses,* ikiwa ni pamoja na kuyafanyia kazi maeneo hayo yote matatu. Kwa hiyo, Serikali inawajibika ipasavyo na ndiyo maana mmeona mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanafanikiwa na Mheshimiwa Ester utakubaliana na sisi kwamba kazi nzuri inafanyika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya, taarifa hiyo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu kutenga ni jambo moja, na kupeleka ni jambo lingine. Sisimami hapa kuongea bila kufanya utafiti. Ungezitaja hapo *data*, mimi ndiyo maana nimekutajia hapa. Zamani Tume ilikuwa inaweza kuwasaidia hata kuwalipia kodi miezi sita, sasa hivi hakuna na wana-*suffer*. Ni jambo la kupokea tu dada yangu, kwa sababu hili ni janga letu sote. Kizazi kinaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wastaafu wanung'unike, vijana tusiwawekee misingi bora. Tutafika wapi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo. Ahsante.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Eng*. Ezra, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kipekee nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Tukiangalia Hotuba hii ya Waziri Mkuu, imeelezea maendeleo ya miradi yote mikubwa ya kitaifa na yote iko katika hali nzuri. Sasa, tunapoona Taifa linawekeza fedha nyingi katika miradi hii ya maendeleo *especially* miundombinu, maana yake ni kwamba hili ni Taifa linalokua, ni Taifa lenye uchumi mzuri na ni Taifa ambalo lina malengo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Mataifa yote makubwa, mfano leo uende China au Dubai na kwingineko, zile nchi bado zinajenga kila siku. Wanajenga barabara kila siku, pamoja na kwamba wana barabara nzuri, wanaongeza reli wanafanya na vitu kama hivyo kwa sababu uwekezaji katika miundombinu ndiyo unaonyanyua Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, pia nampongeza sana sana Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya. Tumemwona amekuwa ni msaada mkubwa sana kwa Mheshimiwa Rais kwenye kuisimamia Serikali, na kila anapofanya ziara, anapokanyaga sehemu, Wabunge wote na wananchi wote wa Tanzania ni mashahidi, amekuwa akiacha alama hasa akikemea ubadhirifu na vitu vingine kama hivyo. Kwa hiyo, tumpongeze. Halikadhalika tunampongeza Naibu Waziri Mkuu, na wasaidizi wake wote kwenye

ofisi yake wakiongozwa na Mheshimiwa Jenista ambaye yuko hapa. Kwa kweli kazi mnayoifanya ni kubwa na hivyo ni lazima tuwapongeze kwa haya mazuri ambayo mnayafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, ninayo mambo kama mawili ya kuongelea kuhusu jimbo langu, na pia nitaongea na mambo mengine ya Kitaifa. Kwenye masuala ya jimbo langu, kwanza nashukuru kwa miradi mingi sana ya maendeleo. Tumepata fedha nyingi kwenye miradi ya maendeleo kama vile maji, barabara, afya, elimu, umeme na mambo mengine ambayo yanafaa kwa ajili ya wananchi. Wananchi wamefarijika na mambo ambayo yanaendelea kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maombi ambayo niliyawasilisha hapa, ni mwaka wa pili sasa. Kwenye maombi ya kimkakati ya Mkoa wa Kagera tuliomba ujenzi wa Stendi ya Biharamulo, tukaambiwa tulete andiko. Tulishaleta andiko la shilingi bilioni 2.7, liko kwenye maombi ya Kimkakati ya Mkoa wa Kagera, sasa ni mwaka wa pili; tumeomba ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, sasa ni mwaka wa pili. Tumeleta maombi ya shilingi bilioni 3.4 na tukajibiwa kwamba wanaingiza kwenye bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu Wilaya kongwe kama ya Biharamulo unapokuja unapofika ofisi za halmashauri zimejaa magrili utafikiri maduka ya Mangi. Kwa kweli ni aibu. Hata sisi ifikie hatua tuonwe, na ionekane kwamba tunastahili kuboreshewa hii miradi. Zile *conditions* ambazo mmeziweka za kupeleka miradi ya maendeleo hasa majengo ya halmashauri kwenye wilaya mpya tu, sioni kama zinafaa kwa sababu zinawaonea hawa wa zamani. Hawa ni wakongwe, na hawakutaka wawe vile. Lazima Serikali iwekeze kote, iangalie hata wa zamani iweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kwenye bajeti hii, hasa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, mambo haya mawili ni muhimu kwa ajili ya watu wa Biharamulo. Nimeshaomba mara nyingi hata mbele ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, naomba tupate majibu watu

wa Biharamulo kwamba ujenzi wa Stendi ya Biharamuro na jengo la halmashauri unaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuliomba habari ya kuongezewa maeneo. Biharamulo ni wilaya iliyokua na ninavyoongea leo ndilo jimbo lenye watu wengi kwa Mkoa wa Kagera, likiongoza kwa Mkoa wa Kagera, na ni jimbo namba 20 kwa wingi wa watu Tanzania hii, lakini hatuongezewi maeneo kwa sababu tumezungukwa na hifadhi kila upande. Kwa hiyo, nimeomba haya maeneo mara nyingi, na ninadhani nitaweka vizuri kwenye hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini ombi lichukuliwe, tuongezewe maeneo, kwani watu wanaongezeka lakini maeneo ya kufanyia shughuli za uchumi ni machache kwa sababu tumezungukwa na Hifadhi ya Buligi, tumezungukwa na maeneo yote ya *TFS,* sasa wananchi hawana pa kwenda. Wakichunga ng'ombe wanakamatwa, wakienda kulima wanakamatwa. Kwa hiyo, Serikali ilione hilo na itoe maelekezo maalumu ili watu waweze kuongezewa maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme kwa niaba ya wenzangu wote wanaotoka maeneo ya mipakani. Tumelia sana na habari ya *NIDA*. Wewe najua unatokea Ilala pale, unaweza usiulizwe kuhusu *NIDA,* lakini sisi tunaotoka mikoa ya pembezoni, *NIDA* imekuwa kilio kikubwa. Sisi ni Watanzania kama Watanzania wengine, lakini inapokuja kwenye suala la kupewa vitambulisho vya Taifa, imekuwa kama tunaonekana tunatokea sehemu nyingine tumekuja kuvitafuta hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba Serikali itoe majibu hapa, maana hili jambo niliuliza humu zaidi ya mara mbili tunaambiwa wanashughulikia, lakini imefikia hatua mbaya. Pale kwangu Biharamulo yuko mtumishi mmoja wa Ofisi ya Uhamiaji, watu wanaenda pale kuomba kujaza hata fomu tu, akishamwona tu, anamwambia wewe sio Mtanzania, anamfukuza. Hata kumpa fomu ajaze hampi. Ukitaja jina, anakwambia siwezi kukupa fomu wewe siyo Mtanzania. Sasa Utanzania wa mtu unapimwa kwa majina au

kwa kumwangalia sura, au umpe fomu ajaze, baada ya hapo ndipo muanze kufanya *vetting,* umjue ni Mtanzania au sio Mtanzania!

Mheshimiwa Naibu Spika, huyo mtu anaenda mbali, alienda Mheshimiwa Diwani mmoja akapeleka watu pale, inafikia *stage* anamwambia mimi si-*deal* na wanasiasa. Hivi kweli hu-*deal* na wanasiasa, Waziri wako Mheshimiwa Masauni ni nani? Siyo mwanasiasa? Kwa hiyo, tunaomba kwanza hizi dharau za watumishi ziishe. Wanapohudumia Watanzania kule wanatengeneza chuki ya watu dhidi ya Serikali yao kwa majibu ya ovyo kama hayo ambayo hata walioko juu hawayajui. Wananchi wanaenda kule wanarudi wakilalamika tumenyimwa vitambulisho, tumenyimwa hiki. Ukiwaambia mjiandikishe kwenda kupiga kura, wanakwambia kwenye kupiga kura mnatukumbuka, lakini kwenye vitambulisho sisi sio Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunawaomba watumishi wa Serikali kupitia Bunge hili wasikie na wajue wapo kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania. Wasiichonganishe Serikali na Watanzania na wasimchonganishe Mheshimiwa Rais na Watanzania. Wafanye kazi yao, wawe na wasemaji. Kama wewe siyo Mtanzania, ujibiwe kwa *documents* na sio mtu unaenda, anakunyima hata fomu. Umesafiri, umetoa nauli, unafika pale hata fomu tu ya kujaza unanyimwa. *That is not fair*. Kwa hiyo, tunaomba hilo liangaliwe, lichukuliwe na Wizara ya Mambo ya Ndani, mtumishi huyo afuatiliwe Biharamulo. Hamkutuletea mtu wa kuwa kero, anatakiwa aondoe kero za wananchi kukosa vitambulisho, asiwe kero hata ya kuwanyima fomu ya kujaza. *That is not fair*. Naomba niliweke wazi hapa ili lichukuliwe na Serikali ilifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimaliza hayo, wewe ni shahidi na unakumbuka kwenye Bunge la mwezi wa Pili Wabunge tulisimama tukaongea kwa habari ya uharibifu wa barabara na tukajibiwa na Serikali, kweli 20% iliyokuwa imebaki ilitangazwa, baadhi ya barabara zinaendelea. *I was very specific*, nilisema, kuna barabara ziliongezwa za shilingi bilioni 350 kwa kutumia *system* ya *EP4R*,

tukaambiwa zitakuja shilingi milioni 500 kila jimbo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha akaliambia Bunge hapa kwamba zile fedha ameelekeza ziende na zile barabara zitatangazwa, lakini ninavyoongea hapa, nawe ni Mbunge wa jimbo, nina uhakika jimbo lako nalo limo, kama zimeletwa Dar es Salaam kwa watu wa mjini, sawa. Kwetu Biharamulo hizo barabara hazijaletwa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ezra jitolee mfano mwenyewe, usiguse kabisa mambo ya Ilala. *(Kicheko)*

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea, hayo ni maelekezo. Najua sigusi Ilala, lakini ni sehemu ya majimbo. Kwa hiyo, ninachoomba, tunataka tupate majibu. Ahadi aliyoitoa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ndani ya Bunge hapa ilikuwa ni kututuliza Wabunge tuondoke kuelekea majimboni ili ile ajenda tuiache au nini? Kwa sababu tumeondoka hapa tukijua barabara zinatangazwa. Tumefika kule, na tulishawaambia wananchi juu ya ujenzi wa zile Barabara, lakini mpaka leo imebaki miezi mitatu tumalize Bunge hili la Bajeti ilhali hatujui *direction* ya ile barabara, hatujui nini kinaendelea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunataka tupate majibu ya Serikali kwamba shilingi milioni 500 ya ile nyongeza ya shilingi bilioni 360 ambayo iliahidiwa humu ndani ya Bunge wakati tunapitisha bajeti hii tunayoendelea nayo, zile barabara zinatangazwa lini? Kwa sababu kama maelekezo yalikuwepo ni lazima tuzione. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, tumesema nchi hii tunafanya miradi mikubwa sana ya maendeleo lakini iko habari ambayo tumekuwa tunaiona, kwamba ushirikishwaji wa Watanzania kwenye miradi hii mikubwa tunayoisema ni mdogo sana. Ni lazima tuseme, miradi hii yote mikubwa; miradi ya reli, miradi ya ujenzi wa barabara tunayoisikia hapa, ujenzi wa meli na vitu vingine vyote

vikubwa haifanywi na wazawa. Miradi hii inafanywa na wageni. Inafanywa na kampuni kubwa sana za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba, tumeona Serikali imefanya bidii kubwa sana kwenye habari ya Wizara ya Kilimo. Katika miradi ya kilimo riba imeshushwa mpaka *single digit,* lakini unavyokuja kuangalia, mwajiri mkubwa katika miradi hii mikubwa ya maendeleo ni Serikali. Kwa hiyo, kama ni Serikali na miradi hii inakatiwa bima, ni miradi ambayo hata *cash flow* yake na *sustainability* yake ni kubwa, hata benki zinapokopesha zina uhakika wa kulipwa kwa sababu ni miradi inayoonekana, ni miradi ya Serikali. Tunaomba kupitia Bunge hili, Serikali irudi mezani ikaongee na benki, kwani wakandarasi wengi wa Kitanzania wanashindwa kuwa *competitive* kwenye miradi hii mikubwa, wanaishia kuwa *sub-contractors*, kwa sababu hawana uwezo wa kukopesheka katika riba nzuri, halikadharika hawezi kushindana kwenye bei wakati wanafanya *tender*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunaomba hata wakandarasi wa nchi hii kupitia Serikali, kupitia *CRB* kaeni chini muongee na benki, wakandarasi wakopesheke kwa *single digit.* Haiwezekani leo mtu anatoka China anakopeshwa kwa asilimia saba kwenye nchi yake, lakini hapa ukakope kwa asilimia 22 na uweze kuwa *competitive*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya Bwana China, muda wako umekwisha.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nami kupata nafasi ya kuchangia katika wizara hii. Nitajikita zaidi katika eneo la kilimo. Tunafahamu kabisa nyanda za

juu kusini, mikoa mitano inalisha takribani Taifa zima. Kinachoshangaza, Benki ya Kilimo ambayo kimsingi tunafahamu kwamba yenyewe ndiyo inatakiwa kusaidia wakulima wadogo wadogo, bado wakulima hao wapo kwenye matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Kilimo kwenye bajeti hii inasema imetoa takribani shilingi bilioni 160 kwa wakulima, lakini ukipiga hesabu ya wakulima hawa, hawazidi asilimia 10 ya wakulima ambao ndio wengi katika Taifa hili. Tunaomba Benki ya Kilimo ijikite kusaidia wakulima wadogo wadogo wapunguze masharti ili wakulima hawa waweze kupewa mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kilimo, kuna mazao ya kimkakati. Tunafahamu zao la chai ni zao muhimu sana, na zao la chai katika soko la dunia bado linahitajika. Hata kama wataalamu na wadau wanadai vita ya Ukrain imesababisha bei hii kushuka, lakini bado chai katika biashara ya ndani inanyweka, hata katika *East Africa* pia chai inanyweka. Chai hii inapatikana sana Wilaya ya Rungwe na kwa inapatikana kwa ndugu zetu wa Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa chai ni watumwa katika Taifa lao. Leo hii tuna wawekezaji, kwa mfano nikichukulia kwa Mkoa wa Mbeya, tuna viwanda viwili; Kiwanda cha Katumba na Kiwanda cha Busokelo. Mwekezaji ameamua kuuza kiwanda kile bila kuwashirikisha wakulima wadogo wadogo. Baada ya kuleta malalamiko, anasema kwamba, anawapa *AMCOS* ndiyo wawe wananunua. Naomba katika wizara hii, msimamie mwekezaji huyu kama kweli hiyo chai anawapa *AMCOS,* tunaomba mfuatilie lakini wakulima walinunua *shares,* leo ni zaidi ya miaka 15 katika zile *share* walizonunua hawajawahi kupata faida na wala kile walichokipanda hawajakivuna bado. Naomba Serikali msimamie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la bei, tumelia sana na bei. Wakati tunaanza kulalamika hapa, bei ilikuwa ni shilingi 132 kwa kilo, angalau mmepandisha mpaka shilingi 366. Kwa hilo

nawapongeza, lakini bado chai inahitajika kuwa na bei kubwa kwa sababu wanunuzi wake wanauza nje kwa bei kubwa zaidi. Kwa nini mkulima anyonywe wakati pembejeo ni za kwake, anaishughulikia yeye, anakuja kupata shilingi 360? Tunaomba chai iongezeke bei ifike shilingi 700 angalau ili mkulima aweze kujikwamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia habari ya parachichi, kule nyanda za juu kusini. Parachichi tunaita ni zao au dhahabu ya kijani, kwa maana leo hii parachichi inalika kama dawa, ni chakula, na ina soko dunia nzima, lakini mzalishaji wa zao hili pesa anayopata ni ndogo. Leo kilo ni shilingi 1,600 au 1,500, lakini ukienda Uingereza kwa soko la leo, parachichi moja ni *pound* saba. Tunamsaidiaje mkulima wa kawaida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi ndugu zetu majirani, *East Africa* wanakuja wananunua parachichi hizi wanapeleka nchini kwao, wanazi-*brand* kwa majina yao wakati sisi tupo. Naomba Serikali msimamie hilo. Wizara ya Viwanda na Biashara hakikisheni mnatoa mafunzo kwa wakulima tuweze na sisi ku-*export* na tupate faida kama Wanarungwe kama Wanambeya, na kama Watanzania na Wananjombe pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, ninazungumzia suala la *TAZARA*, Reli ya *TAZARA* miaka ya 1974 na kuendelea. Rais wa Kwanza alifanya vizuri sana na reli hii ilikuwa inasaidia sana kutoka Dar es Salaam mpaka Zambia, Kapiri Mposhi. Leo hii mzigo mkubwa upo kwa Tanzania. Wenzetu wa Zambia wamekuwa wakisuasua, hawachangii mchango wanaotakiwa kuchanga, deni kubwa limebaki kwa Tanzania. Watanzania kwenye *TAZARA* wanadai madeni mengi sana hasa ya wafanyakazi. Tunaomba msimamie hilo, wafanyakazi wapate haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie madeni. Wakandarasi wengi sana wanadai, lakini kibaya zaidi, mikataba ya ukandarasi tunayoingia inaongeza riba kwa sababu hawalipi kwa wakati. Leo

hii Serikali inadaiwa takribani shilingi trilioni moja, tunawezaje kuweka madeni haya? Mzigo huu ni mzigo kwa Mtanzania anayelipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wamepisha ujenzi wa barabara au miradi yoyote katika nchi nzima, na wanadai shilingi trilioni saba. Serikali hamwatendei haki Watanzania. Tunaomba fedha hizi zilipwe. Watu hawaendelezi majengo, hawafanyi maendeleo, wanadai fedha. Tunaomba mwalipe. Tunaomba sana sana, tusimamie haki ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kujua, kuna suala ambalo sasa linaendelea, Serikali ikisimama hapa itueleze kuhusu mitandao ya kijamii. Tunaomba nchi yetu iende kidigitali. Tumeomba kwa muda mrefu na tumeingia huko. Nimepata taarifa, na ninaiomba Serikali itupe taarifa rasmi kuhusu ulipaji wa *WhatsApp,* kwamba makundi ya *whatsApp* yalipiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sijafahamu, naomba nielekezwe ndani ya Bunge lako Tukufu, makundi haya yapo ya kifamilia, ya kiukoo, ya kijiji na mikataba mbalimbali. Kama ni kweli yanayosemwa kwenye mitandao, tunaomba myaingilie tuweze kuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni unyanyasaji wa kijinsia kupitia hiyo mitandao. Wasichana wengi wamesemwa vibaya na kusingiziwa kwenye mitandao, hata wanasiasa pia. Tunaomba Serikali isimamie. Tunajua wanaoandika na kutuma kwenye mitandao hii ni rahisi kuwapata kwa kuwa *TCRA* ipo. Tunaomba msimamie haki ya watu wanaozushiwa uongo kwenye mitandao. Wanaozusha uongo wowote, wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliyoyasema yafanyiwe kazi. Mwisho wa siku nitaangalia kama naunga mkono au siungi mkono. Ahsante, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tabasam, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Kassinge na Mheshimiwa Yahya Mhata.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami naomba kuchangia katika bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, anazunguka nchi nyingi sana duniani kwa ajili ya kutafuta wawekezaji, na wawekezaji hawa wakija Tanzania wanapewa vibali na mikataba kwa mujibu wa sheria. Sasa hivi urahisi wa wawekezaji kuhudumiwa katika ofisi zetu za umma ni wa hali ya juu sana uko katika mitandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Sengerema sisi tuna mgodi mkubwa unaitwa Nyanzaga. Mgodi huu upo kilomita 43 kutoka Sengerema. Mgodi huu mkataba wake ulisainiwa mwaka 2023, nafikiri kama mwezi wa Nane hivi na mkataba ule kwa mujibu wa sheria za Tume ya Madini ya Taifa ni kwamba ulikuwa unatakiwa ndani ya miezi 18 jiwe la kwanza liwe limeanza kudondoka pale Sengerema kwa ajili ya kusafishwa kwa ajili ya kutoa dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango yote ya ulipaji wa fidia ilishughulikiwa kwa mujibu wa sheria, lakini ulipaji wa fidia uliingia katika mgogoro baada ya wananchi wa Jimbo la Sengerema Kata ya Igalula kulalamikia malipo yale ya fidia kuwa madogo. Wenzetu wa Nyamongo ambayo ni Kanda ile ile ya Ziwa, katika mgodi wa Nyamongo katika Wilaya ya Tarime wanalipwa ekari moja shilingi milioni tano na sisi Wilaya ya Sengerema katika Jimbo la Sengerema ekari moja ilikuwa inalipwa kwa shilingi milioni mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikwenda kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, wakati huo alikuwa Mheshimiwa Lukuvi na Naibu Waziri alikuwa Dkt. Angeline Mabula kuwaomba walishughulikia lile jambo lakini bado pamoja na maelekezo ya Waziri, Mheshimiwa Lukuvi wakati ule, kwamba lazima waangalie uwiano kwa nchi nzima na waone malipo yanalipwa kwa uwiano upi, walisimamia malipo yale.

Sasa sisi juzi tumekwenda Nyamongo kama Kamati ya Madini, tumekuta kule wenzetu wanalipwa shilingi milioni tano. Ni jambo ambalo lilinihuzunisha sana mimi kama Mbunge wa Jimbo la Sengerema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgodi ule wa Nyanzaga umekuwa na matatizo makubwa ya kufanyiwa biashara, ni kama vile tunaowapata wawekezaji wote ni ma-*middleman*. Mgodi huu ulianza mwaka 2002. Kampuni ya *Tankan Mining* ilikuja kufanya pale kuja kupata leseni na kufanya usanifu wake. Wamefanya usanifu pale kwenye ule mgodi, mwaka 2006 wakawauzia watu wa *Barrick*, watu wa *Barrick* wakakaa na huo mgodi na baadaye nao wakauuza ule mgodi tena kwa *Sahara Mining*. *Sahara Mining* akauza tena kwa kampuni nyingine ambapo nayo ikawauzia *OreCorp*. Hawa *OreCorp* wakati wanakuja kupewa leseni, masharti yakaonekana kwamba, baada ya kurekebisha sheria zetu mwaka 2017 kwamba Serikali lazima ipate asilimia 16 katika mgodi, ikaundwa Kampuni ya *Sotta Mining.* Sasa mkataba umesainiwa, Serikali ina asilimia 16 kama *Sotta Mining*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wenzetu wa *OreCorp* ambao walikuwa wanatakiwa mwaka jana, 2023 mwezi wa Nne, mkataba wa miezi 18 ndiyo ulikuwa unakwisha. Kabla ya mkataba kwisha, mwezi wa Tatu wakauza hisa zao, tena kwa kampuni nyingine ya *Silvercorp*. Wale *Silvercorp* waliouziwa zile hisa nao tena wakauza kwa kampuni nyingine tena ya *Sypris* ya Australia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa imeonekana kama kuna mchezo sisi Sengerema tunaingia kwenye matatizo. Wananchi wanasubiri kupata *CSR* baada ya mkataba kusainiwa, kwa sababu ulisainiwa hadharani mbele ya Mheshimiwa Rais. Hili jambo linawaumiza sana wananchi wa Sengerema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunataka tupate majibu, je, haya mauziano yote yanafanywa Sengerema siyo *CSR* yetu sisi ambayo tulikuwa tunajua kwenye mkataba tunapata dola milioni

sita kwa mwaka? Je, hizi pesa zitalipwa na nani? Kwa sababu hawa tayari wanafanya mauzo, lakini hizi kampuni tangu zimeanza kuuza, kuanzia *Tankan Mining* mpaka leo tunakuja kumpata *Silvercorp* tena, na *Silvercorp* naye anakwenda kuuza, je, kodi ya Serikali imelipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tupate majibu. Kutokana na matatizo ya kuuzwa huu mgodi, unakuwa kama ng'ombe yupo zizini. Huu mgodi wa Sengerema, tunaonekana kama Sengerema tupo zizini tunakwenda kuuzwa kila siku, haiwezekani, wakati wenzetu tunaona wanavyowekeza kule katika suala la madini. Tunaiomba Serikali itusaidie, ije na majibu katika jambo hili. Kama haiwezekani, iundwe Tume ya Bunge kwenda kuchunguza mauziano haya tangu *Tankan Mining* mpaka leo kwenye *Sotta Mining,* kwa sababu kama mkataba huu umekwisha mwaka jana, 2023 mwezi wa Nne, tayari huu mgodi unatakiwa urudi kwa Serikali, Serikali ndiyo ifanye biashara. Hawatakiwi kufanya biashara watu ambao tayari muda wao wa leseni umekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba ulikuwa ni miezi 18 kujenga mgodi ule. Watu wamekwenda pale kujiandaa, lakini hawa watu tayari wameshapotea na aliyekuwa *CEO* pale anaitwa Mr. Damian, yule mzungu kapotea na kabadilisha na *line*. Kwa hiyo, inamaanisha mikataba yote iliyokuwa imeingiwa kwa ajili ya uwekezaji, makampuni ya kufanya biashara pale, yote imebakia kuwa hewani. Sasa tunaomba Serikali ije na majibu kuhusiana na suala la mgodi wa Nyanzaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine linaendelea katika nchi hii kuhusu suala la mizani. Hizi mizani zilizopo barabarani zinazuia kabisa uwekezaji katika Sekta ya Usafirishaji. Kwa mfano, gari la mafuta limebeba labda lita 42,000 kutoka labda *Depot* Kigamboni Dar es Salaam, linakwenda Kongo au Rwanda ama Burundi au Uganda. Hakuna chochote ambacho kimezidishwa pale, lakini unaambiwa gari imezidi kilo 50, au gari imezidi kilo 100. Hili ni jambo ambalo Wizara ya Ujenzi ije na majibu sahihi kwa sababu

wananchi hawa wawekezaji au hawa wenzetu ambao ni nchi jirani zinazotumia bandari ya Dar es Salaam, zinakutana na vikwazo kama hivyo vya kupigwa faini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, linguine ni suala la mizani kupima mabasi. Siku moja nimesafiri na basi la *SATCO* kutoka Mwanza kuja Dodoma, basi liko *level seat,* limebeba abiria 42. Basi lile limepimwa katika mizani ya Usagara, linakuja kupimwa katika mizani nyingine kule Tinde linaonekana linazidi kilo 60. Sasa abiria hawa unaowaona, abiria tunazidiana, kuna abiria ana kilo 150, kuna abiria ana kilo 120, hawa wenye mabasi watawezaje kuwapima abiria? Kila abiria akiwa anapanda kwenye basi apimwe, hii itakuwa ni nchi ya kwanza duniani katika jambo hili. Sasa mizani ni ngapi kutokea Mwanza mpaka kufika Dar es Salaam au kutokea Dar es Salaam kwenda Mbeya, Dar es Salaam kwenda Arusha? Haya mabasi kwa nini yaingie kupimwa kwa namna hiyo na yapo katika *level seat*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo ambalo tunaomba wenzetu wa Wizara ya Ujenzi waje na majibu sahihi kuhusiana na hili suala. Leo mabasi yanasafiri usiku, lakini yanavyokuwa yanaingia katika mizani, hata kama gari lipo *level seat,* je, abiria anatakiwa naye apimwe ili aingie kwenye basi? Waje na majibu, watueleze kwamba wenye mabasi sasa waweke mizani kwenye ofisi au stendi zilizopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Stendi ya Ndugai, Dodoma iwe na mizani, abiria akiingia akanyage pale kwenye mizani, aingie ndani ya basi ili haya mabasi sasa yatoke yaache kusumbuliwa. Pia waweke mizani kwenye stendi ya Magufuli pale Dar es Salaam, tujue, kwa sababu kama anaingia na *package* yake ya mzigo wa kilo mbili na wenyewe upimwe iwe kama viwanja vya ndege, kama tunataka kuipeleka nchi kuwa ya hali ya juu kiasi hiki. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo duniani mabasi yanapimwa? Ni Tanzania peke yake. Sisi tunasafiri nchi nyingi, tunashindwa kuelewa katika jambo hili. Tunaomba sana Wizara ya Ujenzi waje na majibu sahihi kuhusiana na suala la mizani la kunyanyasa wawekezaji na wasafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pole na swaumu. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Anayefuata ni Mheshimiwa Ally Kassinge, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Mhata, Mheshimiwa Vincent Mbogo na Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi ambazo anazifanya. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote na Manaibu katika ofisi yake kwa namna ambavyo wanachapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kwamba kutokana na mabadiliko ya tabianchi, maeneo yetu mengi nchini yameathirika na mvua za *El-Nino* ambazo bado zinaendelea. Kutokana mvua hizo, siyo tu miundombinu ya barabara na miundombinu mingine iliyoharibika, bali pia imeleta athari na madhara kwa makazi pamoja na maisha ya watu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kwa upekee wake kuwapa pole Watanzania kwa ujumla wao, pia kipekee wananchi wa Kilwa ambao wameathirika na mvua hizi katika maeneo yafuatayo kwa muhtasari; Somanga, Kinjumbi, Njinjo, Kipindindi, Miguruwe, Chumo, Nanjirinji, Kiranjeranje, Kikole, Mirumba, Makangaga, Mbwemkuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua ambazo Serikali imekuwa ikizichukua, ikiwa ni pamoja na kufika katika maeneo haya

na kwenda kushughulika na miundombinu ya barabara iliyoathirika, lakini kwa upekee wake naomba Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa, kitembelee maeneo haya ya Wilaya ya Kilwa ambayo nimeyataja kwa muhtasari wake ili wakafanye tathmini ya athari iliyopatikana na kwa kweli wananchi hawa wanahitaji msaada wa kibinadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, naipongeza Wizara ya Ujenzi, kwani baada ya madhara haya, walipata fursa ya kuja katika Mkoa wa Lindi na wametembelea katika maeneo machache ambayo yalikuwa yameathirika. Naomba kupitia Bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba, Kilwa nayo ni sehemu ambayo imepata madhara makubwa na imeharibu miundombinu mikubwa ya barabara. Barabara za kutoka Njia Nne mpaka Kipatimu, Nangurukuru mpaka Liwale, Nangurukuru mpaka Kiranjeranje na barabara kutoka Kiranjeranje mpaka Nanjilinji kupitia Makangaga hizi zimeathirika kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Ujenzi, *to see is to believe* (kuona ndiyo kuamini). Wafike katika maeneo haya wajionee ili hatua za haraka zichukuliwe kama ilivyokuwa katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika eneo la barabara ya Nangurukuru - Masoko. Barabara hii nimekuwa nikiizungumzia mara kadhaa katika Bunge lako Tukufu kwamba, ndiyo lango la kupitia kuelekea bandari ya uvuvi ambayo inaendelea kujengwa pale Kilwa Masoko. Vile vile uthamini na usanifu wa barabara hii ulikuwa ni wa muda mrefu, mpaka sasa Serikali bado haijatoa fedha kwa ajili ya kukarabati na kuboresha barabara hii ambayo kiukweli kutokana na shughuli za ujenzi wa bandari zinazoendelea, barabara hii sasa inapitisha mizigo mizito ya mchanga, mawe na *material* nyingine kwa ajili ya ujenzi wa bandari. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla bandari haijakamilika mwakani, kwa ahadi ya Serikali, barabara hii ndani ya bajeti hii

ifanyiwe utaratibu wa kutengewa fedha kwa ajili ya kuiboresha na kipande chake cha kutoka Nangurukuru mpaka Masaninga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika sekta ya miundombinu kwa upekee wake, viwanja vya ndege. Katika Bunge lako hili Tukufu tulipitisha Mpango wa Miaka Mitano wa Kuboresha Viwanja 12 vya Ndege kikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko. Kiwanja hiki hakipo katika kiwango kinachotakiwa, na tulipitisha katika Mpango, lakini mpaka ninapozungumza hapa, bado Serikali haijatoa fedha za kutosha kwa ajili ya kuboresha kiwanja hiki katika kiwango kinachohitajika. Ulifanyika uthamini mwaka 2013 ambapo wananchi 144 walioathirika, walikuwa bado hawajalipwa. Ukafanyika uthamini wa pili mwezi Juni, 2023, wananchi wameongezeka kutoka 144 mpaka 447, bado hawajalipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kilwa wanaathirika. Maeneo hayo ni katika Vitongoji vya Mchomoro na hususan Maeneo ya Mnazi Mmoja, Sanga, Utabiri pamoja na Kisangi. Wamekuwa wakiwasilisha hoja yao hii kila wanapopata fursa ikiwa ni pamoja na kunituma Mbunge wao kulieleza suala hili hapa Bungeni, nami nimelizungumza mara kadhaa ikiwa ni pamoja na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Bajeti. Nirudie, kutokana na athari ambayo wananchi hawa 447 wameendelea kuipata na kutolipwa fidia kwa muda mrefu, wamebaki wakiwa na makazi ambayo hayana hadhi, na wameshindwa kuyaendeleza kwa sababu tayari yapo katika utaratibu wa kulipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mheshimiwa Zainab Telack katika utaratibu wake wa kusikiliza kero za wananchi, alifika Kilwa Masoko. Moja ya hoja alizowasilishiwa ni pamoja na hii. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa akasema, "ninaichukua kwa lengo la kuwasiliana na wenzangu katika Serikali ili wananchi hawa waweze kulipwa fidia." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kwa msisitizo, Serikali ipo hapa Bungeni, walisikilize hili na wananchi wangu hawa walipwe fidia ndani ya muda mfupi ujao kabla hatujamaliza Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yahya Mhata, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbogo na Mheshimiwa Janejelly ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye ameniwezesha asubuhi hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuchangia Bajeti hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nimshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha kwamba jamii hii ya Tanzania inastawi na inasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukurani hizo, naomba nijielekeza katika maeneo yafuatayo: Kwanza, ni kilimo. Wilaya yangu ya Nanyumbu ni Wilaya ambayo ni ya wakulima, na kilimo chetu kikubwa cha biashara ukiondoa ufuta na karanga, ni korosho. Korosho ndiyo uti wa mgogo wa Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii tena kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa programu aliyoileta ya kuhakikisha kwamba wakulima wote wanapata pembejeo za kilimo bure. Kwa hili jambo, namshukuru sana. Vile vile Mheshimiwa Rais amekwenda mbele mwaka huu kwa kuielekeza Bodi ya Korosho iandae utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba kila mkulima

anapata pembejeo. Kwa hiyo, Bodi ya Korosho imekuja na utaratibu wa kusajili wakulima upya na kuhusisha taarifa za wakulima wa zamani ili nao waweze kuziboresha ziwe katika mfumo ulio sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Bodi ya Korosho ina changamoto, kwani imewaajiri vijana wetu ili wafanye kazi ya kusajili wakulima, lakini hawajawapa vitendea kazi. Wamewapa kazi, lakini wale vijana wanatakiwa watumie simu zao za mkononi. Hili jambo kwa kweli halikubaliki. Bodi ya Korosho wameshindwa hata kuwapatia viatu *(gumboot)*. Wale vijana wanaenda kusajili mashamba ya wakulima kwa kutumia viatu vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hiki cha mvua vijana wale wanakwenda kufanya kazi bila miamvuli. Sasa unaanza kujiuliza, lengo la Bodi ya Korosho ni kupata takwimu sahihi za wakulima au kufunika kombe mwanaharamu apite? Kwa sababu lengo ni kupata takwimu sahihi za wakulima wetu. Hawa vijana ambao wamekuwa *trained,* tulitegemea Bodi ya Korosho iwape vitendea kazi kama simu, *gumboot* na vifaa vya kujikinga na mvua. Badala yake vijana wamekwenda hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vijana hawa hawalipwi kama inavyotakiwa. Katika makubaliano ya Bodi ya Korosho ni kuwalipa vijana hao kila wiki. Hivi ninavyozungumza, kuna vijana wana wiki tatu au nne hawajalipwa. Nini matokeo yake? Matokeo yake taarifa ambazo Bodi ya Korosho inategemea izipate, hazitapatikana. Vile vile utakapokuja msimu wa kuwapa pembejeo, wakulima wengi watakosa pembejeo kwa sababu taarifa zao hazijafika kunakohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, lile zoezi ambalo linaendelea ndani ya Jimbo la Nanyumbu likafanywe vizuri. Taarifa zilizopo nyingi siyo sahihi na wakulima wengi takwimu zao hazitapatikana na hivyo

wakati wa kugawanya pembejeo watakosa pembejeo na hivyo kuathiri uzalishaji wa zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili ya zao hili la korosho ni bei kwa mkulima. Bei ya mkulima imekuwa ndogo mwaka hadi mwaka. Mwaka 2023 tumeshuhudia bei ya korosho imefika mpaka shilingi 1,200/= kwa kilo. Hili jambo linahuzunisha sana. Nilifurahi sana Bunge lililopita Waziri wetu, Mheshimiwa Bashe alipotoa msimamo kwamba kuanzia mwaka huu hasa zao la ufuta tutatumia utaratibu wa *TMX* badala ya utaratibu wa zamani. Naomba kusisitiza, *TMX* waingie sasa hivi kuanzia ufuta na mazao mengine yote yanayokwenda kwenye minada yetu. *TMX* ndiyo mwarobaini wa tatizo la bei ya korosho na mazao mengine ya maghala, kwa sababu utaratibu uliotumika unawanufaisha watu wachache. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, msimamo huu asije akaubadilisha, tunaitegemea *TMX* iingie katika zoezi la kufanya uhakiki wa bei za wakulima na jambo hili litamkomboa mkulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ushirika. Sisi watu wa Nanyumbu ni wazalishaji wakubwa wa korosho kama nilivyozungumza hapo awali. Mwaka 2022 tumezalisha tani 16,000 za korosho, mwaka 2023 tani 15 na *point something*. Jirani zetu Tunduru mwaka 2022 wamezalisha tani 15,000 lakini Tunduru wao wana Chama chao cha Ushirika. Sisi watu wa Nanyumbu tunategemea Chama Kikuu cha *MAMCU*. Nafikiri wakati umefika watu wa Nanyumbu tuwe na Chama chetu cha Ushirika ambacho kitahakikisha bei nzuri ya mkulima inapatika ndani ya Wilaya yetu. Kwa nini nasema hivyo? Ni jambo la kushangaza kwamba korosho za Nanyumbu zinakuwa na bei ndogo, lakini Korosho za Masasi zinakuwa na bei kubwa wakati ni ukanda ule ule. Sisi watu wa Nanyumbu tunazalisha korosho nyingi kuliko majirani zetu, lakini tunaendelea kuwa chini ya chama ambacho hakitusaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanalalamika bei ndogo, wanakosa vifungashio vya korosho na hawapati huduma sahihi

kupitia Chama Kikuu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleze, ni taratibu gani tuzitumie watu wa Nanyumbu ili tujitegemee tuwe na chama chetu Kikuu cha Ushirika? Vinginevyo, kwa kweli wananchi wetu wataendelea kuteseka. *(Makofi)*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango mzuri ambao mzungumzaji anaendelea nao, napenda kumpa taarifa kwamba, bei ya korosho inategemeana sana na ubora wa korosho. Kwa hiyo, kuna uwezekano wanalima korosho nyingi lakini labda ubora wa korosho hiyo hauko sahihi sana. Vile vile, inategemea na suala la masoko. Kuna wengine wanapenda *TMX* na wengine kama sisi watu wa Pwani tunapenda mfumo wetu wa Stakabadhi Ghalani wa kulaza boksi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Yahya, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake siipokei. Kwanza, katika korosho bora katika Mkoa wa Mtwara ni korosho ya Nanyumbu. Mzungumzaji ili apate bei nzuri, basi anazileta korosho zake kule na kuchanganya na zetu ili auze. Kwa hiyo, hiyo taarifa siyo sahihi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la pili ni kuhusu ardhi. Mheshimiwa Rais aliunda Kamati ya Mawaziri tisa, iliyozunguka Tanzania nzima chini wa Waziri wa Ardhi wa wakati ule, wakafika mpaka ndani ya Mkoa wetu wa Mtwara. Ndani ya Jimbo langu, moja ya Kata yangu iliathirika sana na zoezi hili hasa katika Vitongoji vya Namalomba, Wanika na Mbunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisafiri kutoka Mtwara hadi kwenye hizo Kata chini ya Waziri wa wakati ule Mheshimiwa Mama Mabula, na tulikubaliana kwamba wananchi wale watoke ndani ya vile vitongoji, wapangiwe maeneo mengine na watalipwa fidia. Kwa masikitiko makubwa, sasa ni mwaka mmoja, wale wananchi hawajalipwa fidia, wapo katika maeneo yale yale, hawajui hatima yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri aliyeteuliwa baada ya Mheshimiwa Mama Mabula, alikuja na Mheshimiwa Rais, akakutana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Nanyumbu akaahidi kwamba mara arudipo Dodoma, atahakikisha wananchi wale wanalipwa ndani ya wiki mbili. Nina masikitiko kwamba mpaka sasa hivi wale wananchi hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini matokeo yake? Wananchi wale wanaendelea kubaki na umaskini, hawajui hatima yao. Sasa watakapokuja hapa kufanya majumuisho, watueleze utaratibu wa wale wananchi kutoka katika maeneo yale upo au haupo? Vinginevyo napata tabu sana ninapokwenda kwenye vikao na wananchi wangu. Wataniuliza, nini hatima yetu? Sina majibu. Ukimwuliza Waziri, naye hana majibu. Sasa aje atuambie hapa, utaratibu wa wale wananchi kulipwa fidia ili waachie yale maeneo waondoke, upo? Vinginevyo tunazidi kuwatesa wananchi na tunawatia umaskini, kwa sababu hakuna kinachofanyika wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu lingine ni umeme. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa jitihada anazozifanya kuhakikisha kwamba umeme unapatikana katika nchi yetu. Hili jambo la kupongeza sana. Kwa kweli ni jambo la kushukuru sana. Kwangu, kati ya vijiji 47 ambavyo vilikuwa na changamoto kubwa ya umeme, bado vijijini vitano tu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda hautoshi, lakini naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Namwita Mheshimiwa Mbogo, atafutiwa na Mheshimiwa Janejelly na Mheshimiwa Cherehani ajiandae.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuwaletea wananchi maendeleo katika sekta mbalimbali za afya, elimu, miundombinu pamoja na mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo Nkasi Kusini lina barabara za kiuchumi ambazo ni barabara ya Wampembe - Kala - Mpasa - Kizumbi. Hizi barabara zimeathirika sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali itenge fedha za dharura ili ziweze kwenda kufanya matengenezo ili wananchi waendelee kupata usafiri na huduma za kiuchumi na biashara zao ziendelee, kwa sababu zinaelekea ukanda wa Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, zilipokatika, wananchi wamebaki kwenye kisiwa. Ziwa likichafuka, hawana pa kwenda. Kwa hiyo, wagonjwa wengine wanakufa kwa sababu miundombinu imeharibiwa. Nilikuwa naishauri Serikali itenge fedha kwa haraka iende ikatengeneze hizo barabara za Wampembe - Kizumbi - Kala - Mpasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni umeme. Yapo maeneo ya uzalishaji ya vijiji, ambayo nilikuwa naomba kabla hii miradi ya umeme kwenda, ukafanyike utafiti kwenye yale maeneo ambayo vijana wamejiajiri katika maeneo ya uzalishaji, ndiyo waanzie huko kupeleka umeme. Mfano, Vijiji vya Masamba, Kyela, Mwinza, Izinga

Kapumbuli na Kilambo cha Mkolechi. Haya maeneo ni ya uzalishaji ukanda wa Ziwa Tanganyika na yanahitaji umeme. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la fidia. Kuna barabara hizi za *TANROADS* zilijengwa. Nyumba nyingi zilibomolewa hasa Kijiji cha Chala. Watu hawaelewi kuwa wananchi wanacheleweshewa maendeleo. Naomba wananchi wangu wapatiwe jibu, wanalipwa ama hawalipwi, ili waendelee kufanya shughuli zao za maendeleo na kujenga nyumba bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Nkasi Kusini, Kata ya Kizumbi na Ninde yapo maeneo mazuri ya kuanzisha uboreshaji wa skimu ya umwagiliaji, lakini katika jimbo zima hakuna skimu hata moja na haya maeneo Kata zilishaandaa. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Kilimo iende kuanzisha skimu za umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Nkasi Kusini pamoja na Mkoa wa Rukwa, kuna Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika, lakini hatuna Chuo cha Uvuvi. Hawa wananchi hawapati elimu ya uvuvi. Pamoja na kupumzisha ziwa na mikakati mingi, lakini kama wananchi hawana *centre*, hawana chuo cha kupata elimu ya uvuvi itakuwa ni kazi bure. Hata tukipumzisha ziwa, samaki wakazaliana, uvuvi haramu utaendelea, kwa sababu wanavua kienyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu wa Waziri Mheshimiwa Mnyeti, alifika Rukwa na nilimwomba akatuahidi ujenzi wa Chuo cha Uvuvi Kata ya Wampembe kati ya Kata tatu ili wananchi wafike pale wapate elimu. Wananchi wa Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa wapate elimu waanze uvuvi wa kisasa. Naomba kwenye bajeti uwekwe huo ujenzi wa Chuo cha Uvuvi Kata ya Wampembe, Jimbo la Nkasi Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala ambalo linachanganya sana. Kwanza niwape pole wananchi wa Wilaya ya Nkasi, Ukanda wa Ziwa Tanganyika. Nimefanya takwimu, ndani ya miaka mitatu, siyo chini ya wananchi 30 wameliwa na mamba ikiwa ni pamoja na

wanafunzi, kwa sababu wengi wanafuata huduma ya maji katika Ziwa Tanganyika. Wakienda kule wanakutana na mamba, wengi wameliwa na mamba hasa wanafunzi na watu wazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hizi tatu; Wizara ya Uvuvi, Mheshimiwa Mnyeti, Naibu Waziri wa Uvuvi, naomba unisikilize Bwana! Hili suala lipo *serious,* na picha nilimtumia Waziri wa Maliasili watu wanavyoliwa na mamba. Wapo wavuvi ambao unawapumzishia ziwa, wanaliwa na mamba. Kwa hiyo, Wizara ya Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Wizara ya Maji wakae pamoja watenge bajeti waende wakaainishe maeneo yaliyo salama kwa kila kijiji ili wananchi wajue kuwa wanapoenda kutafuta huduma ya maji, ni sehemu salama. Kwenye maeneo hatarishi wawekewe mabango, wajue, kwa sababu wanaoliwa ni wanafunzi na wananchi wanaofanya biashara za samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais, alihamasika sana kutoa ruzuku za mbolea na wananchi wamelazimika kulima, na mwaka huu kuna mavuno mengi sana ya mahindi. Naomba Wizara itenge na iongeze vituo vya ununuaji wa mazao, mwananchi asije akapata gharama ya kusafirisha mazao mbali kutoka eneo analolima. Mfano, Kata ya Kala na Kate kutengwe vituo vitakavyomwezesha mwananchi kutokupata gharama ya kusafirisha kutoka eneo la kununulia mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo shule chakavu sana hasa sekondari zile kongwe. Mfano, Sekondari ya Chala ni kongwe, iliyojengwa na wazazi, haikujengwa na lenta, imeharibika. Itengwe bajeti ikaboreshwe pamoja na kupatiwa madawati. Kuna shule za msingi zimechoka, mfano, Shule ya Msingi Yondokazi, Liyapinda, Sintali na Ninde. Hizi shule zimechoka, pamoja na Mahakama za Mwanzo. Mfano, Kata ya Kate, mahakama wanayotumia ni godauni, huku wameweka magunia, huku hakimu anaendelea kuendesha kesi; na nyingine ni Mahakama ya Mwanzo Kata ya Chala. Mahakama hizo zimechoka, naomba zitengwe fedha ili ziweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly, atafuatiwa na Mheshimiwa Cherehani na Mheshimiwa Kasalali ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Baraza lake la Mawaziri. Napongeza sana Baraza lote la Mawaziri kwa sababu kazi waliyofanya ya kumshauri Mheshimiwa Rais ni kubwa sana hasa upande wa watumishi wa nchi hii. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kuanzia Ibara ya 151 kuhusu Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Nawapongeza. Nakumbuka nilipoingia Bungeni, jambo la kwanza nilililia ni Vyama vya Wafanyakazi na Serikali kupeana elimu ya ushirikishwaji, wote kuelewa wanatakiwa wafanye nini? Maana vyama na Serikali hatutakiwi kuwa wagomvi. Tunatakiwa kushauriana kwa sababu tunajenga nyumba moja, tusigombanie fito.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa kuwa naona suala hili wamelifanya, wametoa semina kwa watendaji wa vyama 12 kati ya 33. Nashauri waongeze juhudi hizi ili vyama vyote vipate hiyo elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwani tukiwa Morogoro Mei Mosi, tulikuwa tumeongea humu ndani ya Bunge na niliongea kuhusu vitendea kazi na ameweza kununua magari 30 kuwapa ile Idara ya Elimu na elimu tunaona imeenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara za Elimu kwa kweli sasa hivi ukizunguka huko unawaona kazi wanayofanya imesaidia, wameweza kutoka na kufuta migogoro ya watumishi 5,056, sasa wameenda mpaka 5,678. Siyo suala dogo, wameenda nusu ya kazi.

Hii imesababishwa na kuwa na huduma ya usuluhishi wa migogoro inayotembea. Sasa tuifanye iendelee iwe ni nchi nzima. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee usalama wa afya mahali pa kazi. *OSHA* wanajitahidi sana, lakini kuna baadhi ya watumishi bado wanakwamisha utekelezaji wa haya wanayoyatekeleza. Mkoa wa Dar es Salaam tuna viwanda vingi sana na huwa nafanya ziara kwenye viwanda hivyo na shahidi atakuwa ni Mbunge wa Jimbo la Temeke kwa sababu ana viwanda vingi sana kwenye Jimbo lake kama Mbunge wa Jimbo la Mbagala, lakini ukaguzi unaofanyika pale, nashauri tuuangalie kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna viwanda siwezi kuvitaja majina kwa sababu ni wawekezaji wetu, lakini niwape kazi ya kwenda kufanya. Unakuta watumishi wamefungiwa mle…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** …unakuta hewa hamna, hawana zana za usalama na wanafanya kazi hatarishi. Nilimwita Mbunge wa Temeke awe shahidi. Kiwanda kimefungwa je, hapa ikitokea ajali inakuwaje? Mwenye kiwanda anasema, "nafunga kwa usalama, wasiniibie." Sasa maisha ya watumishi wetu na wananchi wetu ni bora kuliko mali zilizopo pale! Nawaomba *OSHA* waende kukagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama ni pamoja na hali ya mtumishi yule, atakuwaje wakati yupo sehemu ya kazi? Niliwahi kukutana na watumishi wa *OSHA* na watakuwa wananisikiliza. Niliwaambia, subiri nirudi Bungeni. Wakifika hawakagui, nami wakati mwingine huwa navaa dera, naenda kama ombaomba kwenye viwanda ili nijue kinachoendelea kwa watu ninaowawakilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wale watumishi wamekuja pale, yule mwenye kiwanda anasema wameshakuja *OSHA*, vyoo vinafungwa ili wasiende kuangalia usafi wa vile vyoo kule ndani,

lakini kwa sababu nilikuwa nimejifanya mteja siku hiyo, nikawaambia naomba kwenda chooni. Kile choo hawezi kukitumia binadamu, lakini *OSHA* wanatoa *certificate* safi na unaikuta ukutani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna watumishi ambao bado wanaihujumu *OSHA*. Wanamaliza nguvu ya Mkurugenzi. Kwa kweli Mkurugenzi anajitahidi sana sana. Nadhani siku hiyo nilimpigia simu nikamwambia angalia walio chini yako wanakuangusha. Kwa hiyo, naiomba Serikali wakaliangalie hilo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uwajibikaji wa wafanyakazi. Kwa kweli kwa sasa hivi wanawajibika sana, lakini sasa wajibu unaendana na haki; na hili nitaongea sana ikifika Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Bado tuna watumishi wanadai madeni, hapa kuna mtumishi alituma *message* kwa Profesa hapa akasema mwambie Mheshimiwa Janejelly leo aongelee kuhusu nauli zetu za likizo. Bado kuna watumishi hawajalipwa nauli zao za likizo. Sasa kwa hili, tunaharibu maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye yeye ameshaamua watumishi wakae kwa amani, wafanye kazi kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaiongea sana tukifika kwenye Wizara ya Menejimenti ya Utumishi, na Wizara ya Fedha kwa sababu hili tatizo ndiyo lipo kule. Mathalan, madeni ya Walimu, fedha zao huwa zinatoka moja kwa moja Wizara ya Fedha, lakini haipelekwi kwenye zile halmashauri. Kwa hiyo, walimu wanagombana na wakurugenzi kwamba hawajawalipa, lakini ni kwamba mkurugenzi anakuwa hajapelekewa ile bajeti kutoka Wizara ya Fedha hasa hela za nauli ya likizo. Naomba Serikali iliangalie hilo kwa makini sana. Tusiwakorofishe hawa watumishi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la maslahi ya kustaafu. Naomba waongeze *speed* ya kulipa fedha za kustaafu (pensheni). Hebu tufanye haraka ya kuwalipa hawa watumishi wetu. Kuna kipindi walikuja na utaratibu mzuri kwamba, kama pensheni

inachelewa, basi miezi mitatu huyu mtumishi awe ameingizwa kupata yale malipo ya kila mwisho wa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niomba Serikali ifanye hilo hasa upande wa walimu, maana bado wanalia sana, wanalalamika sana na hawa ndio tunaowategemea wawajenge ninyi mawaziri. Hakuna Waziri ambaye hakufundishwa na mwalimu na wala hakuna Mbunge huku ambaye hakufundishwa na mwalimu. Kwa hiyo, tujaribu kuliangalia sana hilo, kwani bado kuna malalamiko hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nikisoma *message,* nitamletea Mheshimiwa Waziri Jenista aone, wanalalamika sana na yawezekana hata elimu ya kikokotoo hatujaitoa ipasavyo kuwaambia faida na hasara zake. Bado wapo kwenye giza, hawaelewi kwamba wanacholipwa kimetokana na nini? Kokotozi zimeendaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni elimu ya kuwaelimisha, yawezekana tunachofanya kina faida, lakini kwa sababu hatujawapa elimu, wanaona kama wanaonewa sana na hawajatendewa haki kwa miaka waliyokaa kazini. Naomba wapewe elimu ipasavyo ili tuwaweke sawa watumishi wa Serikali waelewe ni kwa nini tulifikia malengo hayo ya kusema pensheni sasa isiwe asilimia 50 na iwe asilimia 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana tutoe hiyo elimu kwani imeleta sintomfahamu. Elimu inatakiwa sana. Tukiwaelimisha watajua maana ya kwa nini iliamuliwa hivyo? Tukikaa kimya, wao wanaona kama wameonewa, hela zao zimeenda sehemu nyingine ambapo hazikutakiwa kwenda, kumbe haipo hivyo, yawezekana ni kwa nia nzuri tu. Nawaomba tukalifanyie kazi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni *promotion*. Jana hapa limeulizwa swali na Mheshimiwa Jenista akiwa utumishi ndiyo alikuja na hili suala kwenye bajeti, na kweli waliitenga bajeti na vyeo vya

msererereko vikaruhusiwa. Hata hivyo, kuna sintofahamu kwa wale wasimamizi, tunaenda kwa kuangaliana sura. Hili nalisema bila kuficha. Wanavyopeleka msererereko unakuta wamemsereresha mtu wa mwaka 2018, wamemwacha wa 2014. Sasa unashindwa kuelewa wanatumia kigezo gani? Maana tunaelewa kuserereka huyu aliyetangulia huku kupata cheo cha kwanza ndiye angeserereshwa ili aende kwa haki yake iliyokuwa inatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nasubiri Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, tutakutana kwenye bajeti yake. Katika hilo, majibu wanayotoa wataalam siyo halisi na kinachotendeka kule kwenye eneo la tukio. Wanawaletea taarifa kwamba tumesereresha, lakini kuna watu bado wameachwa na ukiuliza sababu, hawakupi majibu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, huwa naongea na Maafisa Utumishi kwenye manispaa ninayotoka, kwamba, hivi wanaelewa wanachofanya? Sasa unamwacha huyu wa mwaka 2017, unamsereresha wa mwaka 2018, haki ipo wapi? Serikali imekuja na nia nzuri tu kwamba hao watu waserereshwe, wapate haki yao. Naomba, aidha, Maafisa Utumishi wapewe mafunzo, ni kwa sababu wanakaa muda mrefu hawajaenda mafunzo? Sielewi! Siyo kwamba nawatuhumu, ila nasema kile ambacho watumishi wanakutana nacho. Hilo la msererereko tuliangalie kwa sababu nia ya Serikali ilikuwa ni nzuri sana, kuwapa watumishi maslahi yao. Naomba tuliangalie sana hilo, kwani linatuletea sintofahamu huko chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Serikali ndiyo ilitaja watendaji wapewe ile shilingi 100,000/=. Hivi ugumu uko wapi? Nimepiga kelele, nimeuliza maswali ya msingi, lakini bado hao watendaji hawalipwi haki yao. Shida ipo wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichunguza shida ilipo, hili halijafanywa kama ni *first charge,* halijafanywa kama ni *priority* kwenye manispaa zetu. Hawaoni kama ni kitu cha muhimu kumlipa

huyu mtendaji haki yake? Leo nairudia, hii ni mara ya nne ndani ya Bunge hili, hata ukiangalia *Hansard,* naongelea hizi posho za watendaji. Shida ni nini? Tatizo liko wapi? Basi kama tuliona tulilitoa tu kwa utashi wa kisiasa, haliwezekani, tulifute.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Cherehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali na Mheshimiwa Shamsia Azizi ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambazo anazifanya kwenye nchi yetu ya Tanzania hasa kwa upande wa wakulima, hali ya ruzuku ya pembejeo, na pia masoko yanazidi kuongezeka, bei za wakulima wetu zinazidi kupendeza. Tumshukuru sana pia Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambazo amezifanya kwenye mradi mkubwa wa maji wa Bwawa la Nyerere ambapo sasa tunaenda kuondoa kabisa kero ya umeme kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Kamishna wa Madawa ya Kulevya nchini, Ndugu yetu Lyimo kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwenye nchi yetu kuteketeza mashamba mengi ya bangi, kukamata wauzaji wa madawa ya kulevya. Ni kazi kubwa ambayo anaifanya kijana wetu, lazima tumtie moyo, lazima tumpe nguvu kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite sana kwenye suala la barabara. Hali ya mwaka huu imekuwa ni ngumu sana katika maeneo mengi hapa nchini hasa katika Jimbo la Ushetu. Nawapongeza Wizara ya Ujenzi kwa kazi kubwa ambayo wameifanya hasa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ndugu yangu Mheshimiwa Bashungwa, amezunguka katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kukagua barabara, lakini kazi ambayo naiona ni

usimamizi hafifu, kwa sababu maeneo mengine hata mvua ikinyesha kidogo tu, unaona madaraja yanaenda na maji, ma-*calvat* yanabomoka kwa sababu namna ya ufuatiliaji wa barabara zetu na usimamizi kwa wakandarasi umekuwa ni hafifu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Ujenzi iwasimamie wakandarasi kwa sababu kama hajafika Waziri eneo lile katika mkoa ule pia kuna Meneja wa *TANROAD*. Hawa watu wanafanya kazi gani kwenda kukagua wakandarasi wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia barabara nyingi zinazojengwa, haziwekewi mitaro ya maji. Sasa niendelee kuwaomba, zamani niliona Mawaziri wakati mwingine walikuwa wanazunguka, watu wa *TANROAD* wanazunguka mpaka na nyundo kugongagonga kuona usimamizi mzuri wa barabara. Ukiangalia hata zile lami zinazojengwa kabla hata mkandarasi hajakabidhi mradi, tayari unakuta barabara imeanza kubomoka, imeanza kuwa na mashimo na kuanza kuwekewa viraka. Unafika mahali magari yanapata ajali wakati mwingine kupitia yale mashimo ambayo mkandarasi ameshindwa kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama Wizara ya Ujenzi ina changamoto ya nyundo kukagua zile barabara, nipo tayari kuwapa zile nyundo ili wakandarasi wakakaguliwe kuhakikisha barabara zinakuwa imara na fedha anazopeleka Mheshimiwa Rais kwenye ujenzi wa barabara zetu ziweze kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu baada ya mwaka mmoja, kunahitajika marekebisho, na baada ya muda mfupi yanahitajika marekebisho. Hizo fedha zingefanya kazi nyingine hata kununua madawa katika hospitali zetu. Kwa hiyo, naomba eneo la ujenzi wakandarasi wakasimamiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tuna changamoto ya utunzaji wa mazingira. Jana katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 78 ameongelea sana suala la nishati, lakini tunagawa

gesi na gesi hizi nyingi zinagawiwa mjini. Niendelee kuwaomba Wizara ya Nishati, wakae na watu wa maliasili na kama kuna fedha ambazo wanazitenga kwa ajili ya kukusanya kwenye maeneo yetu, kwenye mageti, naomba wakusanye fedha wakawape ruzuku wananchi wetu kwa ajili ya mitungi ya gesi. Kwa sababu ukiangalia wananchi wana mwitikio mkubwa sana, na jana Waziri alitoa taarifa akasema wameanza kutoa mitungi ya kilo tatu, tano na sita. Hongera sana kwa Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuwaomba waweke ruzuku. Kama Serikali imeweka ruzuku kwenye mbolea, imeweka ruzuku kwenye mafuta na leo hii tunaenda kudhibiti ukataji miti na uharibifu wa mazingira kwenye nchi yetu, naomba waweke ruzuku pia kwenye matumizi ya gesi. Unakuta gharama ya kuweka mtungi mmoja ni zaidi ya shilingi 30,000. Sasa mwananchi yupo kilometa 30, mitungi ya gesi inayopatikana ipo mjini, ipo kwenye Makao Makuu ya Halmashauri, lakini kwenye kata zetu na vijiji hakuna mahali ambapo inauzwa mitungi ya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaposema kuelekea 2025/2026 tunaenda kuwa na mabadiliko makubwa sana ya utunzaji wa mazingira, wananchi wote watumie gesi, wanaenda kuipata wapi? Mwananchi ili asafiri kupata mtungi wenye gesi, leo tunagawa mtungi labda katika kijiji fulani, lakini ili aende kupata mtungi wenye gesi atembee kilometa 70; nauli ni shilingi 10,000, kwenda na kurudi ni shilingi 20,000, mtungi ni shilingi 35,000, jumla ni shilingi 55,000. Wananchi wa maisha ya kawaida wanapata wapi zile fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iweke ruzuku kwenye upande wa mitungi ya gesi ili tuwasaidie wananchi waweze kupunguza matumizi ya kukata kuni, tuelekeze nguvu sasa kwenye ruzuku. Mfano maliasili, pale wanatumia fedha nyingi sana kwenye magari mengi sana kukimbizana na wananchi wetu. Nenda kwenye mageti yote ya *TFS,* wameweka mageti lakini wanakamata baiskeli zetu. Mwananchi wetu wa maisha ya kawaida hasa sisi wenye

majimbo ya vijijini, kuipata baiskeli, mwananchi wetu anatumia zaidi ya miaka miwili, ananunua baiskeli ya shilingi 150,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwananchi huyu anabeba gunia lake la mkaa, amelipia vibali, anakuja kufanya kosa dogo ananyang'anywa baiskeli yake, au pikipiki yake, lakini zinalundikwa kwenye mageti halafu matokeo yake hawarudishiwi, hata utaratibu kwamba watazipataje, hakuna. Yaani wananchi na watu wa maliasili ni kama wana vita hivi. Sasa mahusiano ya kikazi hayapo. Mwisho wa siku zinapigwa mnada na kuchomwa moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Maliasili iweke utaratibu wa kuwarejeshea wananchi wetu baiskeli zao walizozikamata kwenye mageti, walizozikamata kwenye ofisi zao ili zisaidie kwenye kujenga uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda siyo mrefu tunaenda kuwaomba kura wananchi wetu na hawa wananchi walio wengi ndiyo wapigakura wetu wazuri na wanafanya kazi nzuri ya kujenga uchumi wa nchi yetu. Leo hii wanaenda kukamatiwa baiskeli zao, zinakusanywa, nendeni kwenye mageti yote Waheshimiwa Wabunge wenzangu hasa kwenye mageti ya majimbo ya vijijini, baiskeli zimelundikana kule. Sasa kwa nini Maliasili isiweke utaratibu mzuri na rafiki kabisa wa kuhakikisha hata kama umemkamata mwananchi, basi mpe utaratibu mzuri wa lini atakuja kukomboa baiskeli yake? Anakuja kukomboaje pikipiki yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya hili ni kwamba mwananchi anarudi tena kukusanya fedha yake kwa muda wa miaka mingine kununua baiskeli. Wananchi wanakuwa na hasira na sisi. Kwa hiyo, niendelee kuiomba Maliasili, leo tuna miaka 60 ya uhuru, karne ya 21 bado tunakimbizana na wananchi na magari. Sasa kwa nini zile gharama za mafuta na za kulipa wale maaskari tusizipeleke kwenye ruzuku ya mitungi ya gesi ili kuwapunguzia wananchi kukata miti?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mikopo ya asilimia kumi, kuna Halmashauri zilifanya kazi vizuri, zilikuja kuponzwa na Halmashauri chache ambazo hazikufanya kazi vizuri. Naomba ufanyike utafiti wa kutosha kabla hatujazuia kitu kama hiki, tunazuia mikopo kwa akina mama, tumezuia mikopo kwa walemavu na kwa vijana wetu waliokosa ajira, walikuwa wanapata fedha huko, wanapata hizi bodaboda wanaendesha, wanajiajiri, lakini leo hii tumezuia mikopo nchi nzima. Leo ni karibu mwaka wa pili, hawa vijana walikuwa na mitaji yao sasa wanateseka wanarejeshaje marejesho benki wakati tayari sasa utaratibu wa kukopeshwa tena umeshasimamishwa nchi nzima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kosa la watu wachache linasababisha nchi nzima kukosa mikopo. Naomba uwe unafanyika upembuzi mzuri. Pia kuna hawa vijana wetu wanaozidi miaka 35 waliotoka vyuo vikuu, hawana ajira, hawajapata ajira, wako mitaani, lakini hili kundi bado halihesabiki kukopeshwa. Naomba Wizara inapokuja, ije pia na utaratibu wa hawa wananchi wetu vijana ambao wanazidi miaka 35, kwa sababu hata kwenye ajira hawajapata, lakini wanapoenda upande wa pili tena wanaambiwa umri umezidi. Sasa hili kundi nalo ni kubwa, tulifikirie kwenye utaratibu wa kuingia kwenye asilimia 10, liweze kupata mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naendelea kuiomba Wizara ya TAMISEMI, inabebeshwa mizigo mikubwa sana. Ukiangalia zahanati ziko TAMISEMI, shule za msingi ziko TAMISEMI, sekondari ziko TAMISEMI, Hospitali za Wilaya za Halmashauri ziko TAMISEMI, leo hii pia Maafisa Ushirika na wenyewe wako TAMISEMI, sasa hawa TAMISEMI wamepewa mzigo mzito mno wa namna ya usimamizi wa zahanati zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Hospitali za Halmashauri na Wilaya zipelekwe Wizara ya Afya zikasimamiwe vizuri ili tuwapunguzie mzigo hawa TAMISEMI. Ndiyo maana sasa unakuta hata matukio mengine yanapotokea, namna ya usimamizi kwa wataalam wetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante. Ni kengele ya pili hiyo.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali, atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima. Pia nakupongeza wewe kwa namna ambavyo unakiongoza kikao hiki vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na njema, ya maana anayoifanya kwa Watanzania, kwa bajeti ambazo amekuwa anatuletea hapa na sisi tukizipitisha na namna ambavyo zinaonyesha matunda chanya kwa Watanzania wa mijini na vijijini. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye leo bajeti yake ndiyo tunaijadili hapa. Amekuwa ni mtu mwema, mchapakazi, msimamizi mwema na msaidizi mwema wa Mheshimiwa Rais na Watanzania wote. Nampongeza kwa jambo hilo na ninaomba nitumie nafasi hii kumtia moyo yeye na Waheshimiwa Mawaziri wanaofanyanao kazi ofisini kwake; Mama yangu Mheshimiwa Jenista na Manaibu wake wote, Mheshimiwa Deogratius na Naibu Mawaziri wengine wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mniruhusu nizungumze maneno machache ya kushauri namna bora ya kuwahudumia Watanzania, na kwa sababu leo tunazungumza na Ofisi ya

Msimamizi wa Mawaziri wote, naamini kupitia yeye watanielewa na kutekeleza yale ambayo nitayashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichonileta humu ndani ni wananchi wa Sumve ambao walinipigia kura, na kuna mambo niliwaambia nitafanya kwa kushirikiana na Serikali kwa kuishauri. Sasa yale mambo ambayo tumekuwa tukiwashauri na kusimamia Serikali, tunashukuru yamefanyika mengi, lakini kuna jambo la msingi sana kwenye Jimbo la Sumve naliona kama vile haliko sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ni ya kwetu sote. Watanzania wote tunalipa kodi na tunategemea maendeleo yanapokwenda kwa Watanzania yaende walau kwa kuangalia kila eneo linapata nini? Maendeleo yanapokuwa yanajazana labda Dar es Salaam, tunaona sijui trilioni ngapi zinajenga mwendokasi, halafu Sumve tangu niwe humu, leo ni mwaka wa nne huu Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wake wamekuwa wakinisikia nikisema kwamba kuna Jimbo kule linaitwa Sumve halina hata milimita moja ya lami. Halafu nikimaliza kuongea hivyo, anatokea Mheshimiwa Waziri anayehusika anatoa ahadi lukuki na hatekelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza kuzungumzia suala la Wilaya yetu ya Kwimba kuunganishwa kwa lami na Mkoa wa Mwanza tangu nilipoingia humu, sioni utekelezaji, naona majibu yasiyotekelezwa. Nimeanza kuhangaika na Mheshimiwa Dkt. Chamuriho akiwa Waziri wa Ujenzi, akawa ananikalisha pale kwenye kiti chake kila siku ni ahadi lakini hakuna kitu. Nikaenda kwa Prof. Mbarawa, akapata hiyo nafasi, tena yeye tulikwenda ofisini kwake Wabunge wote wa Mwanza, tukaahidiwa, lakini hakuna kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi yupo kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa, naye hakuna kitu. Nikiongea nao wananiambia michakato ya manunuzi, na kadhalika. Yaani wananchi wa Sumve na watu wa Kwimba hawajui hayo mambo ya upembuzi yakinifu na hayo manunuzi. Wanachojua ni lami itokee

Magu ipite Bukwimba iende mpaka Hungumalwa, tuunganishwe na sisi. Wanachojua ni lami itokee Fukalo ije Nyambiti iende Malya ili iunganishe na mnyororo wa utalii wa Mbuga ya Maswa na Mbuga ya Serengeti tufaidike na utalii. Sasa hatuwezi kuendelea hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka nikichangia bajeti yangu ya pili, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Waziri wa Fedha wakati ule aliniandikia mpaka *memo* ya kuniambia kwamba, tunajenga hivi na hivi. Baadaye tena wakasema sijui wanakopa nini? Yaani hawajengi, kila siku ni *story* tu. Sasa wananchi wa Sumve wameniambia hivi, ukifika Bungeni kwa heshima waliyonayo na Ofisi ya Waziri Mkuu na namna ambavyo mambo yanakwenda, wewe nenda ukaunge mkono bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama itafika bajeti ya ujenzi, halafu hakuna mambo yanayoeleweka, usiiunge mkono. Watu wa Ujenzi niko *very serious* kwenye hili. *Very serious,* na sitaki mchezo. Wananchi wa Sumve wanataka na wenyewe wawe na lami. Haiwezekani ninyi kwenye Majimbo yenu mna lami, sisi hatuna halafu bado tunakuja humu wote tunaitana Wabunge. Ni lazima tuheshimiane kabisa. Hatuwezi kuwa tunakuja hapa tunaahidiwa vitu ambavyo havitekelezwi. Haiwezekani. Ni bora sasa sisi watu wa Sumve tuambiwe hatuhusiki humu. Kitu cha msingi hapa tunataka lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu waambie Mawaziri wako wanaohusika, waache kuwapa ahadi hewa watu wa Sumve. Nami Mbunge wa Sumve sitaki ahadi hewa kwa niaba ya wananchi wangu. Tunataka na sisi tujengewe barabara ya lami, *story* za kilometa 10 mnazotuambia ambazo na zenyewe hamjengi, sisi hatuko *interested* na kilometa 10 za kulambishwa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka lami ambayo itatufanya na sisi tuweze kwenda mjini na magari yetu mazuri, lakini hii namna ya

kutufanya sisi tuwe tunatuma nginjanginja, ninyi mnatanua na magari mazuri mjini, haipo. Watu wa Sumve wameniambia kuhusu miundombinu mtatusamehe, tunataka barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo naomba nihamie kwenye suala lingine la ushauri tu. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa kuhusu suala la kikokotoo. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua ambazo amezichukua na maelekezo ambayo amekuwa akiyatoa na kuonesha moyo na nia ya kutamani jambo hili liende na liishe vizuri ili watumishi wetu waishi kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kikokotoo linakuja kwenye hoja ya kwamba ukiliangalia kwa undani lina hoja, kwamba watumishi wetu uwezo wao wa kutunza pesa na kupanga matumizi ya pesa ni mdogo. Ndiyo hoja ya kikokotoo inakuja hapo. Yaani watu wakipewa hela zao hawataweza kuzitumia vizuri, hawatazitunza vizuri, kwa hiyo, sisi Serikali tuwatunzie, tutawapa kidogo kidogo. Ndiyo hoja yenyewe ukiiangalia ukubwa wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka tujadiliane hapa kwa kushauriana, hawa watumishi ndiyo leo wako kwenye maofisi, ndiyo leo wanatuletea makabrasha yote tunajadili bajeti hapa, ndiyo leo wamepanga kila kitu huko, ndiyo hao wanaolinda nchi yetu na ndiyo hao wanafanya kila kitu, lakini tukifika wakati wanastaafu sasa, maana unajua huwa tunasema kwenye utumishi tunataka *experience*. Hawa watu mpaka wamestaafu wana uzoefu na matumizi ya pesa, wana uzoefu na maisha na wanajua wanafanya nini. Eti sasa wakishazeeka tunawaona hawa hawawezi kutunza pesa zao, tuwatunzie tuwe tunawapa pole pole. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye *logic* inaonekana kwamba siyo jambo jema. Jambo hili sisi tunasema ni zuri. Kuna wakati niliambiwa hapa sijafanya utafiti, lakini ukweli ni kwamba huko *site* hili jambo halijaingia kwenye vichwa vya watumishi, yaani

limefeli na hawalielewi na wale ambao wamelazimika kuingia kwenye kikokotoo, wengi imewa-*frustrate*, wengi wanakufa kabla ya muda.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali, ahsante sana.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iliangalie jambo hili kwa jicho lingine. Nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Shamsia atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda na Mheshimiwa Mpakate ajiandae.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nzuri na leo hii nimeweza kusimama katika Bunge hili. Kwanza, nachukua fursa hii kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha analeta maendeleo mijini na vijijini. Mwenyezi Mungu amjalie afya Mheshimiwa Rais wetu, azidi kutuletea maendeleo katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Jenista Mhagama na dada yangu Mheshimiwa Ummy Nderiananga, kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi kubwa katika Wizara hii. Mwenyezi Mungu awajalie na ninawaomba waendelee kuitumikia vema Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 16 Septemba, 2023 Mheshimiwa Rais alikuja na kufanya ziara katika Jimbo langu. Moja

ya changamoto kubwa ambayo nilimpa Mheshimiwa Rais ni maji katika Kata ya Nanguruwe Kijiji cha Nanguruwe. Kwa masikitiko makubwa, ule mradi Rais alisema ufanyike haraka ili wananchi wa Kata ile waweze kufurahia huduma hii muhimu ya maji safi na salama. Tokea terehe hiyo ambayo Mheshimiwa Rais alikuja mpaka kufikia leo, unasuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana kaka yangu, Mheshimiwa Waziri wa Maji, wewe ni msikivu na unafanya kazi nzuri, naomba ufuatilie suala la maji. Wananchi wangu walikuwa na mategemeo makubwa, wana shida ya maji na wanataka kuona mradi huu umekamilika haraka ili waweze kupata huduma hii muhimu ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa inayolikabili Jimbo langu la Mtwara Vijijini ni changamoto ya maji, lakini vyanzo vya maji vipo. Tunacho chanzo cha Maji cha Mayembechini na tuna Chanzo cha Maji cha Mto Ruvuma, uthamini ulishafanyika na mchakato wa kuhakikisha wanamaliza tatizo la maji kwa ujumla katika Mkoa wetu wenye changamoto ya maji, lakini mpaka leo mradi huu unasuasua. Uthamini ulifanyika kwa wananchi, wananchi wale toka wamefanyiwa uthamini mpaka leo hii hawajui kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji hivyo ambavyo vimefanyiwa uthamini ni Kijiji cha Kitaya, Kihamba, Dindwa, Kivava, Mahurunga, Kihimika, Magomeni Nyasi, Tangazo, Litembe, Litambo, Ziwani, Namindondi, Mtendachi na Mtawanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2015 takribani miaka 10 mpaka kufika hii leo wananchi hawa hawajalipwa fidia, wanashindwa kuendeleza maeneo yao, hawana wanachokielewa mpaka sasa hivi. Sasa naomba *commitment* ya Serikali, ni lini wananchi hawa watalipwa fidia? Kama hakuna fidia na hakuna chochote kinachoendelea, basi wawaruhusu wananchi hawa waendeleze maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nina chambamoto. Kuna kata moja inatwa Lipwidi, tokea tumepata uhuru kata hii haijawahi kufurahia huduma hii muhimu ya maji safi na salama. Naiomba sana Serikali iiangalie Kata hii. Wananchi wapo katika mazingira magumu sana. Wananchi wanakunywa maji machafu sana karne hii. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Maji na Serikali iangalie kata hii kwa jicho la huruma ili wananchi wangu waweze kufurahia huduma hii muhimu ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala la barabara. Tokea nimekuwa Mbunge wa Viti Maalum, nimekuwa nikiililia sana barabara ya uchumi, barabara inayotoka Mtwara Mjini kuelekea Msimbati ambako kuna mitambo na visima vya gesi kule. Natamani kulia maana hali ni mbaya. Sehemu kubwa ambayo imewekezwa na Serikali, barabara ni mbovu. Juzi nilikuwa huko, barabara haipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wakija hapa, nikiwauliza maswali tokea kipindi hicho mpaka leo majibu yao hayaridhishi. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini, naiomba Serikali iangalie barabara hii ya uchumi iwekwe lami. Hivi yakitokea ya kutokea, hatuombei yatokee, lakini kule kuna vitu muhimu Serikali inawekeza. Leo hii kukitokea la kutokea kule, kutoka mjini mpaka kufika kule si tutakuta vitu vimeshaharibika? Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie barabara hii ya uchumi na iijenge kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara ya ulinzi ambayo ni muhimu sana kutokana na ulinzi na usalama wa watu wetu. Barabara hii nayo kwa muda mrefu ni mbovu, chafu na ninyi wenyewe mnatambua kwamba Jimbo langu limepakana na nchi jirani ya Msumbiji. Mnatambua hali iliyopo kule. Leo hii watu wetu wa ulinzi na usalama wanapata tabu na wanapata ajali kutokana na ubovu wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iangalie barabara hii kwa umuhimu wake, nayo ijengwe kwa kiwango cha

lami. Nimekuwa nikipiga kelele mara nyingi kwa ajili ya barabara hii, kwa hiyo, naiomba Serikali muiangalie barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye suala la afya. Jimbo langu la Mtwara Vijijini lina changamoto mno ya watumishi kwenye kada ya afya na elimu. Tunayo shida ya watumishi upande wa afya na walimu pia. Upande wa walimu kuna shule ina wanafunzi wengi, shule ya Msingi Kivava. Kwenye shule hiyo kwanza hakuna nyumba za walimu na ukiziona nyumba za walimu utalia. Walimu wanaishi katika mazingira magumu na pili, kuna walimu watatu tu. Naiomba sana Serikali ituletee walimu wa kutosha katika Jimbo langu la Mtwara Vijijini. Vilevile, tunaomba watuletee watumishi wa afya katika Jimbo langu la Mtwara Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ardhi, kwanza nampongeza Mheshimiwa Jerry Silaa kwa kazi kubwa anayoifanya katika Wizara hii. Juzi nilikuwa Jimboni kwangu Mtwara Vijijini, Kata ya Mahurunga Kijiji cha Kivava, kumetokea mafuriko makubwa sana na hii ni mara ya pili yanajirudia mafuriko haya. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi alichukue hili. Wananchi wangu wametoa maeneo, lakini inahitajika kulipwa fidia kwenye mashamba yao. Namwomba Mheshimiwa Jerry lichukue hili, twende ukalipe fidia kwa wananchi wale ili tuepukane na mafuriko haya kujirudia mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie upande wa asilimia kumi. Wananchi wangu wamekuwa wakiniuliza sana kuhusu suala hili la asilimia kumi, hawaelewi sintofahamu iliyokuwepo mpaka leo hii. Hatuelewi hili suala limefikia wapi? Hatuelewi mwendelezo wa suala hili ukoje kwa sababu wananchi wanataka kukopa, lakini mpaka leo hii wakienda kwenye Halmashauri zetu…

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mchangiaji anayechangia kwamba suala la asilimia 10 kukwama limewadumbukiza wanawake na vijana kwenye mikopo ya riba kubwa ambayo ni Kausha Damu. Wanawake na vijana wengi wamefilisiwa badala ya kuwainua, wameenda kuanguka. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia, endelea na mchango wako.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaipokea taarifa hii tena kwa mikono miwili. Ni kweli kwamba wananchi wetu wamekuwa na sitofahamu kuhusiana na mikopo hii ya asilimia 10. Kwa hiyo, tunataka kujua taratibu hizi za kutoa mikopo kwa ajili ya wananchi wetu wa asilimia kumi imefikia wapi? Mikopo hiyo itakapokuwa tayari isiangalie vyama. Kuna ubaguzi ambao unaendelea ndani ya mikopo hii, toeni mikopo kwa wananchi wote. Serikali hii, Rais na Mawaziri wote ni wa wananchi wote, kwa hiyo, msiangalie itikadi ya vyama katika kutoa mikopo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, nakushukuru sana kwa fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili nami nitoe mchango wa mawazo kuhusiana na bajeti ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi za dhati kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na

timu yake yote ambao wamewasilisha bajeti yao vizuri, bajeti ambayo imesheheni mambo mengi ambayo yanaenda kulisukuma Taifa hili katika maendeleo ya dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumshukuru Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kile ambacho amekifanya kwenye maendeleo ya kilimo kwa msimu ambao umeisha. Tulipitisha bajeti iliyopita ya 2023/2024, fedha ziliongezwa kwenye kilimo na tumeona mikakati mingi ambayo Serikali imeifanya ikiwemo ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na mengine mengi ambayo yataleta tija kwenye kilimo chetu, ukizingatia kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu. Kwa hiyo, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika pongezi hizo, nitoe mfano wa kile ambacho Serikali imekifanya. Kwa mfano, wakulima wa zao la korosho katika nchi yetu ya Tanzania, kwa msimu wa 2023/2024 Serikali ilijitahidi kutoa pembejeo bure kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji kama vile ambavyo iliahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo, tunashukuru sana kwamba kwa mfano kwenye zao hilo la korosho uzalishaji umeongezeka kidogo tofauti na msimu wa mwaka 2022/2023. Msimu huu wa mwaka 2023/2024 kutokana na kutolewa kwa pembejeo ambazo zilikuwa bure, ongezeko lipo. Tunaishukuru sana Serikali kwa sababu hali ya wananchi wetu katika mifuko ilikuwa ni ngumu na hivyo wasingeweza kupulizia. Wananchi wengi wanaolima korosho katika nchi hii wamenufaika na pembejeo zile, na zao la korosho uzalishaji angalau umeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mtwara, ukienda kwenye Chama Kikuu cha Ushirika cha Watu wa Tandahimba na Newala *(TANECU)* kwa msimu wa mwaka 2022/2023 uzalishaji ulikuwa ni tani 33,000 peke yake, lakini kwa msimu huu wa 2023/2024 zimeongezeka tani 33,000 na kufanya uzalishaji kuwa tani 74,000. Tunaishukuru sana Serikali kwa sababu hali hiyo isingefikiwa. Hicho ni

chama kimoja tu, ikija kuunganishwa kwa Tanzania nzima kwa zao la korosho, basi tutaona ongezeko litatofautiana sana na lile la msimu wa mwaka 2022/2023. Tunaishukuru Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ongezeko hilo, nashukuru pia kwenye hotuba ambayo tumeletewa iliyopo mbele yetu, ukienda aya ya 46 inasema: "Pamoja na mambo mengine Serikali itahakikisha kilimo kinakuwa na faida kwa kuhamasisha uongezaji wa thamani kwenye mazao na upatikanaji wa masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi." Tunashukuru sana kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee hapo. Pamoja na uzalishaji kuongezeka, hili ambalo Serikali imelisema la kutafuta thamani ya mazao pamoja na kutafuta masoko ndani na nje ya nchi, ndipo changamoto ilipo kwa wakulima wetu wengi; na mazao mengi yanakwama kwenye masoko. Ukienda kwa watu ambao wanazalisha mpunga, wanazalisha mpunga mwingi lakini unakuta wanakwama kwenye bei. Ukienda kwenye korosho, halikadhalika, uzalishaji ndio huo, lakini kwenye bei inakuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, msimu huu ambao umeisha, huu wa mwaka 2023/2024 changamoto ya bei imekuwa ni kubwa mno kwenye zao la korosho, bei iko chini. Pamoja na bei kuwa chini, kuna utitiri wa tozo ambazo zinamkumba mkulima wa korosho. Naiomba Serikali yangu tukufu ambayo inasikia, ijaribu kutafuta namna ya kupunguza tozo kwa sababu mkulima anachopata ni kidogo, lakini tozo zimekuwa nyingi kiasi kwamba sasa kile anachokipata pamoja na udogo wake chote kinaishia kwenye tozo. Kwa hiyo, kunakuwa na tofauti kubwa kati ya zile gharama za uzalishaji kuanzia palizi, upuliziaji mpaka kuja kuvuna na kile ambacho mkulima akienda kuuza anakuja kukipata kama *take home*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iangalie, ikae chini itafakari suala la tozo ili mkulima apate angalau kitu ambacho

kitamfariji, kwa sababu sasa hivi kwa kweli imekuwa ni chanagamoto kubwa. Hapo niseme tu, lawama kubwa tunaibeba sisi ambao ni wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo, Serikali iendelee kututafutia masoko na pia kuangalia hizi tozo kwani zimekuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye zao la korosho kunakatwa *Export Levy*. *Export Levy* ilivyokatwa, tunashukuru baadhi ya matunda tumeanza kuyaona ikiwemo na pembejeo. Basi naiomba Serikali ifanye kitu ambacho *Export Levy* itakuja kumnufaisha mkulima wakati anauza zao lake kwa sababu kwa kweli hali imekuwa siyo yenyewe. Hali hii ni kwa sababu sisi bado tunategemea kuuza korosho ghafi, hicho ndicho ambacho tunakwama nacho. Uuzaji wa korosho ghafi ndiyo unaotufikisha hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua jitihada za Serikali za kuweka mpango wa kutengeneza au kuanzisha *industrial park* ambayo itachakata korosho zote hapa ndani na hatimaye tuuze korosho ambazo siyo ghafi tena, lakini, hiyo ni *long term plan*. *Short term plan* lazima tuitafute. Masoko ya korosho yanatafutwa kipindi msimu tayari umeshatangazwa wa kuuza korosho. Kwa hiyo, inakuwa kama kuna uharaka fulani, matokeo yake tunaenda kuangukia kwa wanunuzi ambao wanatulalia kwenye bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sababu imeshaweka kwenye mikakati kutafuta masoko ya bidhaa zake za kilimo, basi ifanye mapema kabla ya msimu kutafuta wanunuzi. Kwa sababu, kama itafanyika mapema, ule uharaka haraka ambao mara nyingi hauna baraka utapotea na mkulima yule ataenda kunufaika na soko la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niongelee suala la maji. Nashukuru sana Serikali yetu inafanya jitihada kubwa sana kuhakikisha kwamba suala la maji linafikia hatua nzuri. Katika Sera yake ya Maji inasema ifikapo 2025, basi kwa wale ambao wanaishi

mijini wapate maji safi na salama kwa asilimia 95 na wale ambao wako vijijini wapate maji safi na salama kwa asilimia 85 ifikapo 2025. Katika kufikia hilo, tunaona juhudi ambazo Serikali imekuwa ikizifanya ili kuhakikisha kwamba maji safi na salama yanapatikana kwa wananchi wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu kulikuwa na mradi wa miji 28. Mradi ule ulisuasua sana, lakini bahati nzuri ukasainiwa mwaka juzi, 2022 na umeanza utekelezaji katika baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wananewala ni wanufaika wa huo mradi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kengele ya pili hiyo.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyamoga.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami mchana huu nichangie hoja iliyopo Mezani. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kutoa mawazo yangu mawili matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea miradi mingi kwenye majimbo yetu pamoja na Jimbo la Tunduru Kusini. Moja ya miradi ambayo inaleta faraja kwa watu wa Jimbo la Tunduru Kusini ni miradi ya afya, elimu, maji pamoja na

barabara. Jimbo la Tunduru Kusini lilibahatika kupata vituo vya afya vitatu na zahanati nane. Vituo vya afya viwili vimekamilika lakini hamna watumishi mpaka hivi leo, na hata vifaatiba bado havijaweza kupatikana. Kati ya zahanati nane, zahanati tatu bado hazina watumishi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nianzie hapo kwa sababu Bunge lililopita 2021 Waheshimiwa Wabunge tuliongelea sana suala la ajira ya watumishi wa afya na walimu. Hiyo imekuwa ni changamoto kwa upande wa mikoa na majimbo yaliyopo pembezoni mwa nchi. Tunapoajiri wafanyakazi kutoka maeneo mbalimbali kwenda kwenye majimbo yetu hasa ambayo siyo asili ya maeneo yale, matokeo yake baada ya mwaka mmoja watumishi wote wanakuwa wanahama, wanarudi huko walipotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mwaka wa fedha uliopita pekee yake, Jimbo la Tunduru Kusini na Halmashauri ya Tunduru wamehama wafanyakazi wa afya 57 na kuacha zahanati nyingi zikiwa na mtumishi mmoja mmoja au wawili na nyingine hazina watumishi kabisa, kwa sababu ya wafanyakazi wote walioajiriwa kwa mwaka 2021 wamepata uhamisho kurudi mahali ambapo wametokea. Mara nyingi inatokea hasa kwa watumishi wa kike, wengi wameajiriwa wakiwa hawajaolewa, lakini baada ya mwaka mmoja wote wanaleta vyeti vya kuolewa na wanaondoka katika maeneo yetu na kuacha wananchi wetu bila huduma yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni ule ule niliotumia mwaka 2021, tunaomba Serikali iangalie, wakati wanaajiri watumishi hawa, basi waangalie mazingira wanayowapeleka yafanane na yale waliyotoka ili angalau kila jimbo au kila halmashauri ipate watumishi; walimu na watumishi wapya kutoka maeneo yao ili waendelee kukaa katika maeneo yetu, kwa sababu inaonekana sasa imekuwa ni kama mradi, wanachukua ajira kupitia maeneo yetu na baadaye wanafanya mipango, wanarudi kwenye maeneo ambayo wametokea. Hili jambo kwa kweli kwenye maeneo yetu ya

upande wa kusini imekuwa ni changamoto kubwa. Ninaomba Serikali waliangalie, wakati wanatoa ajira hizi, basi waangalie watu wanaotoka maeneo ambayo yanafanana ili waendelee kukaa na kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda niongelee ni suala la barabara. Barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi – Tunduru imekuwa ni kilio chetu cha muda mrefu. Tayari barabara hii imeshafanyiwa upembuzi yakinifu tangu mwaka 2020, lakini kila mara, hata asubuhi mwenzangu, Mbunge wa Namtumbo ambaye ana kilometa 200 kwenye barabara hii, nami nina kilometa 100, amelizungumza na kuulizia. Barabara hii iko kwenye Ilani ya Uchaguzi. Upembuzi yakinifu tayari, lakini mpaka leo dalili za kuwa barabara hii inatengenezwa kwa kiwango cha lami, bado hazionekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu hasa kwa upande wa ulinzi. Jimbo letu la Tunduru Kusini pamoja Namtumbo limepakana na Msumbiji, hali ni mbaya upande wa pili, na askari wetu wanaitumia sana barabara hii kwa ajili ya kufanya *patrol* na kulinda nchi yetu ili tusiathirike na wale waasi wanaotoka upande wa pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaikumbusha Serikali, kwa sababu ya umuhimu wa barabara hii ya ulinzi na uchumi wa Wilaya hizi mbili; Tunduru na Namtumbo, wanategemea katika maeneo haya, basi ni vyema sana Serikali ifanye hima watusaidie kupata kipande cha lami ili barabara ile iweze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nilizungumze, ni kwamba Mkoa wa Ruvuma tumepata neema kubwa ya kuwa na makaa ya mawe maeneo ya Ngaka pamoja na Wilaya ya Mbinga na Songea Vijijini. Neema hii imekuwa ni kubwa, na magari yamekuwa ni mengi. Tumekuwa na mpango wa muda mrefu wa kujenga reli ya kusini, lakini kila mwaka tunavyokuja

kwenye bajeti hatuoni dalili zozote za kuwa na mpango wa kujenga reli hii. Tumekuwa tunazungumza, na mara nyingi wanasema kuhusu *PPP*, lakini reli hii itakuwa ni mkombozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu barabara ya kutoka Songea kwenda Mbinga, Songea kwenda Makambako, Songea – Tunduru – Masasi mpaka Mtwara, kwa sababu siyo chini ya malori 2,000 kwa siku yanapita kwenye barabara hizi, matokeo yake barabara zinachimbika. Dawa pekee ya kuhakikisha barabara hizi zinaendelea kudumu ni ujenzi wa reli ya kusini ambapo upembuzi yakinifu ulishafanyika kwa muda mrefu. Ni reli ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa. Makaa ya mawe huwezi kusafirisha kwa ndege, yakisafirishwa kwa treni itakuwa ni bora zaidi na itaongeza uchumi kwenye kanda zetu za kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hili jambo pamoja na kwamba bajeti zetu hazisemi, mara kwa mara tunaendelea kutafuta wahisani. Naomba sana, Reli ya Kusini ni muhimu ili barabara zetu ziweze kupona kwa ajili ya mizigo mikubwa ambayo inasafirishwa na malori yale. Pamoja na barabara hiyo kuwa hivyo, barabara ya Songea kwenda Njombe, nayo mwaka jana, 2023 bajeti iliyopita walisema wataanza kujenga kilometa 100, lakini mpaka leo ile barabara bado haijaanza kufanyiwa chochote. Barabara ile sasa hivi ni mbaya kwa wanaopita na magari madogo, kwa kweli naiona adha ile ambayo wanaipitia. Barabara ile ina mashimo mengi sana kutokana na hayo malori ambayo tumeyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa sana nilizungumzie ni mgao wa maeneo. Majibu ya Serikali tunayasikia, lakini kuna maeneo hatutendi haki kwa sababu ya ukubwa wa maeneo yaliyokuwepo. Halmashauri ya Tunduru ni miongoni mwa halmashauri ambazo eneo lake ni kubwa ukilinganisha na wilaya nyingine. Wilaya yetu ina *kilometer square* zaidi ya 18,776, hata watumishi waliopo maeneo haya kuhudumia, Mkuu wa Wilaya imemhitaji atumie zaidi ya mwaka mmoja ili angalau apitie kila kijiji kwenda kufanya mikutano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba, pamoja na dhamira nzuri ya Serikali kuendelea kuhudumia halmashauri ambazo hazina huduma, tunaomba mgao wa wilaya hii. Ni muhimu sana. Kwa sababu, eneo letu ni kubwa sana ambapo inakuwa ni ngumu kwa watumishi wetu kuhudumia hili eneo. Halmashauri tuna kata 35, kata moja ina watu zaidi 24,000 zingine zina watu zaidi ya 18,000, ni kwa sababu ya wingi wa watu na ukubwa wa eneo. Kwa kweli, tunaomba mtusaidie tupate eneo la utawala, halmashauri inahitajika nyingine ili tuweze kuwahudumia watu wetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa napenda sana niliongee ni suala la tembo au ndovu. Ndovu kwenye Wilaya ya Tunduru ni kilio kikubwa sana. Mkutano wa Bunge uliopita tulipewa bajeti hapa kwa ajili ya askari wa kufukuza tembo. Tunashukuru tumepata askari wasiopungua wanane, lakini hawatoshi. Sasa hivi ndiyo kipindi cha tembo, na kwenye maeneo yetu wameshaanza kuleta madhara. Watu wawili wameshakufa mpaka sasa. Kwa mwezi wa Pili mwishoni tayari tumeshazika kwa sababu ya majanga ya tembo, lakini bado tayari wameshaanza kushambulia mazao ya wakulima kwenye mashamba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana jambo la kifuta jasho cha wakulima kwa ajili ya tembo kuharibu mazao yao tukigeuze, badala ya kuwa kifuta jasho, yawe ni majanga. Kwa sababu, mkulima amelima heka mbili au heka tatu, asubuhi ameenda tembo amekula mahindi kwenye shamba lote. Hili ni janga. Huyu mtu atakula nini asubuhi? Kesho atakula nini? Kwa sababu shamba lake lote limeliwa na tembo. Tuweke katika maeneo ya majanga ili mkulima badala ya kusema apewe kifuta jasho, Hapana, liwe janga. Serikali iwafidie wakulima ili waweze kuishi vizuri, kwa sababu tusipofanya hivyo, kila mwaka kilio cha tembo kimekuwa ni kitu cha kawaida. Serikali imeshindwa kudhibiti tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa, kwa sababu tumeshindwa kuwafanya hao tembo wasiharibu mazao ya wakulima, basi hiyo iwe ni sehemu ya majanga ili inapotokea

uharibifu, basi wakulima walipwe fidia na Serikali, badala ya kulipwa kifuta jasho, kwa sababu lile ni janga, ni jambo ambalo hawakukusudia. Mtu ameamka asubuhi, amekuta shamba lake limeliwa na tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati huu tunapoendelea na zoezi hilo, basi tunaomba tuongezewe askari. Sasa hivi ndiyo wakati mgumu sana kwetu sisi wakulima wa Tunduru kwa sababu tembo ndiyo wanatoka. Sasa wale wanaotoka Msumbiji wanakuja Tanzania pamoja na kujaa mto, lakini wanaogelea, wanakuja Tanzania kwa ajili ya malisho. Wanajua tayari Tunduru ina mazao yameshakuwa tayari, wanakuja kuyatumia kama chakula chao na hao tembo wa *Selous* ndiyo nao wanataka kutoka *Selous,* wanapita mbuga zetu za hifadhi za wananchi, wanarudi Tunduru. Kuna maeneo ambayo mpaka jana na juzi nimeongea na Mheshimiwa Naibu Waziri... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyamoga, jiandae Mheshimiwa Mkundi, Mheshimiwa Mkundi hayupo. Mheshimiwa Shabiby.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo.

**NAIBU SPIKA:** *Okay*.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na nafasi hii niliyoipata ya kuweza kuchangia hoja hii. Pili, kwa niaba ya wananchi wa Kilolo namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya ya miradi mingi ambayo inatekelezwa katika Jimbo la Kilolo. Miradi ni mingi, siwezi kuitaja yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi, barabara ya kutoka Iringa Mjini hadi Kilolo kwa sasa inajengwa, mkandarasi yupo *site* na tunashukuru sana. Pamoja na Barabara, pia ipo miradi mingine mingi sana ambayo yote kwa ujumla wake tunaishukuru Serikali kwa kazi nzuri inayofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, napenda kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa utekelezaji wa mambo mengi. Tunaona kazi zao, na kwa kweli tunawapongeza. Nawapongeza Mawaziri wote na Waziri *Senior,* dada yangu Mheshimiwa Jenista kwa kazi nzuri na Manaibu wake tunampongeza na tunamshukuru kwa kazi nzuri sana ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuzungumza mambo mawili muhimu ambayo nadhani yanaweza kusaidia ustawi wa Taifa letu na pia kwa maeneo yetu. Jambo la kwanza ambalo napenda kuzungumzia ni suala zima la upelekaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa *TARURA* na kwa *TANROADS*. Kwenye miaka ya nyuma tulikuwa na utaratibu mzuri ambapo barabara hizi zinatangazwa mapema, ikifika mwezi Januari au mwezi wa Pili, basi barabara zinatangazwa. Hii ilitokana na kwamba maeneo yenye mvua kama Jimbo la Kilolo, Mufindi na maeneo mengine, barabara zinatakiwa zianze kutengeneza mwezi wa Saba halafu ikifika mwezi wa Kumi mvua zinaanza. Kwa hiyo, tutakuwa tumekamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana, 2023 jambo hili halikufanyika kwa sababu kulikuwa na kitu kinaitwa *NEST,* ambao ni mfumo wa manunuzi, ulikuwa unabadilishwa. Kwa hiyo, ukavuruga utaratibu wote na barabara hazikutangazwa mapema. Kilichotokea ndicho hiki tunachokiona sasa, barabara nyingi zimeharibika kwa sababu hazikutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, mwaka huu Serikali ijiridhishe kama barabara zimekwisha kutangazwa tayari kwa

ajili ya kuanza kujengwa mwezi wa Saba kama ambavyo tumekuwa tukifanya miaka mingine. Hii imesababisha barabara nyingi sana kuharibika. Nikitoa tu mfano kwenye jimbo langu, barabara karibu zote, nyingi zimeharibika. Barabara ambayo nimeitaja hata asubuhi ya kutoka Idete – Kidabaga – Kilolo haipitiki, imefungwa. Barabara ya kutoka eneo la Ukwega, kata nzima imejifunga na haipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna baadhi ya maeneo ya Kata ya Ukumbi, barabara zote zimejifunga. Ukitaka kupita kutoka Kilolo kwenda Pomerini kwenda Mwatasi, zote zimejifunga. Sasa hii imetokana na kuchewelesha kutangaza, halafu wakandarasi wapo, lakini hawawezi kupeleka vifaa kwa sababu mvua zinanyesha. Jambo hili naomba sana, muda wowote ambapo mtalijadili, fedha za barabara zipelekwe mapema, na kibali cha kuzitangaza kitolewe sasa hivi ili wakati tutakapomaliza kupitisha bajeti, ile asilimia inayotakiwa kwenda mapema, iende na barabara zijengwe mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, izingatiwe kwamba haya ni maeneo yenye mvua na kwa hiyo, yanahitaji fedha mapema ili kuhakikisha kwamba tunakidhi yale tuliyojiwekea na ili kuondoa kero, kwa sababu barabara ni kero kubwa na ndiyo inayozuia uchumi kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano ipo mingi kwa Uchumi, kwa mfano uchumi wa misitu, badala ya kuuza mti kwa shilingi 15,000/= hadi shilingi 20,000/=, barabara ikiwa mbovu mwananchi anauza kwa shilingi 2,500/= ili mtu aweze kuvuna, achane mbao na hii inamrudisha nyuma sana kimaendeleo. Kwa hiyo, tunapoomba sana, kwamba hata hiyo fedha kidogo iliyopo ipelekwe mapema, tunataka uchumi wa haya maeneo uweze kukua na wananchi waweze kufaidi, na vile vile kuondoa kero nyingi ambazo sasa hivi tunazipata kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo napenda kulizungumzia na ambalo nadhani hatujali-*exploit* vizuri na labda Mheshimiwa Waziri wa Mipango anaweza akalichukua na kuliangalia ni kuhusu biashara ya *carbon*. Sasa maeneo mengi ya Tanzania ina misitu takribani hekta milioni 48. Nataka nitoe mfano mmoja tu wa Wilaya ya Tanganyika, vijiji vinane mwaka 2023 vimepata shilingi bilioni nane. Halmashauri nyingi zinapata shilingi bilioni mbili, shilingi bilioni tatu. Vijiji vinane kwa kufanya biashara ya *carbon* vimepata shilingi bilioni nane. Mwaka huu wanatarajia shilingi bilioni 14 kwa vijiji vinane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi kikubwa cha misitu Tanzania ikiwemo misitu ya Kilolo haivunwi *carbon* wala hatuuzi *carbon* ambayo ingeweza kuipunguzia Serikali gharama kubwa ya kupeleka fedha kwenye halmashauri. Tatizo lipo kwanza kwenye utaalamu kwa sababu tunahitaji wataalamu. Pale TAMISEMI amewekwa mtu mmoja kwa ajili ya biashara ya *carbon,* na huyo mtu mmoja mwenyewe utaalamu wake ni wa kujifanyia juhudi yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa kunafanyika makongamano ya biashara ya *carbon,* lakini hawapelekwi wataalamu wowote halafu hata hizo shilingi bilioni nane au shilingi bilioni 14 tunazozipata zinatokana na mtu kati, yaani yule mnunuzi ni wa sita kutoka kwetu sisi, ndiyo tunapata shilingi bilioni 14. Hebu fikiria, ninyi mnafahamu biashara ya watu kati, kama sisi ni wa sita, je kama sisi wenyewe tungeuza tungepata shilingi ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nchi ingeweza kuwa na uchumi mkubwa sana kama Serikali ingetenga kitengo maalamu pale kwenye Wizara ya Mazingira ambapo hawa watu wanaofanya biashara ya *carbon* wangewekwa, lakini kakiangalie kile kitengo kina watu wangapi? Kuna wataalamu wangapi wa nchi hii wanaoweza kujadili biashara ya *carbon,* na wanaoweza kuwatafuta wanunuzi halisi wa biashara ya *carbon,* wakakaa waka-*negotiate*?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi jirani zina wanunuzi, na wanunuzi wanafahamika. Mnaenda kwenye makongamano, wanaonekana, halafu wewe unatumia mtu kati wa sita wakati wewe mwenyewe kwenye makongamano unaenda na unawaona na wanajitambulisha, mimi ndiyo mnunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi huku, tunawauliza, wale watu wa Tanganyika wamekuja wanasema sisi wanunuzi hatuwajui, tunatumia madalali. Kwa nini nchi isiwe na wataalamu wa kuwatafuta watu halisi wa biashara hiyo ya *carbon,* sisi wenyewe tukajadiliana nao? Mbona kuna nchi jirani wanafanya biashara ya moja kwa moja! Sasa si twende tukajifunze wao wamewapataje? Kwa kuwa wanajulikana, kwa nini hatuoni umuhimu wa kuwekeza kwenye biashara ya *carbon?* Hii misitu tunayoitunza ni ya nini kama hatuwezi kufanya biashara? Biashara hizi zina msimu, itaenda baada ya muda itaisha, tutakuwa hatuja-*exploit* hela yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mipango ituambie, hivi kuna kizuizi gani cha ku-*exploit* hiyo *opportunity* ambayo kwa sasa duniani kote wanaizungumzia? Changamoto yake ni nini? Nami nazungumza hivi wa sababu misitu ya Serikali za vijiji peke yake tu, kwa Kilolo ni zaidi ya hekta 54,000, lakini misitu ambayo Kilolo inayo ambayo sasa ingeweza kuingizwa kwenye soko ni zaidi ya hekta 170,000. Hiyo ingeweza kuingiza fedha ambayo ni mara 15 ya hela ambayo wanakusanya. Mama Ntilie wanafukuzwa, sijui watu gani, tusingekuwa na haja ya kuhangaika na hizi hela ndogo na fursa ipo. *Opportunity* ipo, mifano ya halmashauri zinazopata tunayo, lakini tumekaa tunaangalia fedha kidogo tulizonazo. Kwa nini tusitumie *brain* tuliyonayo Mungu aliyotuijalia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao wataalamu wazuri sana katika hii nchi, kwa nini kisiundwe kikosi kazi kizuri cha wataalamu kitufanyie tathmini? Tunawezaje kunufaika na biashara ya *carbon* kabla haijaisha, kabla hili soko halijaondoka? Natamani wakati wa majumuisho tupate majibu mazuri ya kuelewa hiki kitu kitafanyika lini kwa sababu nina uhakika kina maslahi mapana kwa Taifa letu, lakini

nina uhakika kingewapunguzia mzigo mkubwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi hadithi za wafanyakazi wachache, wataalamu wasiokuwepo, na wale waliokuwepo wasipokuwa na *commitment* kwenda kwenye makongamano na kuzunguka kwenye *shopping mall* na kurudi hapa wamenunua vitu vichache, tusingependa jambo hilo liendelee. Tunatamani kuona biashara ya *carbon* inafanikiwa kwenye nchi yetu na sisi tunapata manufaa kama nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujifunze kutoka kwenye nchi nyingine kwa sababu biashara ya *carbon* ni uchumi. Sisi tunaotoka kwenye maeneo ya misitu tunajua tungeweza kunufaika kwa namna kubwa. Kwa kweli hili ni jambo ambalo ningependa lifanyiwe kazi na tuone jinsi gani tunavyoweza kunufaika na biashara ya *carbon*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nilitaka nichangie ili nione kama pia leo hamtasikiliza, maana ni mara yangu ya nne kuzungumzia biashara ya *carbon,* basi nitajua hamtaki wala hamtaki hizo fedha, wala hamtaki ku-*exploit* hiyo *carbon*. Machoni kwa Watanzania, ninanawa mikono, tumeshaipigia kelele, sasa ni kazi kwa Serikali, kama wataiacha, waiche, lakini sisi tumezungumza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, umechangia vizuri sana, *big up*. Tunakwenda kwa Mheshimiwa Shabiby; naona atachangia kesho. Sasa namwita Mheshimiwa Mkundi, atafuatiwa Mheshimiwa Raymond. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Natumia nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia

Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kutuletea maendeleo kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imesheheni mambo mengi na kuonesha dira ya Taifa letu na namna gani mambo mbalimbali ikiwemo miradi ya maendeleo namna ilivyotekelezwa. Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote kwenye Wizara hii na watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua Mheshimiwa Jenista na wasaidizi wake namna gani wanafanya kazi kubwa, na Ukerewe ni moja kati ya maeneo yaliyonufaika na miradi mikubwa ya maendeleo ambayo Mheshimiwa Rais ameweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa kwenye maeneo kama mawili na muda ukiruhusu basi nitaongeza eneo la tatu. La kwanza, ni eneo la kilimo. Tanzania tumebahatika kuwa na eneo kubwa lenye sifa ya kuweza kutumika kwa ajili ya uzalishaji wa mazao mbalimbali. Kwa kuangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuanzia aya ya 46, inaonesha namna gani kupitia mradi wa *ASDP II* ulivyotunufaisha ingawa pamoja na mafanikio tuliyoyapata kwa sababu kwa mujibu wa hotuba mpaka sasa tumefanikiwa kwa asilimia 66 na mradi wenyewe unaenda mpaka mwaka 2027/2028.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kupitia Sekta ya Kilimo tunaweza tukafanya mambo makubwa sana kupitia hii *ASDP II,* tunaweza tukafanya vizuri sana na tukitumia maeneo tuliyonayo yenye rutuba na uwezo wa kuzalisha mazao, tukawa na uchumi mkubwa na endelevu kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna maeneo mengi hatujaweza kuyafanyia kazi pamoja na dhamira ya Serikali kuweza kuongeza uzalishaji kwenye maeneo yetu mpaka kufikia hekta zaidi

ya 1,200,000, lakini bado kuna maeneo mengi na hasa rasilimali maji hatujaweza kuitumia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua jitihada za Serikali kutengeneza mabwawa na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, lakini bado hatujaweza kufanya vizuri. Nikitoa mfano, mimi natoka Jimbo la Ukerewe ambapo tumezungukwa na maji. Katika eneo tulilonalo, zaidi ya kilometa 6,400, asilimia 90 ni maji. Inasikitisha kwamba pamoja na eneo tulilonalo ambalo tuna hekta karibu 31,000, lakini kwa sababu hatufanyi kilimo cha kisasa ambacho kinaweza kuleta tija kila mwaka katika maeneo tuliyonayo, tunaona mahitaji ya chakula ni tani 151,000, lakini uwezo wa kuzalisha chakula ni tani 104,000 pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake, pamoja na kwamba kitaifa tuna ziada ya chakula karibu tani 400,000 lakini bado Ukerewe kila mwaka tunakuwa na upungufu wa chakula karibu tani 40,000. Naomba kwamba, pamoja na jitihada kubwa ambazo zinafanyika kwenye kuimarisha kilimo, maeneo yenye rasilimali kama Ukerewe ambayo ina rasilimali maji, basi itumike kwa ufanisi ili angalau tuweze kuzalisha chakula kwa wingi na eneo husika vile vile liweze kujikidhi kwa mahitaji yake ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwenye eneo lililo na maji kwa kiasi kile kila mwaka kuendelea kuwa na upungufu wa chakula, kuwa na shida ya usambazaji wa maji safi na salama. Wakati Wakerewe wanaona wamezungukwa na maji, ukiwaambia tuna shida ya maji, watu hawawezi kuelewa. Kwa hiyo, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla wake ione namna, na haja ya kutumia rasilimali tulizonazo kwa ajili ya uzalishaji na kuondokana na changamoto zinazotukabili kama nilivyotoa mfano kwenye eneo la Ukerewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji kwenye Sekta ya Uvuvi. Ni kweli siku chache zilizopita katika uwekezaji uliofanyika wa zaidi ya shilingi bilioni 13 kwenye

kununua boti, lakini na ufugaji kwa kutumia njia ya vizimba, sisi Ukerewe ni wanufaika wa mradi ule. Nashauri kwamba, pamoja na jitihada zote hizi, kama ilivyofanyika kwenye eneo la kilimo kuanzisha *BBT,* lifanyike *BBT* vilevile kwenye eneo la uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri hivi kwa sababu Ukerewe tuna visiwa karibu 38 na vyote vinafanya shughuli za uvuvi, kwa hiyo, kinaweza kutengwa hata kisiwa kimoja kikatumika kama eneo la kutengeneza mradi wa *BBT* ili tuone matokeo yake yanakuwaje, kwa sababu zaidi ya asilimia 90 ya wakazi wa Ukerewe wanategemea Sekta ya Uvuvi. Kupitia *BBT* sasa inaweza kuwa njia ya kuonesha wananchi wa Ukerewe namna gani uvuvi kwa kutumia vifaa vya kisasa unaweza kuwatoa kwenye shida waliyonayo na kuweza kupata mafanikio ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nilitamani kuchangia ni eneo la nishati. Kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aya ya 73 mpaka 75, amelezea namna gani tulivyo na changamoto kwenye eneo la nishati, lakini nafarijika kwa sababu Serikali imeonesha jitihada zinazofanyika kuimarisha Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mpaka sasa kama Taifa tuna umeme kidogo, tunazalisha *Megawatt* chache pamoja na kwamba kupitia Bwawa la Mwalimu Nyerere tunategemea zaidi ya *Megawatt* 2,000 kuongezeka kwenye *Grid* ya Taifa, lakini bado tunahitaji kuzalisha zaidi nishati ya umeme, kwa sababu umeme kama nishati, ni kichocheo cha maendeleo ya eneo lolote lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Ukerewe ni kweli kwamba karibu vijiji vyote vimefikiwa na nishati ya umeme, lakini bado maeneo ya visiwa yana changamoto kubwa. Natambua jitihada za Wizara kuweka mradi wa kutoa umeme kwenye kisiwa kikubwa cha Ukerewe kwenda kwenye visiwa, kwa mfano kama Ukara, lakini bado kuna changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, pamoja na jitihada inazozifanya, bado kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba vitongoji vyote vinapatiwa nishati hii ya umeme ili wananchi sasa waweze kutumia nishati hii kujiletea maendeleo kupitia uanzishaji wa shughuli mbalimbli za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, natambua harakati zinazoendelea kufanya Bwawa la Mwalimu Nyerere lianze kutoa uzalishaji katika uwezo wake wa juu, lakini pamoja na jitihada zinazofanyika, kuna changamoto ninayoiona katika miaka michache ijayo inaweza kukwamisha jitihada zote hizi. Tumewekeza pesa nyingi sana kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini tunatambua vyanzo vya maji yanayoenda Bwawa la Mwalimu Nyerere ni kuanzia Morogoro, Iringa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kosa moja linalofanyika, tumeruhusu mifugo mingi sana kuwepo kwenye eneo la Morogoro, jambo ambalo miaka michache ijayo itaathiri mazingira kwenye eneo lile na vyanzo vya maji vinavyotiririsha maji kuelekea kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere kuathirika. Sasa matokeo yake ni kwamba jitihada na rasilimali kubwa zinazowekezwa na Taifa hazitakuwa na tija kwenye miaka michache ijayo, jambo ambalo itakuwa ni hasara na tutakuwa hatujawatendea haki wananchi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ichukue hatua madhubuti kudhibiti uwepo wa mifugo mingi sana kwenye eneo la Morogoro ili sasa maji na vyanzo vya maji vinavyotiririsha maji kuelekea kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere visiathirike na kufanya rasilimali nyingi na pesa nyingi tunazozitumia kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere zisiwe na faida tena hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua tuna changamoto kubwa ya miundombinu kutokana na mvua kubwa zilizonyesha. Eneo la Ukerewe ni moja kati ya maeneo yaliyoathirika sana kwenye miundombinu yake. Barabara nyingi zimeathirika kutokana na mvua kubwa iliyonyesha. Natambua kwamba Serikali iliahidi kutenga pesa

kwenye kila jimbo ili kuweza kurekebisha miundombinu hii. Naomba sasa vile vile Ukerewe iangaliwe kwenye eneo hili, kwani barabara zetu zimeathirika sana. Kwa hiyo, Serikali iangalie namna ya kutusaidia pesa ili barabara zinazotengenezwa kwenye maeneo haya ziweze kuwa imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba Serikali tayari imepata mkandarasi kwa ajili ya barabara ya kutoka Kisorya kuja Nansio, ninashukuru, lakini bado kuna umuhimu wa kuimarisha barabara ya kutoka Nansio kuelekea Ilangala ambako ndiko lango la uchumi wa Ukerewe liko, ambako kuna uzalishaji mkubwa wa samaki. Naomba Serikali ione umuhimu wa kutengeneza barabara hii ili wananchi wa Ukerewe waweze kunufaika na rasilimali zinazozalishwa kwenye eneo hili, hasa mazao ya uvuvi. Natambua kazi kubwa wanaifanya, lakini naomba sana hili jambo liweze kutiliwa nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni juu ya ugawaji wa majimbo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili, Mheshimiwa Mkundi, ahsante. Mheshimiwa Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Nashon William Bidya.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya mchana huu kuweza kutoa mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2023/2024 na Mwelekeo wake wa Mwaka 2024/2025 katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa afya njema, amani tuliyonayo katika nchi yetu. Kipekee kabisa namshukuru Mungu kwa kutupa Rais wetu mahiri kabisa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anayesimamia Ilani ya CCM kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitazungumzia mambo mawili tu. Kati ya yote aliyozungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu, niseme naunga mkono hoja yake, lakini nataka tu ufafanuzi na labda niseme nataka utekelezaji katika maeneo mawili. Maeneo hayo ni eneo la mifugo na eneo la pili ni la nishati safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi nimekuwa nasimama hapa Bungeni kwa kipindi chote nilichokuwepo nikizungumzia mifugo. Niseme kwamba wafugaji wapo wa aina mbili; wale wanaofuga kwa kuswaga ng'ombe na wale wanaofuga kwenye *zero grazing.* Wafugaji wote hao wanatamani kuchangia pato la Taifa, nami mwenyewe natamani kuona kwamba mifugo inachangia pato la Taifa katika mapana yake kama ilivyo kwa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo na mifugo ni mapacha, haviwezi kutenganishwa. Ukiwa na mifugo mizuri itakupa mbolea, kilimo kitaboreka. Ukiwa na kilimo kizuri, pia mifugo itapata malisho na wananchi wote watakula na kuwa na Taifa lenye wananchi wenye afya nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizungumzia hapa mifugo, wanasema mifugo na uvuvi, tumeona kasi katika eneo la uvuvi ni kubwa sana na mpaka sasa hivi ikielezewa kama ingekuwa ni kupima kwenye mizani, tunaona kwamba kwenye uvuvi kumeenda kasi na kunazalisha zaidi ya mifugo. Tatizo liko wapi? Tumeona katika ripoti ya Waziri Mkuu ametueleza kwamba kwa kipindi chote cha mwaka mmoja imenenepeshwa mifugo 2,176, hao ndiyo ng'ombe walionenepeshwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina watu milioni 62, Tanzania ni kubwa, na Tanzania ina tija iwapo kila mmoja atawezeshwa katika hali nzuri ya mifugo. Sasa najiuliza tatizo liko wapi?

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo haijapewa uzito. Ukiwa na mifugo mizuri, siyo siri, utapata ngozi nzuri, utapata samadi ya kutosha, utapata maziwa kwa afya ya watoto na watu wazima, na pia utapata nyama ambayo itauzwa ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali hii makini na sikivu ni kutoa nafasi na uwezo kwa wananchi wengi kufuga wakiwemo wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro. Siyo rahisi kuizungumzia Tanzania nzima kwa mapana yake, ila nina hakika kila mfugaji angependa kuchangia katika pato la Taifa, lakini wale wa Kilimanjaro wako wanaongoja kuboreshewa mitamba mizuri ili wafuge, wapate mazao niliyoyataja awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo mifugo hii ambayo inanenepeshwa, ingenenepeshwa kwa ushindani kihalmashauri. Halmashauri zetu ziko 184, ukigawa kwa hii mifugo, tuseme kila halmashauri imenenepesha ng'ombe 10 tu kwa mwaka mzima, sasa hiyo ni nini? Yaani hainiingii akilini kabisa kwamba tumefanya kadri tunavyoweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara ya Mifugo na Uvuvi iweze kupanua uwezo wake wa kuelimisha wananchi katika kunenepesha hiyo mifugo na pia katika kuzalisha maziwa kwa wingi zaidi ili Sekta ya Mifugo iweze kuchangia pato la Taifa kwa ukubwa wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vijana wanaomaliza shule wanakuwa *idle,* wapo tu. Wao wanaona kasi ya Mheshimiwa Rais;

barabara zinajengwa, hospitali zinajengwa, miundombinu ya maji iko vizuri, miradi ya kimkakati inaenda vizuri, na hiyo wanakwambia imeshafanyika, imeenda hiyo. Nami nakubaliana nao. Hata katika *management,* Maslow alisema, *"once a need is satisfied, is no longer motivation." (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kwenye *another need,* ndiyo maana kila mwaka tutakaa hapa tunazungumzia ubora na uendelevu wa bajeti yetu na hakuna siku ambayo tutakaa tuishiwe namna ya kuishawishi Serikali ifanye zaidi na zaidi. Naungana na wote wanaompongeza Mheshimiwa Rais, lakini namwomba atupie jicho pia kwa wale ambao wamekaa katika majimbo yao, au kwa wananchi wetu wanaosubiri wawezeshwe ili waende na hiyo kasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nimesema kuna vijana ambao ni wahitimu, kuna wanawake ambao wana afya zao nzuri sana, pia kuna ambao walikuwa wanafanya kazi na sasa ni wastaafu, wana chochote walicholipwa, lakini hawawezi kwenda na kasi kwa sababu wanangoja Serikali nayo iwawezeshe kiasi fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena lile ombi na nitalirudia mpaka nimalize Bunge hili la Serikali kutupa mitamba ambayo inastahili kufugwa katika nchi hii. Wazee wetu walianza, Kenya, Uganda na Tanzania. Uganda ina mitamba mizuri sana na inauza maziwa mpaka Tanzania. Kenya ina mitamba mizuri sana na inauza maziwa mpaka Tanzania. Sisi hatuuzi popote zaidi ya hapa hapa. Tuna nini? Tatizo liko wapi? Naiomba Serikali iangalie jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wa Kilimanjaro wako tayari kufuga, wako tayari kunenepesha, lakini pia kama nilivyosema awali, tunaomba tuweke ushindani katika halmashauri ili kila mmoja aweze kuifaidi *cake* ya Taifa aliyoichangia. Tusije kunyang'anyana hapa tu, tunamkemea Waziri wa Fedha ambaye pia hatuchangii sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka nitoe shukrani za dhati sana kwa Mheshimiwa Rais kwa hii ajenda ya kuboresha nishati safi na salama kwa sababu wanawake wengi waliugua vifua kwa kukoka moto na sasa tunakwenda kujikomboa. Naomba tuendelee kuongea na wadau, naye mwenyewe aendelee kutusemea zaidi anakojua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru sana mdau mmojawapo anayeitwa *Oryx*. Imeweza kugawa mitungi mingi na kuweza kufikia eneo kubwa wakiwepo viongozi wa dini, wananchi walio kwenye wilaya au kata ambazo ziko pembezoni na sasa kila mtu anapika chai ambayo hainuki moshi. Tunaomba *Oryx* isiishie hapo, bado Tanzania inataka kuona kwamba nishati safi na salama ndiyo agenda ya Tanzania. Tunataka kunywa chai inayonukia mdalasini au karafuu na siyo chai inayonukia moshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Wizara ya nishati, pamoja na nishati bora zilizoboreshwa za aina zote ukiwemo umeme, majiko sanifu na mengineyo mengi, zile gesi za kilo sita ziendelee kugawiwa kila kukicha ili watu waweze kuona manufaa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba elimu. Siko tayari kusikia kwamba nyumba imelipuka na gesi ya *Oryx,* hapana. Waitwe kwenye mikutano waje wasikilize, wafundishwe namna ya kutumia gesi, wafundishwe namna ya kujikinga na gesi ikilipuka na kadhalika. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, itakapokuja semina ya *Oryx,* wote mhudhurie. Nitaileta ili mweze kupata mafunzo na pia mweze kujua namna ya kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, jambo lile ambalo lilikuwa limeombwa siku nyingi la kuunganisha ile mifuko yote ili sasa iende kule kwenye Wizara mojawapo iweze kuwafikia vijana, lifanyike katika *speed* ya juu zaidi. Nasema hivyo kwa sababu gani? Siyo rahisi sana vijana kuandika barua kule waliko wakaifikia mifuko hiyo. Kwa hiyo, naunga mkono

lile tamko la awali kwamba tuiunganishe mifuko hiyo, iongezewe fedha hata kama na halmashauri au na bajeti ili vijana wengi zaidi wafaidike kuliko ilivyo sasa, kwamba unaanza kupiga simu unaulizwa, unapiga kama nani? Napiga kama mwakilishi. Hapana, kijana mwenyewe alete barua, kijana mwenyewe alete kitambulisho cha *NIDA*. Mlolongo, *red tape* hizo na *bureaucracy* zimekuwa ndefu sana. Sasa vijana wamekaa mitaani wanakata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jambo moja, kuna maeneo ambayo wamekuwa wengi lakini eneo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Raymond. Ni kengele ya pili.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nashon William Bidya, halafu tutaongeza muda kidogo ili Mheshimiwa Kawawa awe mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Kwanza naomba nimpongeze yeye mwenyewe kwa jinsi ambavyo aliweza kuwasilisha vizuri. Pia niwapongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Naibu Mawaziri kwa jinsi wanavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi anayoendelea kuifanya katika majimbo yetu ambapo kwa kweli ni tofauti na ilivyokuwa miradi mingi sana ya maendeleo kama vile maji, afya na elimu. Kwa kweli tunaendelea kuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye eneo la umeme wa *REA*. Umeme wa *REA* ulikuja kwa lengo moja la kuwasaidia kule vijijini, kuhakikisha kwamba wanajikwamua na maendeleo. Pamoja na kuutumia kuwasha kwenye nyumba zao, lakini utafanya kazi kuwawezesha vijana kujikimu katika kuhakikisha wanatumia ule umeme uwasaidie kupata kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba Serikali inaendelea kupeleka umeme kwenye vijiji vyetu na baadhi ya vitongoji, lakini bado katika vijiji vyenyewe kuna maeneo hayajapelekewa umeme. Mbaya zaidi ni kwenye baadhi ya vijiji ambavyo Serikali ilivitambua kama ni miji ambayo nayo haijawa miji, bado ni mamlaka ya vijiji. Kwa mfano, Nguruka na pia pale Kijiji cha Uvinza, hivi ni vijiji kama vijiji vingine. Ni Mamlaka za Vijiji kama vijiji vingine, lakini vijiji hivi viliamriwa kutoa shilingi 320,000 kama mijini. Sasa ni kitu ambacho kiliwanyong'onyeza sana na mpaka sasa hakuna mtu ambaye ameshalipia hiyo shilingi 320,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelalamika sana hapa Bungeni kwenye Wizara ya Nishati ili waweze kuondolewa kwenye eneo hilo la shilingi 320,000 ambayo ni *rate* ya mji, wakati wao sio mji. Maana yake inapingana na ile ya kuhakikisha kwamba vijiji vyote vinapelekewa umeme na wananchi wanaweka umeme ili waweze kuutumia kwa maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kwenye eneo hilo la Nguruka pamoja na Uvinza, kwa kweli nina imani na vijiji vingine katika nchi hii viko ambavyo vilipelekwa kwenye *tariff* hiyo ya mjini, waweze kuviondoa huko ili wananchi waweze kuanza kulipa shilingi 27,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Serikali, pale tuliposhuhudia utiaji wa saini katika mradi wa umeme wa maji *Igamba Falls* kwenye Jimbo langu Uvinza kwa lengo la kupata *Megawatts* 49.5. Mradi ule ni wa miaka mingi sana na ulizungumziwa sana hapa Bungeni kabla sijawa Mbunge. Nampongeza

Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kurudisha mradi huu na umeweza kusainiwa, na mkandarasi sasa anatarajiwa kwenda kuanza kazi. Kwa sasa hivi, mkandarasi ambaye anajenga njia ya kusafirisha umeme kutoka hapo *Igamba Falls* kwenda Kidawe, alishaanza kujenga njia ya kusafirisha umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili naomba niwahakikishie kwamba, inaanza kuwaonesha wananchi wa Mkoa wa Kigoma kwamba sasa mkoa unafunguka kwenye eneo hilo la nishati ya umeme. Naomba wakati mkandarasi anaendelea kujenga hiyo njia ya umeme, mweze kuhakikisha kwamba wananchi ambao watapitiwa na njia hiyo ya umeme wanalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nizungumzie kwenye eneo la barabara ya Simbo - Kalya. Barabara hii ina urefu wa kilometa 235, ni barabara ndefu sana. Ni barabara ambayo inahusu kata nane za Jimbo la Kigoma Kusini za Wilaya ya Uvinza ambao ni ukanda wa maji. Wananchi hawa kabla barabara hii haijafunguliwa walikuwa wakisafiri na maboti na wengi walikufa sana majini na wengi walipoteza mizigo yao mingi. Sasa baada ya barabara hii kufunguliwa, kwa kweli naomba niipongeze *TANROADS,* wanaendelea kuifanyia kazi vizuri sana barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya barabara hii kufunguliwa, wananchi wa hizo kata nane walipata ukombozi. Kwenye barabara hiyo nakumbuka Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Kasekenya aliwahi kupita mara mbili. Naomba nichukue nafasi hii nimshukuru, anapenda sana kuwa anapita kwenye hiyo barabara, anaijua, alitoa maelekezo ya barabara hiyo iweze kuwekewa zege katika maeneo korofi na kwa kweli Mheshimiwa Naibu Waziri, hili jambo likifanyika litaweza kusaidia kabla barabara hii haijawekewa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwenye eneo la Kivuko pale Ilagara. Daraja hili liko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na tayari Serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya

upembuzi yakinifu. Taarifa nilizonazo ni kwamba, huyu mkandarasi wa upembuzi yakinifu alishamaliza kazi, lakini bado kuna fedha kidogo anaidai Serikali ili aweze kuikabidhi hiyo *document*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iweze kumlipa fedha zake ili aweze kuikabidhi *document* hiyo ili hilo daraja lianze kujengwa. Wananchi wa kata nane wanahitaji daraja. Juzi kivuko kilisombwa na maji kwa sababu maji ya Mto Malagarasi ni mengi na yanatembea kwa kasi sana. Pia pale ndiyo mwishoni na mto ule ni mrefu sana, unaanzia huko Kibondo, lakini unapofika pale ni mpana na maji ni mengi, yalisomba kivuko kile na watu wakiwemo ndani pamoja na magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitsha zaidi, kwa sababu barabara ile ndiyo inakwenda kule kwenye eneo la Buhigu ambako kuna *TANAPA,* kuna watalii walikuwemo kwenye ile gari na magari yao ambayo yalikuwa yanapelekwa kule, bahati mbaya sana kwa kweli walisombwa kupelekwa kwenye maji mengi (ziwani) na wamekaa kule mpaka jioni. Hata hivyo, naishukuru Serikali ya Mkoa pamoja na Wilaya walikwenda kuona namna ya kuweza kuwaokoa hao wananchi na waliweza kuwatoa na baadaye kivuko kile kurudishwa kwenye eneo lake na sasa hivi kinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wananchi hawana imani na kile Kivuko. Kwa hiyo, naomba kwenye lile daraja upembuzi yakinifu ukamilike, na Serikali ianze kuona namna ya kujenga hilo daraja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nashon.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi, baada ya kusema hayo, nakushukuru. Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa nyingine unaweza kumpelekea Waziri kwa maandishi. Mheshimiwa Vita Kawawa, ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho na naongeza muda mpaka hapo atakapomaliza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii leo ili niwasilishe ushauri wangu katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa juhudi kubwa anazozifanya kwa kushirikiana na wasaidizi wake na hadi leo hii Serikali inaendelea kufanya kazi nzuri sana ya kuboresha uchumi wetu ambao unaendelea kuwa *stable* kama unavyoendelea. Hongera sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia, hongera sana Makamu wa Rais, hongera sana Waziri Mkuu na hongera sana Mawaziri wote kwa kufanya kazi nzuri hii ya kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani pia kwa Serikali kwa kutupatia mbolea ya ruzuku kwenye msimu huu. Msimu huu utaratibu wa pembejeo ulikwenda vizuri sana. Wakulima walipata pembejeo kwa ruzuku na siyo kama msimu uliopita ambapo tulipata shida sana kuzipata mbolea za ruzuku. Hivyo basi, wakulima wamelima vizuri na mazao mazuri yako mashambani, na kwa sisi wakulima wa mahindi, yapo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakwenda kwenye masoko. Tunaiomba Serikali, sisi dira yetu kwa bei ya zao la mahindi ni *NFRA*. Kwa hiyo, tunaiomba sana Wizara ya Kilimo itangaze mapema soko la ununuzi wa mahindi, kwani yenyewe ndiyo inachukua dira ya bei kwa zao hili la mahindi. Tutashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kule kwetu Namtumbo hatuna stendi yenye hadhi. Tuna njia tu ya kupitishia mabasi na kuondoka. Mwaka 2023 niliomba Serikali katika vipindi vya Bunge hapa kwamba tujengewe na Serikali kwa sababu mapato yetu ni ya chini sana na hatuna uwezo wa kujenga stendi ya mabasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitujibu kwamba, halmashauri iandike andiko ili iweze kuleta TAMISEMI ndiyo Serikali iweze kuichukua na kuifanyia kazi kutusaidia kujenga stendi yetu. Kwa hiyo, ni lalamiko letu kubwa sana kuwa hatuna stendi. Naikumbusha tena Serikali kuwa andiko letu tumeshaandika, basi tunaomba tujengewe stendi yetu pale Mji wa Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni wanyama waharibifu hususan tembo. Mwenzangu Mbunge wa Tunduru amezungumza hapa kuhusu tembo. Ni kweli sisi tumepakana na Selous, vijiji vyetu tunapata shida sana ya tembo. Tembo wanaua watu wetu. Juzi mwezi mmoja uliopita walimuua mama mmoja alikuwa anakwenda shambani. Vilevile, siku za nyuma waliua katika Kijiji cha Nambecha, pia waliua katika Kijiji cha Mputa na hii juzi waliua pale katika Likuyuseka. Hata hivyo, tembo wanatamba sana katika mashamba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wetu ni watu wa hali ya chini, wanategemea uchumi wao kwa kulima ekari zao chache, lakini zote zinaliwa na tembo. Leo hii tembo ndiyo anatuvuruga kabisa kiuchumi katika Wilaya yetu ya Namtumbo pamoja na Tunduru. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali itumie weledi wake kuzia hawa tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi babu yangu Mfaume Ali Kawawa, alikuwa *Game Officer* toka miaka hiyo ya 1919/1920 mpaka baba yangu anazaliwa mwaka 1926, alimzaa akiwa porini wakiwa wanasaka na kuzuia tembo. Yeye alipewa jina la Kawawa kwa sababu ya ufundi…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa, sema vizuri, nani alizaliwa na tembo? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, babu yangu akiwa anafanya kazi ya kuzuia tembo waharibifu wasiharibu kwenye vijiji miaka ya 1920 na kitu, mwaka 1930 aliteuliwa kuwa *Game Officer* wa Selous, akapelekwa Liwale. Wakati huo hawakuwa na

magari, walitembea kwa miguu. Waliweza kudhibiti tembo wakati huo na walikuwa tembo wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tuna wasomi wengi wanasomea *behavior* za wanyama hawa, tuna teknolojia na tuna magari, tunashindwaje kuwazuia tembo kufanya uharibifu? Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali itumie weledi wake ili kuzuia hawa tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, historia niliyokuwa nayo, tembo wakienda kwenye kijiji wakifanya vurugu, babu yangu alikuwa anakwenda anakaa kuwa-*study* siku tatu tu, halafu anampiga tembo huyu mmoja, wote wanaondoka pale na hawarudi tena. Leo hii tunazuia, ndiyo; kuna Sheria mbalimbali za kuzuia kuwapiga tembo, lakini lazima tuwapunguze wale waharibifu na kidogo kidogo hawatarudi tena. Tembo hawa wanaua, wanaharibu vyakula na kadhalika. Kwa hiyo, tunaomba sana kwenye eneo hili la tembo Serikali ilichukue kwa sababu ina weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni miradi viporo katika halmashauri zetu. Halmashauri yetu ya Namtumbo tuna miradi mingi ya nyuma ambayo ni viporo. Tunaishukuru sana Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kutujengea madarasa na vituo vya afya. Kwangu tumejenga vituo vitatu vya afya na madarasa 86. Pia, tumejenga na kuongeza madarasa katika shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna shida ya miradi viporo ya nyuma ambayo haijakamilika. Sasa haiwezi kuendelea kukaa kama maboma. Tunaiomba na kuishauri Serikali itenge fedha za kukamilisha miradi hii viporo ili twende kama ilivyokusudiwa. Miradi hii ilijengwa kwa nguvu za wananchi na Serikali ilisema itakuja kumalizia kwa vifaa vya viwandani, lakini mpaka leo ipo haijajengwa. Wakati ni huu, tunaomba sasa tuweze kujenga na kukamilisha miradi viporo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule kwetu tuna mradi wa Urani. Nchi yetu tunahitaji fedha na tunahitaji kupunguza gharama za

uendeshaji kwa kupata mapato. Mradi wa Urani ni moja ya mradi ambao utatusaidia sana katika kuingiza mapato. Leo nilikuwa naangalia hapa katika hotuba ya Waziri wa Fedha aliyoitoa kwenye Bunge, alizungumzia mikopo aliyokopa karibu shilingi trilioni 2.7. shilingi trilioni 1.7 tumelipia hati fungani, lakini shilingi trilioni moja tumelipia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kupunguza mikopo hii maana yake lazima tuwe na miradi ya uzalishaji. Sasa sisi tunao mradi wa Urani ambapo kuna urasimu na hatuelewi. Wanasema mara inafanyika *strategic environment assessment,* sijui inafanyika lini? Mradi ule hauanzi mpaka leo na urani imepanda bei. Leo ile wakia moja ni dola 72. Duniani sasa hivi kuna viwanda au vinu 57 vinajengwa kwa ajili ya kutaka kuzalisha umeme hasa nchi za Ulaya. Kwa hiyo, kwetu sisi urani ni soko mojawapo kubwa sana. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali imalize urasimu ili ule mradi wa urani uweze kuanza kule Mkuju wilayani Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni tumbaku. Tumbaku inalimwa kwa mkataba na mkataba wenyewe ni kwa dola. Sasa Serikali katika uboreshaji wa biashara, tumepata mikataba ya kuzalisha tani nyingi sana za tumbaku, lakini tuna changamoto ya pembejeo kuwa ghali sana kwenye uzalishaji. Tunaomba Serikali itupatie ruzuku kwenye zao la tumbaku. Kwa sababu kwanza inauzwa kwa dola, nasi tuna shida ya dola, lakini tuna mkataba wa kuzalisha tani nyingi sana za tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wanashindwa kulima mashamba mengi au ekari nyingi kwa sababu hawana uwezo wa kununua mbolea ya *NPK* ambayo haina ruzuku. Kwa hiyo, sisi tunaomba tumbaku ipate mbolea ya ruzuku. Leo wenzetu wa korosho wanapata ruzuku au pembejeo yao bure. Sisi tumbaku tunanunua bila ruzuku. Tunaomba Serikali isitugawe, sote tunazalisha kwa ajili ya wananchi na nchi hii. Tunaomba tumbaku nayo ipate ruzuku katika uzalishaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yetu ya leo imekwisha. Nawaomba Wabunge wote mnaotaka kuchangia Wizara zinazokuja pamoja na hii, mjaze na mtumie mtandao wa Bunge kuomba nafasi za kuchangia. Pale Mbunge anapopata changamoto awasiliane na watu wa TEHAMA wa Bunge, watakusaidia kusajili jina lako kwenye mtandao.

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia na kuwakumbusha tena, leo Benki ya *NMB* imeandaa *Iftar* maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge. *Iftar* hii itafanyika katika viwanja vya Bunge siku ya Alhamisi ambayo ndiyo leo kuanzia saa 12.00 jioni. Tunawasihi na kuwaomba Wabunge wote, watumishi wote na waalikwa wote kuhudhuria shughuli hii muhimu ambayo itafanyika katika viwanja vyetu leo.

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.12 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 5 Aprili, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*